# Kiswahili

## Shule za Sekondari

### Kitabu cha Mwanafunzi

**Kidato cha Nne**



Taasisi ya Elimu Tanzania

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*

# KISWAHILI

## Shule za Sekondari

### Kitabu cha Mwanafunzi

### Kidato cha Nne


JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
WIZARA YA ELIMU, SAYANSI
NA TEKNOLOJIA

*Cheti cha Ithibati*

Na. 750

Jina la Chapisho: Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Nne

Mchapishaji: Taasisi ya Elimu Tanzania

Mwandishi: Taasisi ya Elimu Tanzania

ISBN: 978-9987-09-396-0

Kitabu hiki kimeidhinishwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia tarehe 2 Machi, 2022 kuwa Kitabu cha Kiada kwa ajili ya Mwanafunzi wa Kidato cha Nne katika ngazi ya Elimu ya Sekondari nchini Tanzania kulingana na Muhtasari wa mwaka 2005.

Dkt. Lyabwene M. Mtahabwa
Kamishna wa Elimu

Taasisi ya Elimu Tanzania

KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 1 07/03/2022 16:49

© Taasisi ya Elimu Tanzania 2022

Kimechapishwa 2022

ISBN: 978-9987-09-396-0

Taasisi ya Elimu Tanzania
S.L.P. 35094
Dar es Salaam - Tanzania

Simu: +255735041168
+255735041170

Baruapepe: director.general@tie.go.tz

Tovuti: www.tie.go.tz

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kunakili, kurudufu, kuchapisha, kutafsiri, wala kutoa kitabu hiki au sehemu yake kwa namna yoyote ile bila idhini ya maandishi ya Taasisi ya Elimu Tanzania.

# Yaliyomo


**Orodha ya Vielelezo** ........ v

**Vifupisho** ........ vi

**Shukurani** ........ vii

**Dibaji** ........ viii

**Sura ya Kwanza: Uundaji wa maneno** ........ 1

Dhana ya uundaji wa maneno ........ 1

Mambo yanayosababisha kuhitajika kwa maneno mapya ........ 2

Njia za uundaji wa maneno ........ 3

Umuhimu wa kuunda maneno ........ 9

Zoezi la marudio ........ 11

**Sura ya Pili: Kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi ya Waingereza na baada ya uhuru** ........ 13

Kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi ya Waingereza ........ 13

Kukua na kuenea kwa Kiswahili baada ya uhuru ........ 19

Zoezi la marudio ........ 23

**Sura ya Tatu: Uhakiki wa kazi za fasihi andishi** ........ 26

Dhana ya uhakiki ........ 26

Kuhakiki kazi za ushairi ........ 30

Kuhakiki tamthiliya ........ 42

Kuhakiki riwaya ........ 54

Zoezi la marudio ........ 61

**Sura ya Nne: Utungaji wa kazi za fasihi** ........ 63

Dhana ya utungaji ........ 63

Kutunga mashairi ya kimapokeo ........ 65

Zoezi la marudio ........ 69




KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 3 07/03/2022 16:49

**Sura ya Tano: Uandishi ....................................................................71**
Dhana ya uandishi....................................................................................71
Kuandika insha .......................................................................................73
Kuandika hotuba .....................................................................................81
Kuandika risala .......................................................................................85
Kuandika kumbukumbu za mikutano ......................................................89
Zoezi la marudio .....................................................................................97
**Sura ya Sita: Ufahamu ....................................................................100**
Dhana ya ufahamu ...................................................................................99
Ufahamu wa kusikiliza ..........................................................................100
Ufahamu wa kusoma..............................................................................103
Ufahamu wa kuona ................................................................................110
Zoezi la marudio ....................................................................................111
**Faharasa.................................................................................................114**
**Bibliografia ...........................................................................................118**



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 4 07/03/2022 16:49

# Orodha ya Vielelezo

Kielelezo Na. 3.1: Vipengele vya uhakiki wa fasihi andishi ............................................28



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 5 07/03/2022 16:49

# Vifupisho

| | |
|---|---|
| ASP | Afro Shiraz Party |
| AZISE | Asasi Zisizo za Serikali |
| BAKITA | Baraza la Kiswahili la Taifa |
| BASATA | Baraza la Sanaa la Taifa |
| CHAKIZA | Chama cha Kiswahili Zanzibar |
| CHALUFAKITA | Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania |
| CKD | Chuo Kikuu cha Dar es Salaam |
| CMS | Church Missionary Society |
| CWT | Chama cha Walimu Tanzania |
| DUCE | Dar es Salaam University College of Education |
| EALB | East African Literature Bureau |
| LUKU | Lipia Umeme Kadiri Unavyotumia |
| MKUKUTA | Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania |
| MNMA | Mwalimu Nyerere Memorial Academy |
| MU | Mzumbe University |
| SKILUKI | Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni |
| TAKILUKI | Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni |
| TANU | Tanganyika African National Union |
| TATAKI | Taasisi ya Taaluma za Kiswahili |
| TET | Taasisi ya Elimu Tanzania |
| TUKI | Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili |
| UDOM | University of Dodoma |
| UKIMWI | Upungufu wa Kinga Mwilini |
| UKUTA | Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania |
| UWAVITA | Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania |



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 6 07/03/2022 16:49

# Shukurani

Taasisi ya Elimu Tanzania (TET) inatambua na kuthamini michango ya washiriki waliofanikisha uandishi wa kitabu hiki cha Kiswahili Shule za Sekondari Kidato cha Nne. Pia, TET inatoa shukurani kwa taasisi zote za umma na za binafsi zilizoshiriki kwa namna moja ama nyingine katika kufanikisha uandishi wa kitabu hiki. Taasisi hizo ni Chuo Kikuu cha Dar es Salaam (CKD), Chuo Kikuu cha Dar es Salaam - Chuo Kishiriki cha Elimu Dar es Salaam (CKD - DUCE), Chuo cha Kumbukumbu ya Mwalimu Nyerere (MNMA), Chuo Kikuu cha Dodoma (UDOM), Chuo Kikuu Mzumbe (MU), na Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA). Aidha, TET inatoa shukurani kwa vyuo vya ualimu, Idara ya Uthibiti Ubora wa Shule, na shule za sekondari.

Kipekee, TET inatoa shukurani za dhati kwa michango iliyotolewa na wataalamu wafuatao:

**Waandishi:** Bi. Razia Y. Shemlugu, Bi. Aurelia F. Mutajunwa, Bi. Sarah O. Msafiri, Bw. Jivitius C. Sabatho, Bw. Jailan M. Hafidhi, Prof. Kulikoyela K. Kahigi, na Dkt. Rose J. Mbijima

**Wahariri:** Dkt. Titus M. Ngeme (CKD), Dkt. Adventina Y. Buberwa (CKD), Dkt. Luinasia E. Kombe (CKD - DUCE), Dkt. Athumani S. Ponera (MNMA), Dkt. Mussa M. Hans (CDK), na Bw. Mussa R. Kaoneka (BAKITA)


**Msanifu:** Bw. Kuyonza K. Kuyonza

**Wachoraji:** Bi. Rehema H. Magaga na Alama Art and Media Production Co. Ltd

**Mratibu:** Bi. Aurelia F. Mutajunwa

Pia, TET inatoa shukurani kwa walimu na wanafunzi wa shule za sekondari walioshiriki katika hatua ya ujaribishaji wa muswada wa kitabu hiki.

Aidha, TET inatoa shukurani za pekee kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia kwa kuwezesha uandishi na uchapaji wa kitabu hiki.



Dkt. Aneth A. Komba
Mkurugenzi Mkuu
Taasisi ya Elimu Tanzania



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 7 07/03/2022 16:49

# Dibaji

Kitabu hiki ni cha nne katika mfululizo wa vitabu vinne vya Somo la Kiswahili kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne kilichoandaliwa mahususi kwako mwanafunzi wa Kidato cha Nne wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Kitabu hiki kimeandaliwa kwa kuzingatia Muhtasari wa Somo la Kiswahili wa mwaka 2005 uliotolewa na iliyokuwa Wizara ya Elimu na Utamaduni. Maudhui yaliyomo katika kitabu hiki ni mwendelezo wa yale yaliyomo katika kitabu cha Kiswahili Kidato cha Tatu.

Kitabu hiki kimegawanyika katika sura sita ambazo ni: Uundaji wa maneno, Kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi ya Waingereza na baada ya uhuru, Uhakiki wa kazi za fasihi andishi, Utungaji wa kazi za fasihi, Uandishi, na Ufahamu. Maudhui ya kitabu hiki yamewasilishwa kwa njia ya matini, maswali, kazi za kufanya, vielelezo, na picha ambazo zinachochea ujenzi wa umahiri unaokusudiwa katika kila sura. Vilevile, kila sura ina mazoezi yenye lengo la kujenga na kupima uelewa pamoja na ujuzi katika somo hili. Hivyo, unapaswa kufanya mazoezi na kazi zote zilizomo katika kitabu hiki na kazi zingine utakazopewa na mwalimu.

**Taasisi ya Elimu Tanzania**

# Sura ya Kwanza

## Uundaji wa maneno

**Utangulizi**

*Kuna njia mbalimbali za uundaji wa maneno katika lugha ya Kiswahili kama zilivyo lugha zingine. Maneno mapya huundwa ili kukidhi haja ya mawasiliano. Katika sura hii, utajifunza njia hizo za uundaji wa maneno, sababu za kuhitajika kwa maneno mapya katika lugha, na umuhimu wa kuunda maneno mapya. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kubaini namna maneno yanavyoundwa katika lugha ya Kiswahili na mambo yanayosababisha kuhitajika kwa maneno mapya.*

### Dhana ya uundaji wa maneno

**Kazi ya 1.1**

**Chunguza picha zifuatazo, kisha jibu maswali yanayofuata.**



### Maswali

1. Andika jina la kila picha uliyoichunguza.
2. Eleza namna maneno uliyoyabainisha katika swali la 1 yalivyopatikana.
3. Pendekeza maneno mengine matano yanayofanana kimuundo na yale uliyoyabainisha katika swali la 1.
4. Kwa nini lugha huhitaji maneno mapya?

**Zingatia**

Hakuna lugha inayojitosheleza kimsamiati. Hivyo, kila lugha huhitaji maneno mapya ili kukidhi mahitaji ya mawasiliano. Mahitaji ya maneno mapya huongezeka kadiri mabadiliko yanavyotokea katika jamii. Kutokana na mabadiliko hayo, lugha huhitaji kuongeza msamiati wake. Mchakato au utaratibu wa kuongeza maneno mapya katika lugha ndio huitwa uundaji wa maneno.

## Mambo yanayosababisha kuhitajika kwa maneno mapya

### Kazi ya 1.2

Soma maandiko mbalimbali kuhusu uundaji wa maneno, kisha bainisha mambo yanayotajwa kuchochea uundaji wa maneno mapya.

**Zingatia**

Kuna mambo kadhaa yanayosababisha lugha ihitaji maneno mapya ili kukidhi haja ya mawasiliano. Jambo mojawapo ni mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia. Lugha huhitaji maneno mapya ili kukidhi dhana mbalimbali zinazovumbuliwa au kuibuka kutokana na mabadiliko hayo. Kwa mfano, maneno kama **satelaiti**, **dijiti**, na **tovuti** yameundwa kutokana na maendeleo ya sayansi na teknolojia. Pia, mabadiliko ya kiuchumi huchochea kuhitajika kwa maneno mapya katika lugha ili kukabiliana na mabadiliko hayo. Kwa mfano, maneno kama **chenji**, **kodi**, na **hisa** yameundwa kutokana na mabadiliko ya kiuchumi. Vilevile, mabadiliko ya kisiasa husababisha kuhitajika kwa maneno mapya katika lugha. Kwa mfano, wakati wa ukoloni, kulikuwa na maneno kama **liwali**, **akida**, na **jumbe** na baada ya ukoloni kukawa na maneno kama **bunge**, **diwani**, na **ufisadi**. Pia, katika kipindi cha siasa ya Ujamaa na Kujitegemea, kuliibuka maneno kama **kupe**, **kabwela**, **magendo**, na **bwanyenye**.

Kadhalika, shughuli za kijamii, mabadiliko ya tabianchi, na matukio kama vita, magonjwa, mafuriko, na njaa yanapotokea hupewa majina ili lugha husika iweze kuendana na mabadiliko na matukio hayo. Mfano wa maneno yaliyotokea kutokana na matukio yaliyosababishwa na mabadiliko ya tabianchi ni **elininyo** na **sunami**.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 2 07/03/2022 16:49

Aidha, mwingiliano wa kiutamaduni huweza kuchochea kuhitajika kwa maneno mapya. Kwa mfano, maneno kama **sketi**, **shati**, **chipsi**, na **supu** yametokana na mwingiliano wa kiutamaduni baina ya Waingereza na Waswahili.

Kwa ujumla, hayo ni baadhi ya mambo yanayosababisha lugha ihitaji maneno mapya.

## Zoezi la 1.1

1. Chunguza mambo yafuatayo, kisha eleza namna yanavyochochea uundwaji wa maneno mapya katika lugha.
   (a) Mabadiliko ya kisayansi na kiteknolojia
   (b) Mabadiliko ya kiuchumi
   (c) Mabadiliko ya kisiasa
   (d) Mabadiliko ya kijamii
   (e) Mabadiliko ya tabianchi
2. Orodhesha maneno manne yanayotokana na kila aina ya mabadiliko yaliyotajwa katika swali la 1, bila kurudia mifano iliyotajwa katika sura hii.

## Njia za uundaji wa maneno

## Kazi ya 1.3

**Soma mazungumzo yafuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Mwandishi**: (*Baada ya kufika kwenye mlango wa ofisi ya mwalimu wa somo la Kiswahili, anabisha hodi.*) Ngo ngo ngo! Hodi!

**Mwalimu**: (*Anaitikia huku akipanga mafaili.*) Karibu!

**Mwandishi:** Asante! Habari za leo mwalimu?

**Mwalimu:** Nzuri, karibu kiti!

**Mwandishi:** (*Anaketi, kisha anaeleza sababu iliyomleta.*) Kama tulivyokwishazungumza mapema kwa njia ya simu, nia yangu ni kutaka kujua namna maneno mapya ya Kiswahili yanavyoundwa. Hii ni kwa sababu tunaona maneno mapya yakiongezeka katika lugha ya Kiswahili. Hivyo, lengo langu ni kuandika makala katika gazeti la *Mwalimu wa Leo* ili kuelimisha umma kuhusu njia za uundaji wa maneno.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 3 07/03/2022 16:49

**Mwalimu:** (*Anacheka kidogo.*) Ha ha ha! Ni kweli maneno mapya huongezeka kwenye lugha kutokana na mabadiliko yanayotokea katika jamii. Wazo lako la kuchapisha makala inayohusu uundaji wa maneno katika gazeti hilo ni zuri. Tutanunua nakala kadhaa ili ziwasaidie walimu na wanafunzi.

**Mwandishi:** (*Huku akitikisa kichwa kuashiria kukubaliana naye*) Naam! Miongoni mwa kazi zangu ni kueneza maarifa.

**Mwalimu:** Sawa, tuanze. (*Mwandishi anashika kalamu na daftari, kisha mwalimu anaanza kuzungumza.*) Tunaposema "uundaji wa maneno," tuna maana ya utaratibu wa kuzalisha maneno kwa kufuata kanuni za lugha inayohusika. Utaratibu huu hutumika kuzalisha maneno mapya endapo kuna mahitaji, hasa dhana mpya zinapoingia katika jamii.

**Mwandishi:** (*Huku akitabasamu kidogo*) Ahaaa! Kumbeee … Nimekuelewa mwalimu. Tuendelee.

**Mwalimu:** Vema sana! Kuhusu njia mbalimbali za uundaji wa maneno, kuna wanafunzi waliojiandaa kueleza njia hizo. Nitawaita sasa hivi ili wajibu maswali yako.

**Mwandishi:** Hakuna shida kabisa mwalimu. Nitafurahi kusikia maelezo ya wanafunzi.

**Mwalimu:** Sawa! (*Mwalimu anamwita mwanafunzi aitwaye Fifi aliyekuwa akipita karibu na ofisi ya mwalimu. Fifi anaingia.*) Kaniitie wale wanafunzi wa kidato cha nne waliojiandaa kwa mada ya uundaji wa maneno. *(Fifi anakimbia upesi kuelekea alikoagizwa.)*

**Wanafunzi**: (*Wanafunzi wanane wanaingia ofisini.*) Shikamooni!

**Mwalimu na Mwandishi:** Marahaba! (*Wanajibu kwa pamoja.*)

**Mwalimu:** (*Huku akimtazama mwandishi*) Hawa ni wanafunzi wa kidato cha nne. Wamejifunza uundaji wa maneno. Watakuelezea namna maneno ya Kiswahili yanavyoundwa. Kila mwanafunzi ataeleza njia moja ya uundaji wa maneno. Baadaye, unaweza kuwahoji kwa maelezo zaidi iwapo kuna mahali utakuwa hujaelewa.

**Mwandishi:** Sawa mwalimu! Niko tayari kuwasikiliza. (*Anachukua kalamu na daftari, akiwa tayari kuanza kuandika.*)



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 4 07/03/2022 16:49

**Mwalimu:** (*Akiwatazama wanafunzi*) Huyu ni mwandishi wa gazeti la *Mwalimu wa Leo*. Anataka kuandika makala kuhusu uundaji wa maneno. Ninaamini mko tayari kumwelezea njia za uundaji wa maneno.

**Wanafunzi:** (*Wote kwa pamoja*) Ndiyo mwalimu!

**Mwalimu:** Sasa mnaweza kuanza.

**Mwanafunzi wa 1**: Mimi ninaitwa Maganga. Nitaelezea njia ya *unyambulishaji*. Unyambulishaji ni upachikaji wa viambishi kwenye mzizi wa neno unaobadilisha maana, hali au aina ya neno. Unyambulishaji huweza kufanyika kwa kuongeza kiambishi mwanzoni au mwishoni mwa mzizi wa neno. Kwa mfano, mzizi **som**- wa neno **soma** ukiongezwa kiambishi **m-** mwanzoni na kiambishi **-i** mwishoni unatupatia neno **msomi**. Katika unyambulishaji, nomino huweza kuzalishwa na mizizi ya vitenzi au mashina ya vivumishi. Kwa mfano, tunaweza kuzalisha nomino **somo**, **msomi**, na **msomaji** kutoka kwenye kitenzi **soma** chenye mzizi **som-** kwa kupachika viambishi **m-**, **-o**, **-i**, na ***-aji*** kwenye mzizi huo. Unyambulishaji unaohusu vitenzi ni mpana na umechangamana zaidi kwani unahusisha viambishi vingi zaidi. Kwa mfano, kitenzi **kata** kinaweza kuwa **katana**, **katika**, **katwa**, na kitenzi **sema** kinaweza kuwa **semea**, **semesha**, **semana**, **semeka**, au **semwa**. Katika mifano hii, viambishi vilivyopachikwa ni **e-**, **-esh**, **-an-**, **-ek-**, **-ik-**, na **-w-**. Vilevile, tunaweza kuzalisha nomino kwa kutumia mashina ya vivumishi kwa kupachika kiambishi **u-** kwenye shina. Pia, vivumishi vinaweza kuzalishwa katika Kiswahili kwa kutumia viambishi. Kiambishi kimojawapo ni **-fu**/**-vu**. Mifano ya vivumishi vinavyotokana na upachikaji wa kiambishi -fu/-vu ni **adilifu** (kutokana na **adili**), **changamfu** (kutokana na **changamka**), **kakamavu** (kutokana na **kakamaa**), pamoja na **shupavu** (kutokana na **shupaa**).

**Mwalimu:** Vizuri! Haya, anayefuata!

**Mwanafunzi wa 2**: Jina langu ni Katambi. Njia nitakayoelezea ni *uambatanishaji*. Hii ni njia ya kuunganisha maneno tofauti ili kupata neno moja. Maneno hayo yanaweza kuwa mawili au zaidi. Maneno yanayozalishwa kutokana na njia hii yanaitwa maneno ambatani. Mifano ya maneno ambatani ni **batamzinga**, **mwanajeshi**, **mwananchi**, **mwanaharamu** na **bwanashamba**.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 5 07/03/2022 16:49

**Mwalimu:** Vyema, anayefuata!

**Mwanafunzi wa 3**: Ninaitwa Taboa. Nitaelezea njia ya *ufananisho*. Hii ni njia ya kuunda maneno kwa kuiga mlio wa chombo au kitu husika, kufananisha kitu na kazi yake au kitu na umbo lake. Kwa mfano, neno **mtutu** limetokana na mlio wa bunduki. Vilevile, neno **kengele** limetokana na mlio wa kengele, na neno **kipimajoto** limetokana na kazi ya kifaa hicho.

**Mwalimu:** Vizuri! Anayefuata ni nani?

**Mwanafunzi wa 4**: Jina langu ni Limuli. Nitaelezea njia ya *urudufishaji* au *uradidi*. Hii ni njia ya kuunda maneno kwa kurudiarudia neno zima au sehemu ya neno. Kwa mfano, neno **takataka** limetokana na kurudiwa kwa neno zima **taka**. Neno **kizunguzungu** limetokana na kurudiwa kwa sehemu ya neno **zungu**. Mifano mingine ya maneno yanayotokana na uradidi ni **teketeke**, **chepechepe**, **chapachapa**, **chapuchapu**, **kinyumenyume**, **kiwiliwili**, **kichefuchefu** na **kimbelembele**. Urudufishaji unahusu aina nyingi za maneno katika lugha ya Kiswahili. Miongoni mwa aina hizo ni vitenzi. Vitenzi vingi vinakubali utaratibu huu. Mifano ya vitenzi vya aina hiyo ni **pigapiga**, **chekacheka**, **limalima**, **semasema**, na **kimbiakimbia**.

**Mwalimu:** Vyema! Mwingine aendelee.

**Mwanafunzi wa 5**: Mimi ni Lugendo. Nitaeleza njia ya *ufupishaji*. Njia hii huhusisha uchukuaji wa herufi au silabi za mwanzo za jina refu lenye muundo wa kirai au kikundi kirai, na kuunda neno kwa kuunganisha herufi au silabi hizo. Mifano ya maneno yaliyofupishwa ni **TET** (Taasisi ya Elimu Tanzania), **CKD** (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), **UKUTA** (Usanifu wa Kiswahili na Ushairi Tanzania), na **UKIMWI** (Upungufu wa Kinga Mwilini).

**Mwalimu:** Safi! Mwingine aendelee.

**Mwanafunzi wa 6**: Jina langu ni Chaupele. Nitaelezea njia ya *kukopa*. Hii ni njia ya kuchukua maneno kutoka katika lugha nyingine na kuyaingiza katika lugha inayokopa ili

kukidhi mahitaji ya mawasiliano. Maneno ya mkopo katika Kiswahili ni mengi. Mifano ni **redio**, **benki**, **data**, na **delta** (kutokana na Kiingereza). Mengine ni **abiri**, **dalili**, **madhabahu**, **darasa**, na **alfajiri** (kutokana na Kiarabu). Aidha, kuna maneno kama **kitivo**, **kipera**, **bunge**, na **ngeli** (kutoka lugha za Kibantu). Baadhi ya maneno ya mkopo hubadilishwa matamshi au tahajia ili kuendana na matamshi au tahajia ya lugha inayokopa. Kitendo cha kubadilisha matamshi au tahajia ya maneno ya mkopo ili kuendana na lugha inayokopa hujulikana kama *kutohoa*. Kwa mfano, neno **shati** limetoholewa kutokana na neno **shirt** la lugha ya Kiingereza.

**Mwalimu:** Vizuri sana! Mwanafunzi anayefuata aendelee.

**Mwanafunzi wa 7**: Jina langu ni Kenu. Nitaelezea njia ya *upanuzi wa maana*. Hii ni njia ya kuunda maneno kwa kuchukua neno lenye maana ya msingi na kulipatia maana ya ziada. Kwa mfano, maana ya msingi ya neno **tawi** ni sehemu ya mti inayoota kutoka katika shina ambalo, aghalabu, hutoa majani na, pengine, matunda. Maana ya ziada ya neno hilo ni sehemu au ofisi ndogo ya chama, shirika au asasi nyingine yoyote. Vilevile, maana ya msingi ya neno **kupe** ni mdudu mdogo ambaye anauma kwenye ngozi za wanyama na kung'ang'ania hapo ili kuwafyonza damu. Maana yake ya ziada ni mtu anayepata mapato bila kutumia jasho lake au mtu mwenye nguvu asiyefanya kazi ambaye huwategemea wengine ili aishi.

**Mwalimu:** Vizuri Kenu! Mwanafunzi wa mwisho amalizie.

**Mwanafunzi wa 8**: Mimi ni Bera. Nitaelezea njia ya *unasibu*. Hii ni njia ya kubuni maneno mapya kinasibu. Kama ilivyo kwa sauti za lugha kuwa na unasibu, baadhi ya maneno pia huundwa kinasibu. Mifano ya maneno hayo ni **kucha**, **maji**, na **paka**. Maneno haya hayana uhusiano wa moja kwa moja na vitu halisi vilivyopewa majina hayo.

**Mwalimu:** Mmeeleza vizuri sana wanafunzi wangu. Hongereni sana!

**Wanafunzi:** (*Wanaitikia kwa pamoja*.) Asante mwalimu!

**Mwalimu:** (*Anamgeukia mwandishi.*) Bila shaka, umesikia walichozungumza wanafunzi. Kama una maswali, unaweza kuwauliza.

**Mwandishi:** Ninapenda kuwashukuru nyote kwa namna mlivyonielezea vizuri njia za uundaji wa maneno. Kwa kweli, nimeelewa vizuri sana. Nikiwa na maswali, wakati wa kuandika makala yangu nitawasiliana na mwalimu kupata ufafanuzi.

**Mwalimu:** Sawa! Ninakushukuru sana kwa ujio wako. Karibu tena siku nyingine!

**Mwandishi:** Asante mwalimu! Ninawashukuru kwa kunifumbua macho kuhusiana na njia za uundaji wa maneno. Nimejifunza mengi. Nanyi wanafunzi ninawatakia masomo mema.

**Mwalimu:** (*Anawageukia wanafunzi*.) Sasa, mnaweza kurudi darasani.

**Wanafunzi:** Asante sana! (*Wanaondoka ofisini.)*

## Maswali

1. Mazungumzo uliyoyasoma yanahusu nini?
2. Kwa nini mwalimu aliwataka wanafunzi wa kidato cha nne waeleze njia za uundaji wa maneno?
3. Bainisha maneno mengine yanayoweza kuundwa kwa kutumia viambishi **-i**/**-e**, **-ish**-/-**esh**-, -**an**-, na -**w**-.
4. Bainisha njia zilizotumika kuunda maneno yafuatayo: mwanariadha, pepopunda, kiribatumbo, kipindupindu, unyevunyevu, mchezo, chajio, mwimbaji, na cherehani.
5. Ukiwa kama mwandishi uliyeenda kwa mwalimu wa Kiswahili katika shule ya sekondari kupata habari kuhusu uundaji wa maneno, andika habari yenye maneno yasiyopungua 250 kuhusu mada hiyo.

**Zingatia**

Kuna ufupishaji wa aina kadhaa: *ukatishaji*, *akronimia,* na *uhulutishaji*. *Ukatishaji* huhusisha kudondosha baadhi ya sehemu za neno na kupata neno jipya. Mifano ya *ukatishaji* ni: **shem** (badala ya **shemeji**), **prof** (badala ya **profesa**), **Dar** (badala ya Dar es Salaam). *Akronimia* ni ufupishaji wa kuchukua herufi au silabi za mwanzo wa maneno yanayounda jina na kuziunganisha kuunda neno jipya fupi ambalo



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 8 07/03/2022 16:49

linaweza kutamkika kama mfululizo wa sauti au kama neno kamili. Kwa mfano, TAKILUKI (Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni), BASATA (Baraza la Sanaa la Taifa), AZISE (Asasi Zisizo za Serikali), CKD (Chuo Kikuu cha Dar es Salaam), CWT (Chama cha Walimu Tanzania), na MKUKUTA (Mkakati wa Kukuza Uchumi na Kupunguza Umaskini Tanzania). *Uhulutishaji* ni uchukuaji wa vijisehemu vya maneno mawili au zaidi katika tungo na kuviunganisha ili kuunda neno moja. Wakati mwingine, vijisehemu vya maneno huunganishwa na neno kamili kuunda neno jipya. Kwa mfano, chajio (**cha**kula cha **jio**ni), masivina (**ma**shairi ya**si**yofuata kanuni ya **vina**), msikwao (**m**tu a**si**ye na **kwao**). Vijisehemu vya maneno vilivyokozwa wino ndivyo vilivyounganishwa kuunda maneno mapya.

### Kazi ya 1.4

(a) Soma maandiko mbalimbali kuhusu uundaji wa maneno, kisha bainisha njia za uundaji wa maneno zilizoelezwa.
(b) Taja neno moja lililoundwa kwa kila njia uliyoibainisha katika swali (a).
(c) Tunga sentensi kwa kutumia kila neno ulilolitaja katika swali (b).
(d) Orodhesha maneno matatu yaliyoundwa kwa kufananisha kitu na tabia yake.

## Umuhimu wa kuunda maneno

### Kazi ya 1.5

**Soma kisamafunzo kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Kafura ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Nisafu. Alikuwa na rafiki yake aliyeitwa Rijita. Yeye alikuwa akisoma katika shule ya jirani. Siku moja, Kafura alipokuwa akitoka shuleni, alikutana na rafiki yake. Walifurahi sana kukutana kwani walikuwa hawajaonana siku nyingi.

Katika maongezi yao, Kafura alimuuliza Rijita kuhusu walichojifunza katika somo la Kiswahili siku ile. Rijita alimjibu kuwa, katika kipindi cha somo la Kiswahili, walijifunza umuhimu wa kuunda maneno mapya katika lugha. Aliendelea kusema kwamba kipindi cha siku ile kilijibu maswali aliyokuwa nayo kwa muda mrefu. Kafura alimuuliza, "Kwani ni maswali gani uliyokuwa nayo?" Rijita alijibu, "Kwa muda mrefu, nimekuwa nikijiuliza kuhusu umuhimu wa kuunda maneno mapya katika lugha iwapo tayari lugha ina maneno yake." Aliendelea kusema kuwa alijifunza vitu vingi kwa kuwa mwalimu wao alifundisha kwa kutoa mifano ya kutosha, na alitaka kila mwanafunzi ashiriki katika ujifunzaji.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 9 07/03/2022 16:49

Kafura akasema, "Sawa! Basi na mimi ningependa kujua umuhimu wa uundaji wa maneno katika lugha." Rijita alikubali kumwelezea Kafura walichojifunza. Kafura alimsikiliza rafiki yake kwa makini ili kujua mawili matatu kuhusu uundaji wa maneno.

Rijita alianza kwa kusema, "Hoja ya kwanza unayopaswa kujua ni kuwa uundaji wa maneno huongeza au hukuza msamiati katika lugha. Maneno mapya yanapoingizwa katika msamiati wa lugha inayolengwa, husaidia msamiati wa lugha hiyo kuongezeka. Hivyo, lugha inayolengwa hukua. Hoja ya pili ni kuwa uundaji wa maneno husaidia kukidhi haja ya mawasiliano kwa watumiaji wa lugha kwa kuwa huhitaji kuwasiliana katika nyanja mbalimbali. Hivyo, huhitaji maneno yatakayoendana na mahitaji ya nyanja zinazohusika. Hoja ya tatu ni mwingiliano wa jamii zenye tamaduni tofauti ambapo huhitaji maneno yatakayoleta maelewano baina ya wanajamii hao. Kwa mfano, kutokana na mwingiliano wa tamaduni za jamii mbalimbali, Kiswahili kimepata maneno kama vile **divai** kutoka Kifaransa, **kanzu** kutoka Kiarabu, na **meza** kutoka Kireno. Hivyo, kutokana na mwingiliano huo, wanajamii hulazimika kuunda msamiati mpya kwenye lugha zao ili kukidhi mawasiliano baina yao. Kafura, rafiki yangu, hizo ni hoja za msingi na muhimu zinazobeba uzito katika kuelezea umuhimu wa uundaji wa maneno, hasa katika lugha yetu ya Kiswahili."

"Ninakushukuru sana rafiki yangu kwa kunielimisha katika hili. Kwa hakika, nimeelewa sana kwa kuwa umenifafanulia hoja vizuri. Kutokana na ufafanuzi huo, kwa sasa, ninaweza kueleza umuhimu wa kuunda maneno mapya katika lugha yetu ya Kiswahili," Kafura alisema.

## Maswali

1. Kutokana na kisamafunzo ulichokisoma, maneno *meza*, *kanzu*, na *divai* yameundwa kwa njia gani?
2. Andika maneno mengine matatu yaliyoundwa kwa njia uliyoibainisha katika swali la 1.
3. Taja njia zingine tano za uundaji wa maneno tofauti na ile uliyoibainisha katika swali la 1.
4. Kuna umuhimu gani wa kuunda maneno mapya katika lugha?
5. Eleza namna mwingiliano wa tamaduni za jamii tofauti unavyochochea kuhitajika kwa maneno mapya.




KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 10 07/03/2022 16:49

**Zingatia**

Mwingiliano baina ya jamii zenye tamaduni tofauti huleta mabadiliko na maendeleo katika jamii. Mabadiliko na maendeleo hayo husababisha kuibuka kwa maneno mapya ili kuwakilisha dhana mpya zilizotokana na mabadiliko au maendeleo hayo. Matumizi ya maneno hayo husaidia lugha lengwa kukua kwani huongeza msamiati wake. Kuongezeka kwa msamiati wa lugha huwawezesha watumiaji wa lugha hiyo kukidhi mahitaji yao ya mawasiliano.

## Kazi ya 1.6



Tembelea maeneo ya soko au gulio, hospitali au zahanati, kisha bainisha maneno matano yaliyoibuka hivi karibuni. Eleza njia zilizotumika kuunda maneno hayo.

## Zoezi la marudio

1. Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi:

(i) Neno **soda** limeundwa kutokana na njia ipi kati ya hizi zifuatazo?
- (a) Ukopaji
- (b) Akronomia
- (c) Utohoaji
- (d) Unyambulishaji
- (e) Ufananisho

(ii) Maneno yapi kati ya haya yafuatayo yameundwa kwa njia ya uambatanishaji?
- (a) Mwanahewa, kizunguzungu, mwimbaji
- (b) Hatimiliki, boresha, pembetatu
- (c) Shamrashamra, televisheni, kataupepo
- (d) Kifaurongo, kisimbuzi, miundombinu
- (e) Mbwamwitu, mitishamba, afisaelimu

(iii) Sababu ipi kati ya hizi zifuatazo <u>haihusiki</u> na uundaji wa maneno katika lugha?
- (a) Kukuza lugha katika jamii inayohusika
- (b) Kutofautisha uchumi na teknolojia katika jamii
- (c) Kukidhi mahitaji ya mawasiliano
- (d) Kuibuka kwa mambo mapya katika jamii
- (e) Kuwa na msamiati wa kutosha katika lugha

(iv) Maneno yapi kati ya haya yafuatayo yameundwa kwa njia ya ufananisho?
- (a) Malapa, kuku, vuma
- (b) Bongolala, nyau, chamcha
- (c) Chemshabongo, jungukuu, mtutu
- (d) Katambuga, pikipiki, ufagio
- (e) Batamzinga, kifaru, kifuniko



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 11 07/03/2022 16:49

(v) Neno lipi kati ya haya yafuatayo <u>halikuundwa</u> kwa njia ya unyambulishaji?
  (a) Wimbo
  (b) Kicheko
  (c) Mchezo
  (d) Chamcha
  (e) Kipigo

2. Oanisha dhana zilizopo katika Orodha **A** na mfano wa maneno yaliyopo katika Orodha **B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Akronimu | A. katakata |
| (ii) Uambatanishaji | B. shikamoo |
| (iii) Uradidi | C. mchezaji |
| (iv) Utohoaji | D. LUKU |
| (v) Ufananisho | E. cherehani |
| | F. chamcha |
| | G. njugumawe |

3. Huku ukitoa mifano, fafanua njia zifuatazo za uundaji wa maneno:
   (a) Ukopaji
   (b) Uambatanishaji
   (c) Ufananisho
   (d) Uradidi
4. Eleza umuhimu wa kuunda maneno mapya katika lugha.
5. Thibitisha kuwapo kwa mambo yanayosababisha kuhitajika kwa maneno mapya.
6. Eleza tofauti kati ya kukopa na kutohoa maneno.
7. Kwa kutumia mifano, fafanua aina za ufupishaji kama njia ya uundaji wa maneno.
8. "Lugha kukopa maneno kutoka lugha zingine ni udhaifu." Kubali au pinga kauli hii kwa kutoa mifano.
9. "Ufupishaji, kama njia ya uundaji wa maneno, haufuati kanuni yoyote." Jadili.
10. Bainisha aina mbili za uradidi, kisha toa mifano mitatu kwa kila aina.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 12 07/03/2022 16:49

# Sura ya Pili

## Kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi ya Waingereza na baada ya uhuru


**Utangulizi**

*Lugha ya Kiswahili ilikua na kuenea kwa njia mbalimbali tangu enzi za ukoloni hadi baada ya uhuru. Katika sura hii, utajifunza kukua na kuenea kwa Kiswahili katika kipindi cha Waingereza na baada ya uhuru. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kubainisha shughuli, asasi, na maeneo yaliyochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania wakati wa utawala wa Waingereza na baada ya uhuru.*

### Kukua na kuenea kwa Kiswahili enzi ya Waingereza

**Kazi ya 2.1**

**Chunguza mchoro ufuatao, kisha jibu maswali yanayofuata.**






KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 13 07/03/2022 16:50

## Maswali

1. Waingereza walisaidia vipi katika kukua na kuenea kwa Kiswahili Tanganyika na Zanzibar?
2. Kamati ya Lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki ilikuwa na mchango gani katika kukuza na kueneza Kiswahili?
3. Vyombo vya habari vilikuwa na mchango gani katika kukuza na kueneza Kiswahili Tanganyika na Zanzibar?
4. Mawasiliano yapi yalifanywa kwa Kiswahili wakati wa ukoloni wa Waingereza?

**Zingatia**

Waingereza walishika hatamu nchini Tanzania (wakati huo Tanganyika na Zanzibar) mwaka 1919 hadi 1961 nchi ilipopata uhuru. Utawala wa Waingereza uliambatana na ongezeko la wamisionari waliokuja Afrika Mashariki. Wamisionari hao walikuja chini ya mashirika mbalimbali. Miongoni mwa mashirika hayo ni *Church Missionary Society* (CMS) kutoka Uingereza. Mashirika hayo yalisaidia kueneza lugha ya Kiswahili kupitia harakati za kueneza dini ya Kikristo. Katika kutimiza lengo lao la kueneza dini, wamisionari walitafsiri kwa Kiswahili na lugha zingine za jamii vitabu mbalimbali vya dini, ikiwamo Biblia. Maneno kama **misa**, **ekaristi**, na **ubatizo** yalitumika katika shughuli za kidini. Kutokana na hali hiyo, Kiswahili kiliendelea kukua kimsamiati.

Utawala wa Waingereza ulichukua hatua ya kusanifisha Kiswahili. Usanifishaji huo ulipitia hatua mbalimbali. Hatua ya kwanza muhimu ilikuwa kuchagua lahaja ya Kiunguja kuwa msingi wa Kiswahili sanifu. Uamuzi huu ulitokana na Kiunguja kuenea katika sehemu kubwa. Pia, kilikuwa kimefanyiwa uchunguzi na wataalamu mbalimbali na kilikuwa kimeandikiwa machapisho mbalimbali. Hatua ya pili ilikuwa kuunda Kamati ya Lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Kamati hii ilipewa jukumu la kusanifisha lugha ya Kiswahili kwa kutumia msingi wa lahaja ya Kiunguja na kusimamia matumizi ya Kiswahili katika mazingira rasmi, hasa katika uandishi wa vitabu. Hatua ya tatu ilikuwa kuanzisha Kitengo cha Uchapishaji wa Vitabu cha Afrika Mashariki (East African Literature Bureau - EALB). Kutokana na mchakato wa usanifishaji, Kiunguja ambacho kilifanyiwa marekebisho katika matamshi, maumbo, miundo, na msamiati, kiliwezesha Kiswahili kuwa na msamiati uliotumika katika shughuli mbalimbali, hivyo, kufanya Kiswahili kukua na kuenea katika mawasiliano rasmi.

Chini ya utawala wa Waingereza, Kiswahili kilitumika kufundishia shule za msingi kuanzia darasa la kwanza hadi la nne. Wanafunzi waliotoka katika maeneo mbalimbali waliweza kutumia Kiswahili wakiwa shuleni na nyumbani. Hali hii iliwezesha Kiswahili kukua na kuenea. Mawasiliano yaliyofanyika shuleni katika kufundisha Kiswahili yaliwezesha kupatikana kwa maneno kama vile **rula**, **peni**, na **begi**.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 14 07/03/2022 16:50

Aidha, katika kipindi cha Waingereza, kamusi mbalimbali zilitungwa. Kamusi hizo ni pamoja na *A Standard English - Swahili Dictionary*, *A Standard Swahili - English Dictionary*, na *Kamusi ya Kiswahili - Kiswahili*. Kamusi hizi zilichangia kukuza Kiswahili kimsamiati.

Sambamba na juhudi hizo zilizochukuliwa katika kukuza na kueneza Kiswahili, kulikuwa na shughuli zingine zilizochangia kukuza na kueneza Kiswahili. Mathalani, shughuli za kilimo katika mashamba makubwa ya mkonge zilihusisha vibarua walioitwa *manamba*. Shughuli hizo zilisababisha mwingiliano baina ya vibarua hao waliotokea maeneo tofauti. Lugha kuu iliyotumiwa kwa mawasiliano katika shughuli hiyo ilikuwa Kiswahili; hivyo, kuifanya ienee kwa watu wengi.

Matumizi ya Kiswahili yalikuwa muhimu katika shughuli zilizohusisha wafanyakazi wa ngazi za chini kama makarani na matarishi. Wafanyakazi hawa walilazimishwa kufahamu Kiswahili ili kukitumia katika shughuli za kila siku za kiutawala, hali iliyochangia kukua na kuenea kwake. Kwa mfano, maneno kama vile **faili**, **ripoti**, **ofisi**, na **bosi** yalianza kutumika katika mawasiliano.

Aidha, shughuli za vyombo vya habari zilizofanywa wakati huo zilikuwa na mchango mkubwa katika kukuza na kueneza Kiswahili. Shughuli hizo ni pamoja na matangazo ya redio, ambapo kulikuwa na Redio Tanganyika iliyokuwa inarusha matangazo yake kwa kutumia Kiswahili. Aidha, kulikuwa na magazeti yaliyokuwa yakichapishwa kwa Kiswahili. Mifano ya magazeti hayo ni *Mambo Leo*, *Sauti ya Pwani*, *Kiongozi*, na *Habari za Leo*. Kwa njia hii, Kiswahili kiliongeza maneno kama vile **magazeti** na **redio**. Kwa kufanya hivyo, vyombo vya habari vilichangia kukuza na kueneza Kiswahili.

Vilevile, shughuli za kisiasa zilichangia kukua na kuenea kwa Kiswahili. Baada ya Vita Vikuu vya Pili vya Dunia, katika nchi zilizokuwa chini ya utawala wa kikoloni, watu walihamasika kuanzisha vyama vya kijamii ambavyo baadaye vilibadilika kuwa vyama vya siasa. Katika harakati za kudai uhuru, kilianzishwa chama cha *Tanganyika African Association* (TAA). Baadaye, chama hicho kilibadilika na kuwa *Tanganyika African National Union* (TANU). Chama hiki kilitumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano kuwaunganisha Watanganyika katika harakati za kudai uhuru. Kwa upande wa Zanzibar, kulikuwa na chama cha *Afro Shiraz Party* (ASP) kilichotumia lugha ya Kiswahili katika harakati za Mapinduzi ya Zanzibar. Kwa ujumla, viongozi wa TANU na ASP walitumia Kiswahili katika mikutano na shughuli zingine za kisiasa. Aidha, nyimbo na mashairi mbalimbali yaliyoghaniwa kwa Kiswahili yaliwahamasisha watu kuwa na umoja na mshikamano. Katika harakati hizo, kaulimbiu kama *uhuru na umoja* na *uhuru na kazi* zilitumika katika kuleta hamasa. Kwa hiyo, kutokana na harakati za kisiasa, Kiswahili kiliendelea kukua na kuenea.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 15 07/03/2022 16:50

## Kazi ya 2.2

Kutoka vyanzo tofauti kama maktaba au makavazi, kusanya matini mbalimbali zinazohusu kukua na kuenea kwa Kiswahili katika utawala wa Waingereza, kisha zisome na kubainisha mchango wa Waingereza katika kukuza na kueneza Kiswahili.

## Zoezi la 2.1

1. Eleza namna utawala wa Waingereza ulivyotumia sekta ya elimu kukuza na kueneza Kiswahili.
2. Lahaja ipi iliteuliwa kuwa msingi wa Kiswahili sanifu? Eleza sababu za uteuzi wa lahaja hiyo.
3. Shughuli ipi ilikuwa na mchango mkubwa zaidi katika kukuza na kueneza Kiswahili katika utawala wa Waingereza? Fafanua kwa mifano.
4. Kamusi zipi ziliandikwa na kuhaririwa wakati wa Waingereza?

## Kazi ya 2.3

Soma maandiko mbalimbali yanayohusu harakati za ukombozi Tanganyika na Zanzibar, kisha wasilisha mambo uliyoyabaini kuhusu mchango wa Kiswahili katika harakati hizo.

**Zingatia**

Licha ya Kiswahili kukua na kuenea chini ya utawala wa Waingereza, kulikuwa na changamoto kadhaa ambazo ziliathiri suala hilo. Miongoni mwa changamoto hizo ni kutiliwa mkazo kwa matumizi ya Kiingereza badala ya Kiswahili katika baadhi ya shughuli za kiutawala. Kwa mfano, uandishi wa ripoti mbalimbali za kiutawala katika ngazi za juu ulifanywa kwa lugha ya Kiingereza na si kwa Kiswahili. Pili, maafisa wa ngazi za juu waliwasiliana kwa Kiingereza na si kwa Kiswahili. Aidha, Kiingereza kilikuwa lugha ya kufundishia darasa la tano hadi la nane katika shule za msingi. Vilevile, vitabu vya dini kama vile Biblia, vitabu vya liturujia, na vya nyimbo vilitafsiriwa kwa lugha za jamii. Hivyo, lugha za jamii zilitumika katika shughuli za kidini, hali iliyozorotesha maendeleo ya Kiswahili. Aidha, baadhi ya wananchi walikihusisha Kiswahili na vibaraka wa kikoloni; hivyo, hawakupendelea kukitumia kwani walikiona kama lugha ya wanyonyaji.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 16 07/03/2022 16:50

## Zoezi la 2.2

1. Fafanua changamoto mbalimbali zilizoathiri kukua na kuenea kwa Kiswahili katika utawala wa Waingereza.
2. Eleza jinsi Kiingereza kilivyozorotesha kukua na kuenea kwa Kiswahili wakati wa utawala wa Waingereza.
3. Bainisha maeneo ambamo Kiswahili hakikuweza kutumika wakati wa utawala wa Waingereza nchini Tanganyika.
4. Kwa nini maeneo uliyobainisha katika swali la 3 yalitumia lugha ya Kiingereza badala ya Kiswahili?
5. Una maoni gani kuhusu matumizi ya Kiswahili wakati wa utawala wa Waingereza nchini Tanzania?

## Kazi ya 2.4

**Chunguza ramani ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**






KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 17 07/03/2022 16:50

## Maswali

1. Vituo vilivyobainishwa kwenye ramani vinahusishwa na maendeleo ya Kiswahili enzi ya utawala wa Waingereza. Unafikiri ni mambo gani yalichangia kukua na kuenea kwa Kiswahili katika vituo hivyo?
2. Eleza namna mambo uliyoyabainisha katika swali la 1 yalivyochochea kukua na kuenea kwa Kiswahili katika kipindi hicho.

**Zingatia**

Katika kipindi cha utawala wa Waingereza, kulikuwa na shughuli mbalimbali zilizochochea kukua na kuenea kwa Kiswahili. Miongoni mwa shughuli hizo ni kilimo, ujenzi wa reli, dini, na elimu. Kwa upande wa kilimo, mazao mbalimbali ya biashara kama karanga, pamba, tumbaku, na mkonge yalizalishwa katika maeneo ya Nachingwea, Shinyanga, Tabora, na Tanga, mtawalia. Kilimo hicho kiliendeshwa kwa kuajiri vibarua walioitwa manamba. Vibarua hao walitoka katika makabila mbalimbali; hivyo, walilazimika kutumia Kiswahili kama lugha ya mawasiliano. Kwa njia hiyo, wengi waliweza kukifahamu na kukitumia na, waliporejea kwao, waliendelea kukieneza.

Hali kadhalika, yalikuwapo maeneo mengine yaliyochochea kukua na kuenea kwa Kiswahili kutokana na shughuli za ujenzi wa reli. Maeneo hayo ni Tabora, Mwanza, Kaliua, Mpanda, Kilosa, Mikumi, Kahe, Manyoni, na Singida. Mawasiliano katika shughuli za ujenzi wa reli katika maeneo hayo yalifanyika kwa Kiswahili. Aidha, katika baadhi ya maeneo, maendeleo ya Kiswahili yalichochewa na shughuli za kidini zilizofanywa na utawala wa Waingereza. Maeneo hayo ni kama Zanzibar, Tabora, Kigoma, na Moshi. Dini iliyoenezwa na utawala wa Waingereza katika maeneo hayo na mengine mengi ilikuwa Ukristo. Dini ilichangia kukua na kuenea kwa Kiswahili kupitia mahubiri yaliyokuwa yakitolewa kwa Kiswahili.

Zaidi ya hayo, baadhi ya maeneo kama Tabora, Iringa, Tanga, na Moshi yalihusishwa na shughuli za kielimu. Katika maeneo hayo, Waingereza walijenga shule mbalimbali, ambapo masomo ya shule za msingi yalifundishwa kwa Kiswahili. Aidha, katika ngazi ya sekondari, Kiswahili kilifundishwa kama somo.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 18 07/03/2022 16:50

## Kukua na kuenea kwa Kiswahili baada ya uhuru

### Kazi ya 2.5

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Semkwa na Gulama ni mtu na binamu yake. Wote wawili wanasoma kidato cha nne. Siku moja, majira ya jioni, baada ya kutoka shuleni, walikuwa wamekaa chini ya mti uliopo nje ya nyumba yao wakizungumza. Mazungumzo yao yalikuwa hivi:

**Gulama:** Hivi unajua ni lini Tanganyika ilipata uhuru kutoka kwa Waingereza?

**Semkwa:** Ninajua. Ilikuwa mwaka 1961, tulipoishusha bendera ya Waingereza na kuipeperusha bendera yetu ya Tanganyika. Inasemekana ilikuwa shangwe, nderemo na vifijo. Utawala wa Waingereza ulibwagwa rasmi, Watanganyika tukawa huru na tukaanza kujimwaga kwa lugha yetu ya Kiswahili.

**Gulama:** Eh! Basi, ishia hapo kwanza binamu maana ninaona nazi imepata mkunaji. Sijakuuliza kuhusu Kiswahili kwani hata mimi ninaelewa kuwa baada ya uhuru Kiswahili kilifanywa kuwa lugha rasmi na lugha ya taifa.

**Semkwa:** Umenikatisha tu, ila bado sijakueleza nilichotaka kukueleza. Tulianza kutumia Kiswahili katika sanaa, vyombo vya habari, elimu, siasa, na shughuli za kibiashara.

**Gulama:** Hata mimi ninaona kama unanikatisha nilichotaka kukueleza. Kiswahili kilifanywa kuwa lugha rasmi na lugha ya taifa. Si hivyo tu, kilifanywa pia kuwa lugha ya kufundishia katika shule zote za msingi za serikali. Vilevile, kiliendelea kufundishwa kama somo kwa shule za sekondari; ndiyo maana mpaka leo mimi na wewe tunajifunza somo la Kiswahili.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 19 07/03/2022 16:50

**Semkwa:** Ngoja sasa nikueleze. Tulitumia pia lugha ya Kiswahili katika vikundi vya kiutamaduni. Aidha, vyombo vya habari vilitumia Kiswahili kufikisha taarifa mbalimbali kwa wananchi. Wafanyabiashara wengi nao walitumia Kiswahili katika mawasiliano yao. Vilevile, kilitumika katika utawala. Hivyo basi, ukae ukijua kuwa, kuanzia mwaka 1961, mambo mengi yalibadilika.

## Maswali

1. Bainisha mambo yaliyochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanganyika baada ya uhuru.
2. Fafanua namna kila jambo ulilolitaja katika swali la 1 lilivyochangia katika kukuza na kueneza Kiswahili.
3. "Mpaka sasa, bado Kiswahili kinaendelea kukua na kuenea." Kwa kutumia mifano, kubali au kataa kauli hii.

**Zingatia**

Baada ya Uhuru wa Tanganyika, tukio muhimu la kwanza lilikuwa hotuba ya Mwalimu Julius Kambarage Nyerere aliyoitoa kwa Kiswahili kwenye Bunge la Kwanza la Jamhuri ya Tanganyika tarehe 10/12/1962. Hii ilikuwa mara ya kwanza kwa Kiswahili kutumika katika chombo cha juu kabisa cha taifa. Kuanzia wakati huo, Watanganyika walipata hamasa mpya ya matumizi ya Kiswahili. Kiswahili kilianza kutumika kama lugha ya mawasiliano katika wizara na idara mbalimbali za serikali. Kwa mfano, kilitumika katika uandishi wa barua, matangazo na katika maelekezo baina ya maafisa wa serikali na taasisi zake.

Ukuaji na ueneaji wa Kiswahili ulichangiwa pia na vyombo vya habari vilivyoanzishwa baada ya Uhuru. Vyombo hivi vilikuwa redio na magazeti. Redio ya Taifa pamoja na magazeti ya *Uhuru* na *Mzalendo* ni miongoni mwa vyombo vya habari vilivyoanzishwa. Vyombo hivi vya habari vilitumia Kiswahili kufikisha habari kwa wananchi, hali iliyowezesha Kiswahili kukua na kuenea kwa kasi zaidi nchini. Mnamo mwezi Februari 1963, Kiswahili kilitangazwa kuwa lugha ya taifa na lugha rasmi. Kuanzia wakati huo, watumishi wote wa serikali walipaswa kutumia Kiswahili kazini.

Jitihada mbalimbali zilifanywa na viongozi waandamizi wa serikali kusisitiza matumizi ya Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru na baada ya muungano wa Tanganyika na Zanzibar. Utekelezaji wa msisitizo huo ulichochea kukua na kuenea kwa Kiswahili. Jitihada ya kwanza ilifanywa mnamo mwaka 1967 na aliyekuwa Makamu wa Pili wa Rais, Hayati Rashid Mfaume Kawawa, ambaye alitoa waraka

wa matumizi ya Kiswahili kwa mawaziri, manaibu waziri, wakuu wa mikoa na wilaya, walimu wote, na watumishi wengine wa serikali. Waraka huo ulisisitiza kuwa kila afisa wa serikali na viongozi wote wawe mfano mzuri katika kutumia Kiswahili. Pia, ulisisitiza kutochanganya lugha. Vilevile, ulisisitiza kuwa maafisa elimu na walimu wote wana wajibu wa kuhakikisha kuwa wanafunzi wa shule zote wanakielewa Kiswahili. Aidha, ulisisitiza kuwa kila mtu aone fahari kutumia Kiswahili.

Jitihada ya pili inahusiana na kutangazwa kwa Azimio la Arusha mnamo mwaka 1967. Kufuatia Azimio hilo, ilitangazwa Sera ya Elimu ya Kujitegemea. Kiswahili kikaamuliwa kuwa lugha ya kufundishia masomo yote katika elimu ya msingi, isipokuwa somo la Kiingereza. Katika elimu ya sekondari, Kiswahili kilifanywa kuwa somo la lazima kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne. Pia, Kiswahili kilifanywa kuwa lugha ya kufundishia katika vyuo vya ualimu, vyuo vya maendeleo ya jamii, na vyuo vya utumishi wa umma. Isitoshe, Kiswahili kilitumika kama lugha ya kufundishia elimu ya watu wazima, ambapo lengo la elimu hii lilikuwa kutoa ujuzi wa kusoma na kuandika kwa Kiswahili. Aidha, Kiswahili kilianza na kinaendelea kufundishwa kama somo katika kidato cha tano na sita.

Katika ngazi ya chuo kikuu, Kiswahili kilianza kufundishwa katika Idara ya Isimu na Lugha za Kigeni ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam mwaka 1968. Mwaka 1970, chuo kikuu hiki kilipozinduliwa kama chuo kikuu kamili, Kiswahili kiliundiwa idara kamili ya Kiswahili katika Kitivo cha Fani na Sayansi za Jamii. Katika idara hii, taaluma za fasihi na isimu zilianza kufundishwa.

Jitihada ya tatu ilifanywa na serikali kupitia Waraka wa Utumishi Na. 1 wa mwaka 1974. Waraka huo ulitoa maelekezo kuhusu matumizi ya Kiswahili katika ofisi za serikali kwamba barua kati ya wizara na wizara ziandikwe kwa Kiswahili, isipokuwa kama anayeandikiwa si Mtanzania. Vilevile, ilielekezwa kwamba vibao vyote vya majina ya ofisi au wizara viandikwe kwa Kiswahili. Aidha, madokezo baina ya maafisa katika ofisi na fomu mbalimbali za serikali ziliamuliwa ziandikwe kwa Kiswahili. Jitihada zote hizi zilichangia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania.

Jitihada ya nne inahusiana na mwamko mpya wa matumizi ya Kiswahili kuanzia mwishoni mwa miaka ya 2010, ikiwamo kutafsiri sheria na majina ya nyadhifa na vitengo mbalimbali kwa Kiswahili pamoja na matumizi ya Kiswahili katika mikutano ya kitaifa na kimataifa.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 21 07/03/2022 16:50

## Zoezi la 2.3

1. Eleza sababu za uamuzi wa kuendelea kutumia Kiswahili katika mawasiliano mara tu baada ya uhuru.
2. Fafanua jinsi matumizi ya Kiswahili katika shughuli za kiutawala yalivyosaidia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.
3. Eleza namna shughuli za kibiashara zilivyochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.
4. Bainisha hatua tatu zilizochukuliwa na serikali katika kuhakikisha Kiswahili kinakua na kuenea nchini Tanzania baada ya uhuru.
5. Tathmini hatua ulizozibainisha katika swali la 4.

## Kazi ya 2.6



(a) Kwa kushirikiana na wenzako katika vikundi, soma matini mbalimbali zinazohusu historia na maendeleo ya Kiswahili, kisha chunguza namna Kiswahili kilivyokua na kuenea nchini Tanzania baada ya uhuru.

(b) Bainisha asasi tano zilizoundwa baada ya uhuru ili kukuza na kueneza Kiswahili. Eleza kwa ufupi majukumu ya kila moja.

(c) Tathmini mafanikio ya asasi ulizozibainisha katika swali (b) katika kukuza na kueneza Kiswahili.

**Zingatia**

Baada ya Tanganyika kupata uhuru, asasi mbalimbali ziliundwa kwa malengo ya kukuza na kueneza Kiswahili. Miongoni mwa asasi za mwanzo ilikuwa Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili kilichoundwa mwaka 1964 kutokana na iliyokuwa Kamati ya Lugha ya Kiswahili ya Afrika Mashariki. Chuo hiki kilikuwa chini ya Chuo Kikuu Kishiriki cha Dar es Salaam. Mwaka 1970, asasi hiyo iliitwa Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (TUKI). Miongoni mwa majukumu ya Taasisi hiyo yalikuwa kuchunguza na kuendeleza Kiswahili katika vipengele vyake vyote kwa kuzingatia mahitaji ya mipango ya maendeleo ya muda mfupi na ya muda mrefu ya Tanzania, Afrika Mashariki na kwingineko. Jukumu jingine lilikuwa kushirikiana na Idara ya Kiswahili na Idara ya Lugha za Kigeni na Isimu chuoni hapo katika kuchapisha jarida la *Kiswahili* na machapisho mengine kama vile kamusi. Miongoni mwa kamusi zilizochapishwa na TUKI ni *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*, *Kamusi ya Kiswahili - Kiingereza*, *na English - Swahili Dictionary.* Pia, Taasisi ilikuwa na jukumu la kukusanya taarifa kuhusu Kiswahili, sera na matumizi yake kutoka duniani kote na kusambaza taarifa hizo. Vilevile, Taasisi ilipaswa kufanya utafiti wa muda mfupi na wa muda mrefu kuhusu lugha ya Kiswahili na fasihi yake. Aidha,



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 22 07/03/2022 16:50

ilikuwa na jukumu la kuandaa mikutano na warsha za kitaaluma kuhusu Kiswahili.

Mnamo mwaka 2009, Idara ya Kiswahili na TUKI ziliungana na kuunda taasisi moja inayoitwa Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (TATAKI). Taasisi hii inajihusisha na ufundishaji, utafiti, na kutoa ushauri kuhusiana na Kiswahili na fasihi yake. Kiswahili kinatumika pia kufundishia masomo ya shahada za awali na za uzamili pamoja na kuendeshea shughuli za utafiti katika taasisi hii.

Asasi zingine zilizoanzishwa ni Baraza la Kiswahili la Taifa (BAKITA), kwa upande wa Tanzania Bara, na Baraza la Kiswahili Zanzibar (BAKIZA), kwa upande wa Zanzibar. BAKITA lilianzishwa mwaka 1967 ilhali BAKIZA lilianzishwa mwaka 2003. Mabaraza haya yalipewa majukumu ya kukuza na kueneza Kiswahili. Katika kutekeleza majukumu hayo, mabaraza haya yamekuwa yakisimamia matumizi ya Kiswahili fasaha na sanifu, kuandaa na kuchapisha kamusi na majarida mbalimbali, kutafsiri na kukalimani kwa Kiswahili, kufanya tafiti mbalimbali za Kiswahili, na kupitia na kusanifu maandishi ya Kiswahili. Kadhalika, mnamo mwaka 1979, iliundwa Taasisi ya Kiswahili na Lugha za Kigeni Zanzibar (TAKILUKI), ambayo ilibadili jina kuanzia mwaka 2012 na kuwa Skuli ya Kiswahili na Lugha za Kigeni (SKILUKI). Majukumu yake makuu ni kufundisha Kiswahili kwa wenyeji na wageni na kufanya tafiti mbalimbali za Kiswahili.

Aidha, kuna vyama mbalimbali vya Kiswahili ambavyo vimechangia kukuza na kueneza Kiswahili nchini Tanzania. Vyama hivyo ni pamoja na Chama cha Lugha na Fasihi ya Kiswahili Tanzania (CHALUFAKITA), Chama cha Kiswahili Zanzibar (CHAKIZA), na Umoja wa Waandishi wa Vitabu Tanzania (UWAVITA). Kwa pamoja, vyama hivi vimekuwa vikitoa mchango wa kukuza na kueneza Kiswahili kupitia shughuli mbalimbali. Miongoni mwa shughuli hizo ni kuandaa na kuratibu makongamano na mashindano mbalimbali ya Kiswahili (kwa mfano, uandishi wa insha), kuhamasisha wataalamu kufanya tafiti kuhusu lugha, fasihi na utamaduni wa Kiswahili, pamoja na kuchapisha machapisho ya Kiswahili.

## Zoezi la marudio

1. Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi:
   (i) Kiswahili kilianza kutumika kama lugha ya mawasiliano na kufanywa kuwa lugha ya taifa nchini Tanganyika wakati gani?
      (a) Enzi ya utawala wa Waingereza
      (b) Enzi ya utawala wa Wajerumani
      (c) Enzi ya utawala wa Waarabu
      (d) Baada ya kupata uhuru
      (e) Baada ya kuingia Wamisionari

(ii) Ipi kati ya asasi zifuatazo za kiserikali iliundwa kwa lengo la kukuza na kueneza Kiswahili Zanzibar?
  (a) BASATA
  (b) BAMITA
  (c) BAKIZA
  (d) BAKITA
  (e) CHAKIZA

(iii) Miongoni mwa magazeti yaliyochapishwa kwa Kiswahili wakati wa utawala wa Waingereza ni ...............
  (a) Habari Leo
  (b) Habari za Leo
  (c) Uhuru
  (d) Mzalendo
  (e) Mwananchi

(iv) Miongoni mwa changamoto zilizoathiri ukuaji na ueneaji wa Kiswahili wakati wa utawala wa Waingereza ni ...............
  (a) Kiswahili kutumika kama lugha ya taifa
  (b) vyombo vya habari kutumia Kiswahili
  (c) wamisionari kutumia lugha za jamii kutafsiri vitabu vya dini
  (d) Kiswahili kuchukuliwa kama lugha duni
  (e) Kiswahili kutumika kama lugha ya mawasiliano

(v) Chuo cha Uchunguzi wa Kiswahili kilianzishwa mwaka gani?
  (a) 1930
  (b) 1963
  (c) 1967
  (d) 1964
  (e) 1970

2. Oanisha asasi zilizopo katika Orodha **A** na miaka ya kuundwa kwa asasi hizo iliyopo katika Orodha **B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) TATAKI | A. 1979 |
| (ii) BAKIZA | B. 2009 |
| (iii) TAKILUKI | C. 1970 |
| (iv) BAKITA | D. 2003 |
| (v) TUKI | E. 2012 |
| | F. 1967 |
| | G. 1972 |

3. Eleza jinsi Kiswahili kilivyoimarika nchini Tanzania kupitia mfumo wa elimu wakati wa ukoloni wa Waingereza.
4. Fafanua sababu tano zilizochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.
5. Maendeleo ya Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru yalikuwa na changamoto gani?
6. Bainisha mambo matano yaliyochangia kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanganyika katika enzi ya utawala wa Waingereza.
7. Vyombo vya habari vilisaidiaje kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru?
8. Eleza mchango wa BAKITA na TUKI katika kukua na kuenea kwa Kiswahili nchini Tanzania baada ya uhuru.
9. Kwa kila asasi zifuatazo, bainisha majukumu makuu matano.
   (a) BAKITA
   (b) BAKIZA.
10. Andika kwa kirefu majina ya asasi zifuatazo:
   (a) BAKITA
   (b) TUKI
   (c) BAKIZA
   (d) TATAKI
   (e) TAKILUKI

# Sura ya Tatu

## Uhakiki wa kazi za fasihi andishi

**Utangulizi**

*Kazi yoyote ya fasihi huwa na dhima mbalimbali. Miongoni mwa dhima hizo ni kueleza uhalisi wa maisha, na kuifunza jamii maadili mema. Hivyo, kazi hiyo huchambuliwa na kufafanuliwa ili kuonesha ubora na udhaifu wake. Katika sura hii, utajifunza kuhakiki kazi za fasihi andishi ambazo ziko katika tanzu za ushairi, tamthiliya, na riwaya kwa kuzingatia vipengele vya fani na maudhui. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuchambua kazi mbalimbali za fasihi andishi na kuonesha ubora na udhaifu wake.*

### Dhana ya uhakiki

**Kazi ya 3.1**

**Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Fasihi kuichambua, wahitaji umakini,
Vigezo kuvitumia, kazi kupata thamani,
Mtindo kupambanua, muundo ni ujengani,
Fasihi kuihakiki, ni fani na maudhui.

Lugha ni wetu msingi, wa kazi kuielewa,
Vipengele vyake vingi, ujumbe kuelezewa,
Semi zajenga msingi, maadili kutolewa,
Fasihi kuihakiki, ni fani na maudhui.

Uhalisi wa maisha, mandhari inahusika,
Wahusika kuwezesha, mawazo kukamilika,
Vyote vinajumuisha, ufundi kuimarika,
Fasihi kuihakiki, ni fani na maudhui.

Dhamira ndiyo kiini, cha muhimu kuhakiki,
Wahakiki kubaini, bila kuwa na mikiki,
Ujumbe ukumbukeni, bila ya kutaharuki,
Fasihi kuihakiki, ni fani na maudhui.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 26 07/03/2022 16:50

Ukinzani kuchunguza, na suluhu kubaini,
Bila ya mauzauza, nawasihi unganeni,
Mtazamo nao waza, muandishi kuthamini,
Fasihi kuihakiki, ni fani na maudhui.

Itikadi yahusika, usawa kutujengea,
Falisafa kuishika, msimamo kutetea,
Vipengele ukishika, uhakiki kutimia,
Fasihi kuihakiki, ni fani na maudhui.

Machache tumeeleza, yafaa kuzingatiwa,
Tanzu zake kuchunguza, msingi umejengewa,
Ujuzi umeukuza, wa uhakiki elewa,
Fasihi kuihakiki, ni fani na maudhui.

## Maswali


1. Andika kichwa cha shairi ulilolisoma.
2. Bainisha misingi ya uhakiki wa kazi za fasihi.
3. Kwa kutumia shairi ulilolisoma, eleza vipengele vya fani na maudhui.
4. Toa maoni yako kuhusu lugha iliyotumika katika shairi hili.
5. Mwandishi wa shairi hili alikusudia kufikisha ujumbe gani kwa msomaji?

**Zingatia**

Uhakiki wa kazi za fasihi huhusisha kuchambua, kufasili, kufafanua, kutathmini, na kutoa maoni kuhusu kazi fulani ya fasihi. Uhakiki wa kazi yoyote ya fasihi haufanyiki kiholela bali huzingatia vipengele vya fani na maudhui. Fani ni ufundi wa kisanaa unaotumiwa na mwandishi kuyawasilisha maudhui yake kwa hadhira. Ufundi huo wa kisanaa hujumuisha muundo wa kazi ya fasihi, mtindo, mandhari, wahusika, na matumizi ya lugha. Maudhui ni mambo mbalimbali ambayo mwandishi anakusudia yaifikie hadhira yake. Maudhui hujumuisha dhamira, ujumbe, migogoro, falsafa, msimamo, mtazamo, na itikadi. Hivyo, msingi mkuu katika uhakiki wa kazi ya fasihi ni fani na maudhui. Vipengele hivi hujengana, hutegemeana na hukamilishana. Tazama Kielelezo Na. 3.1.




KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 27 07/03/2022 16:50




**Kielelezo Na. 3.1:** *Vipengele vya uhakiki wa fasihi andishi*

## Kazi ya 3.2

**Chunguza mchoro ufuatao, kisha jibu maswali yanayofuata.**



1. (a) Fafanua vipengele vinavyounda mchoro huu.
   (b) Kwa nini ni muhimu kufahamu vipengele hivyo?
   (c) Vipengele hivyo vinahusiana vipi na suala la uhakiki wa kazi za fasihi andishi?

2. Kusanya kazi sita za fasihi andishi zilizochapishwa (diwani mbili, tamthiliya mbili, na riwaya mbili), kisha bainisha vipengele vifuatavyo:
   (a) Mchapishaji na mwaka wa kuchapishwa kwa kazi hiyo kwa mara ya kwanza
   (b) Jina kamili la mwandishi
   (c) Mahali mwandishi alipozaliwa na kukulia
   (d) Elimu au taaluma ya mwandishi
   (e) Kazi alizowahi kufanya mwandishi

**Zingatia**

Mwandishi ni sehemu ya jamii. Kwa kuwa mwandishi ni sehemu ya jamii, ni wazi kuwa anayoyaandika katika kazi yake ni yale yanayoihusu jamii hiyo. Hivyo, kabla ya kuanza kuchunguza kazi, ni vyema mhakiki akaanza kujiuliza kuhusu vipengele mbalimbali vinavyohusiana na mwandishi mwenyewe. Miongoni mwa vipengele hivyo ni kuzaliwa kwake. Kipengele hiki hujumuisha mwaka na mahali alikozaliwa mwandishi. Ikiwezekana, mhakiki ajiulize pia kuhusu mahali alikokulia mwandishi. Majibu ya vipengele hivi huweza kumsaidia mhakiki kujua na kuhusisha anayoyaona katika kazi na uhalisi wa mazingira ya asili ya mwandishi. Kipengele kingine kinahusiana na elimu au taaluma ya mwandishi. Kiwango na aina ya elimu au taaluma ya mwandishi hutoa mchango katika kusawiri maudhui yenye mwelekeo fulani. Aidha, kuna kipengele cha mwaka ambao kazi hiyo ilichapishwa. Kipengele hiki humsaidia mhakiki kuhusisha maudhui anayoyaona na uhalisia wa miktadha mbalimbali ya maisha wakati kazi inayohusika ilipochapishwa kwa mara ya kwanza.

## Kuhakiki kazi za ushairi

### Kazi ya 3.3

**Soma ngonjera ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**Kusekwa:**

Tuanzishe mdahalo, kuhusu maisha yetu,
Tujadili jambo hilo, tusije kushindwa katu,
Tutaje jambo ambalo, laipa mioyo kutu,
Tuzichangamshe bongo, tupate kuneemeka.

**Gambaku:**

Umeleta wazo zuri, naiunga yako hoja,
Muda huu si wa shari, wala kufanya vioja,
Ninasikiza habari, kuna hoja yenye tija,
Tujadili ya akiba, naona ina mashiko.

**Wangwi:**

Akiba ni jambo gani, maana yake ni nini?
Tupo sote darasani, unatuweka fumboni,
Tueleze kiundani, na faida yake nini?
Akiba ni jambo geni, tueleze tutambue.

**Kusekwa:**

Bado tupo njia panda, tupe maana tujue,
Bongo zetu zimeganda, hebu nawe zibandue,
Au akiba vibunda, wazazi tuwaibie?
Tufungue masikio, ili nasi tuelewe.

**Gambaku:**

Nilisikia habari, kutoka kwenye redio,
Walisema si hatari, faida kwa wawekao,
Hutaiona fahari, kwa mmoja tu uchwao,
Ni kile kinachotunzwa, kila kipata gawio.

**Wangwi:**

Kidogo ninaelewa, japo sikubali hoja,
Nyumbani niliambiwa, pesa nisije kufuja,
Ni wakubwa hutakiwa, sisi wakati takuja,
Akiba ni kwa wakubwa, wakati wetu si sasa.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 30 07/03/2022 16:50

**Gambaku:**
Tunapaswa kutambua, tungali bado wadogo,
Na hela wakitugea, tuzihifadhi kidogo,
Likizo ikiwadia, tusikose za mihogo,
Akiba ni mazoea, hayaanzi ukubwani.

**Kusekwa:**
Ha ha ha! Wanichekesha, mbavu zangu zinauma,
Ninahisi wapotosha, unaturudisha nyuma,
Kumbe wewe wababaisha, kesho isije kubuma,
Tegemezi ni wazazi, wao waweke akiba.

**Wangwi:**
Huanzia ukubwani, kwetu akiba si kitu,
Umefikiri kichwani, wataka tuibe vitu?
Au tuende kazini, tuzisake mia tatu?
Wataka kutupotosha, akiba si jambo letu.

**Kusekwa:**
Umenena ya moyoni, usemayo ni ya kweli,
Tusilete ubishani, hili kwetu si halali,
Twapaswa tuwe shuleni, tuitumie akili,
Akiba ni kwa wakubwa, wadogo sisi elimu.

**Wangwi:**
Akiba yaleta wizi, tabia hii ni mbaya,
Tutaanza fanya kazi, hebu tuoneni haya,
Tusijifanye wajuzi, tutavunjika na taya,
Akiba ni kwa wakubwa, wakati wetu si sasa.

**Mwalimu:**
Mbona mwaweka vikao, mngali mu darasani?
Hebu futeni ubao, tuianze mada ngeni,
Jumatano jaribio, wiki kesho mtihani,
Futeni tena upesi, niwape hayo maswali.

**Gambaku:**
Hapa kuna mdahalo, ni bora umetokea,
Wabishi kina Kobelo, hadi wameninunia,
Akiba ndo kimbilio, wao wananibishia,
Wanasema siyo sasa, sisi bado ni wadogo.

**Kusekwa:**
Mwalimu tupe elimu, kuhusu hii akiba,
Eti ni kitu muhimu, analeta ya vikoba,
Nahisi atuhujumu, tusije mbele kuiba,
Akiba kwetu halali? Tupe elimu mwalimu.

**Mwalimu:**

Haya futeni ubao, mpate wote kujua,
Nimepata mshangao, akiba kutoijua,
Basi mtajua leo, mada itasubiria,
Kaeni kwa utulivu, msikie nisemacho.

Kile kinachobakia, kwenye chanzo cha mapato,
Faida mnaijua, ukishatoa makato,
Hifadhi nakuambia, ili kilinde kipato,
Kaeni kwa utulivu, msikie nisemacho.

Kila unachokiuza, weka kiasi kidogo,
Hili msije puuza, wala kulipa kisogo,
Sauti ninaipaza, faida zake si ndogo,
Nitasema kwa uchache, kidogo mpate jua.

Ni kweli ninyi wadogo, ila mwapaswa kujua,
Elimu ni kwa wadogo, kuyajenga mazoea,
Mkipewa za mihogo, kiasi kujiwekea,
Kaeni kwa utulivu, msikie nisemacho.

Kuna mambo ya dharura, hayatoi taarifa,
Ajali nyingi zafura, zinayaleta maafa,
Biashara na hasara, mtaji waweza kufa,
Hapa akiba yafaa, kuyakabili majanga.

Maradhi yanatufika, malaria na kifafa,
Kile ulichokiweka, kitakufaa Latifa,
Mnaweza nusurika, na kuliponya taifa,
Hapa akiba yafaa, kutibu yenu maradhi.

Misaada utatoa, kutoka kwenye akiba,
Mtaji hutanyofoa, wala hutakwenda iba,
Nahisi mmetambua, ni nini sasa akiba,
Akiba ni jambo zuri, kwa wakubwa na watoto.

**Kusekwa, Gambaku na Wangwi:** Tunashukuru mwalimu, hakika tumeelewa,
Akiba jambo muhimu, tunapaswa kutambuwa,
Hiki kwetu ni adhimu, hatutakuja ishiwa,
Akiba kitu muhimu, wakubwa wadogo pia.

## Maswali

1. Pendekeza kichwa cha ngonjera uliyoisoma.
2. Unafikiri mwandishi anakusudia kufikisha ujumbe gani kwa jamii kupitia ngonjera uliyoisoma?
3. Bainisha umuhimu wa suala linalojadiliwa katika ngonjera.
4. Eleza maana ya kila sentensi kama ilivyotumika katika ngonjera.
   (a) Tutaje jambo ambalo, laipa mioyo kutu.
   (b) Ni kile kinachotunzwa, kila kipata gawio.
   (c) Akiba ni mazoea, hayaanzi ukubwani.
   (d) Elimu ni kwa wadogo, kuyajenga mazoea.
   (e) Ajali nyingi zafura, zinayaleta maafa.
5. Eleza maana ya dhana zifuatazo za ngonjera huku ukitoa mifano kwa kila moja.
   (a) vina
   (b) mishororo
   (c) beti
   (d) ukwapi na utao
   (e) lugha ya picha

**Zingatia**

Ushairi ni sanaa ya lugha ya mkato inayosawiri jambo fulani kwa kuzingatia mpangilio maalumu wa maneno, matumizi ya picha, na, kwa ushairi wa kimapokeo, urari wa vina na mizani. Ushairi wa fasihi andishi hujitokeza katika vipera vitatu ambavyo ni ngonjera, mashairi, na tenzi. Vipera hivi hutofautiana kimuundo. Ngonjera zinatofautiana na tenzi na mashairi kwa muundo wake wa majibizano. Katika ngonjera, mmoja anatamba; zamu yake ikiisha, anampisha mwingine. Kila zamu ya kutamba huwakilishwa na ubeti angalau mmoja. Kwa mfano, katika ngojera iliyopo katika kazi ya 3.3, kuna majibizano kati ya wahusika wanne. Kwa upande wa shairi, muundo wake hujipambanua kutokana na idadi ya mishororo. Shairi huweza kuwa na mshororo mmoja, mishororo miwili, mitatu, au zaidi. Vilevile, shairi huweza kuwa na muundo wenye vipande viwili au zaidi. Kwa mfano, shairi lililopo katika kazi ya 3.1 limeundwa kwa mishororo minne katika kila ubeti na mizani kumi na sita katika kila mshororo. Utenzi wenyewe hujipambanua kwa muundo wa beti zake ambazo huwa na mistari minne yenye mizani nane kila mmoja. Pia, kituo huwa na kina cha mwisho kinachofanana katika utenzi mzima.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 33 07/03/2022 16:50

Beti zifuatazo zinaonesha mfano wa muundo wa beti za utenzi.

Basi mwanangu elimu,
Ndicho kitu cha muhimu,
Uishike kwa nidhamu,
Mwanangu wanisikia?

Yataka uvumilivu,
Pia uwe msikivu,
Tena uache uvivu,
Elimu kuiendea.

## Kazi ya 3.4

Soma matini mbalimbali kuhusu uhakiki wa kazi za fasihi andishi, kisha fafanua vipengele vya kuzingatia katika kuhakiki vipera vya ushairi.

**Zingatia**

Uhakiki wa kazi za ushairi huhusisha vipengele vya fani na maudhui. Kama ilivyokwishaelezwa, fani hujumuisha muundo, mtindo, matumizi ya lugha, wahusika, pamoja na mandhari. **Muundo** ni mjengo, msuko na mpangilio wa vipengele vinavyojenga kazi ya fasihi. Mhakiki anapochambua muundo wa kazi ya ushairi, huchunguza mambo kadhaa. Chunguza shairi lifuatalo:

**Mama ni mama**

Ninayo mengi moyoni, tayasema kwa awamu,
Nawaomba tulieni, tena shikeni kalamu,
Sikizeni kwa makini, hadithi yangu ni tamu,
Lazima niwambieni, kunyamaza ni vigumu,
Mama ni mama jamani, hakuna wa kufanana.

Hakuna wa kufanana, mama ni mama jamani,
Kanifunza kupendana, toka ningali tumboni,
Nyumbani katulizana, hakuranda mitaani,
Nyota ikaonekana, kanileta duniani,
Kwa upendo kanilea, nampenda wangu mama.

Nampenda wangu mama, kwa upendo kanilea,
Yeye ni mlezi mwema, wote twamtegemea,
Niliposhikwa na homa, kasimama kidedea,
Kanitibia mapema, uhai kautetea,
Nilipofanya makosa, aliniadhibu pia.

Aliniadhibu pia, nilipofanya makosa,
Macho alinikazia, wala hakuyapepesa,
Rafiki alizuia, wale walojaa visa,
Kile alikusudia, niiepuke mikasa,
Zunguka yote dunia, mama kiumbe pekee.

Mama kiumbe pekee, zunguka yote dunia,
Mamia uwaendee, siyo tu wa familia,
Ukweli ujionee, mama kiongozi pia,
Bendera na ipepee, mama kumshangilia,
Sinacho cha kumlipa, kwa aliyonifanyia.

Kwa aliyonifanyia, sinacho cha kumlipa,
Mengi alivumilia, ili nisitoke kapa,
Elimu kanipatia, hata ada alikopa,
Mchicha kajipikia, sana alitapatapa,
Uniondoke ujinga, shule alinipeleka.

Shule alinipeleka, uniondoke ujinga,
Alilalia mkeka, bajeti aliipanga,
Sasa ninaheshimika, natembea ninaringa,
Lakini aliteseka, hilo siwezi kupinga,
Wenzangu nawausia, tusimdharau mama.

Tusimdharau mama, wenzangu nawausia,
Maishani utakwama, baraka zitakimbia,
Mambo takuwa mrama, utafunzwa na dunia,
Mikosi itakwandama, kila siku utalia,
Meli imetia nanga, mwishoni nimefikia.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 35 07/03/2022 16:50

Mwishoni nimefikia, meli imetia nanga,
Penye nia pana njia, walitamka wahenga,
Yote ulonitendea, hakika yamenikinga,
Nitaishinda dunia, umenitoa ujinga,
Mama ni mama jamani, hata akiwa rikwama.

Kwanza, katika muundo, mhakiki huchunguza *idadi ya beti*. Ubeti ni fungu la mishororo linalojitegemea. Idadi ya beti katika shairi hutegemea matakwa ya mwandishi. Shairi linaweza kuwa na ubeti mmoja au zaidi. Kwa mfano, shairi la **Mama ni mama** lina jumla ya beti tisa. Beti za mashairi mengi ya kimapokeo huwa na mishororo minne, ingawa kuna mashairi ambayo beti zake zina mishororo mitano kama katika shairi la **Mama ni mama**. Kwa upande mwingine, ngonjera, aghalabu, huwa na beti chache zenye mishororo minne kwa kila ubeti mmoja. Pia, ubeti mmoja wa ngonjera hubeba wazo kuu moja ambalo huweza kuwa swali au jibu. Utenzi, kwa upande wake, huwa na beti nyingi zaidi kwani huweza hata kufikia mia moja, tofauti na shairi na ngonjera ambazo huwa na beti chache.

Pili, mhakiki huchunguza *mishororo*. Mishororo ni mistari katika ubeti wa kazi ya ushairi. Mhakiki huchunguza ili kuona kazi ya ushairi imejengwa na mishororo mingapi kwa kila ubeti. Mshororo huweza kuwa na kipande kimoja au zaidi kutegemeana na aina ya kipera. Kipera cha mashairi na cha ngonjera huwa na vipande viwili na kuendelea. Kwa upande mwingine, utenzi huwa na kipande kimoja tu. Idadi ya mishororo katika ubeti inaweza kuanzia mshororo mmoja hadi kumi kulingana na aina ya kipera. Shairi la **Mama ni mama** lina mishororo mitano katika kila ubeti. Hivyo, mhakiki huchunguza kazi hiyo ya ushairi imejengwa kwa beti zenye mishororo mingapi.

Tatu, mhakiki huchunguza idadi ya *vipande* katika kila mshororo wa kazi ya ushairi. Kipande ni sehemu ya mshororo. Mishororo ya mashairi mengi huwa na vipande viwili ijapokuwa yapo yenye vipande vitatu. Kipande cha kwanza huitwa *ukwapi*, cha pili huitwa *utao*, na cha tatu huitwa *mwandamizi*. Kwa mfano, katika shairi la **Mama ni mama**, ubeti wa kwanza, mshororo wa kwanza, ukwapi ni *Ninayo mengi moyoni*, na utao ni *tayasema kwa awamu*. Mishororo ya tenzi, kwa upande wake, mara nyingi huwa na kipande kimoja.

Nne, mhakiki huchunguza muundo wa kazi ya ushairi. Huangalia kazi hiyo imejengwa kwa *vina* vya namna gani. Vina ni silabi za kati na za mwisho za sauti zinazofanana. Kina cha kati huitwa *ukwapi* na kina cha mwisho huitwa *utao*. Beti za kazi ya ushairi hujengwa kwa kina kimoja au zaidi kutegemeana na aina ya kazi ya ushairi. Mashairi na ngonjera huwa na vina viwili au zaidi, lakini tenzi huwa na kina kimoja tu. Kwa mfano, katika shairi la **Mama ni mama** ubeti wa tatu, kina cha kati ni **ma** na kina cha mwisho ni **a**.

Tano, mhakiki huchunguza *mizani*. Idadi ya silabi katika kila mshororo huitwa mizani. Mishororo ya mashairi mengi ya kimapokeo imejengwa na mizani kumi na sita, yaani mizani nane kwa kila kipande. Kwa upande mwingine, mishororo ya tenzi hujengwa na mizani nane tu. Kwa mfano, mshororo wa kwanza wa ubeti wa kwanza wa shairi la **Mama ni mama** una jumla ya mizani kumi na sita kama inavyooneshwa hapa chini:

| | | | | | | | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| /Ni/ | /na/ | /yo/ | /me/ | /ngi/ | /mo/ | /yo/ | /ni/, | /ni/ | /ta/ | /ya/ | /se/ | /ma/ | /kwa/ | /ha/ | /mu/, |
| 1 | 2 | 3 | 4 | 5 | 6 | 7 | 8 | 9 | 10 | 11 | 12 | 13 | 14 | 15 | 16 |

Sita, katika muundo, mhakiki huchunguza pia *kituo* au *kibwagizo*. Kituo au kibwagizo ni mshororo wa mwisho katika kila ubeti wa shairi ambao huwa kama kiitikio. Kituo, kinaporudiwarudiwa katika beti zote, huitwa kituo bahari, na kisiporudiwarudiwa huitwa kituo kimalizio.

Saba, muundo wa kazi ya ushairi hujengwa kwa *utoshelevu*. Utoshelevu ni hali inayohusiana na kupatikana kwa maana katika kipashio cha kazi ya ushairi. Mara nyingi, hali hii hudhihirika katika kazi nzima ya ushairi, katika ubeti, na, wakati mwingine, katika mshororo. Kwa mfano, mshororo wa pili wa ubeti wa pili katika shairi la **Mama ni mama** umejitosheleza, yaani umebeba maana kamili. Mshororo huo ni "*Kanifunza kupendana, toka ningali tumboni*".

Nane, muundo wa kazi ya ushairi hujengwa na *muwala*. Muwala ni mtiririko na mpangilio mzuri wa vipengele vyote vya shairi. Mtiririko huo huleta uwiano baina ya vipengele vya fani na maudhui katika shairi.

Kipengele kingine cha fani cha kuzingatia wakati wa uhakiki ni **mtindo**. Mtindo ni upekee wa mwandishi unaodhihirika katika kazi yake. Upekee ndio hutofautisha kazi ya mwandishi mmoja na kazi za waandishi wengine. Mtindo huhakikiwa kwa kuangalia kama shairi limezingatia au halijazingatia kanuni za utunzi wa mashairi. Miongoni mwa kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo ni kuwapo kwa urari wa vina, urari wa mizani, utoshelevu, na kituo. Kwa hiyo, shairi linaweza kuwa la kimapokeo kama limezingatia kanuni hizo au la kisasa kama halikuzingatia kanuni hizo au litazingatia baadhi ya kanuni. Tazama mfano wa shairi la **Kiswahili**.

**Kiswahili**

Kiswahili lugha yangu,
Nakupenda,
Tokea utoto wangu,
Nakusema,
Wewe ni fahari yangu,
Nakuenzi.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 37 07/03/2022 16:50

Kiswahili lugha tamu,
Nakubali,
Wewe ni lulu adhimu,
Najidai,
Umeishika hatamu,
Wapepea.

Kiswahili si Kizungu,
Kwa hakika,
Kinaondoa machungu,
Nikiimba,
Paa hadi mawinguni,
Nakutuma.

Kiswahili kinapaa,
Duniani,
Ulaya kinasambaa,
Kwa madaha,
China chakata mitaa,
Kinang'aa.

Kiswahili Tanzania,
Hadi Kenya,
Twakitumia kuandaa,
Na mitalaa,
Msingi kujifunzia,
Hadi vyuo.

Shairi hili ni mfano wa mashairi ya kisasa kwa kuwa halikuzingatia urari wa vina na mizani.

Vilevile, kipengele cha mtindo hujumuisha matumizi ya tanzu zingine za fasihi ndani ya kazi ya ushairi. Kwa mfano, mwandishi anaweza kuingiza wimbo, au hadithi. Pia, matumizi ya nafsi ni sehemu ya mtindo. Mhakiki anapaswa kuchunguza ni nafsi ya ngapi imetumika zaidi katika kazi husika. Kwa mfano, mwandishi anaweza kutumia nafsi ya kwanza, ya pili, au ya tatu zikiwa katika umoja au wingi. Katika shairi la **Mama ni mama**, mwandishi ametumia nafsi ya kwanza na ya tatu umoja.

Kipengele kingine cha fani ambacho mhakiki huchunguza ni **matumizi ya lugha**. Matumizi ya lugha hujumuisha uteuzi wa maneno anayoyatumia mtunzi, upangaji wa maneno hayo, pamoja na mpangilio wa sauti za lugha na maneno ili kuleta maana kamili. Mwandishi wa kazi ya ushairi anapaswa kuteua maneno kulingana na kile anachokiandikia.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 38 07/03/2022 16:50

Aidha, mwandishi anapaswa kutumia lugha ya picha na tamathali za semi ili kumvutia msomaji wa kazi ya ushairi. Tamathali mojawapo ni *tashibiha,* yaani kulinganisha kitu kimoja na kingine kwa sura, sifa au tabia. Nyingine ni *sitiari,* yaani kutumia kitu kimoja kuwakilisha kitu kingine ambacho hakina uhusiano nacho. Kwa mfano, mwandishi anaweza kutumia neno "ua" akiwa na maana ya mke. Pia, mwandishi anaweza kutumia *tasfida* kwa lengo la kuficha jambo au kupunguza ukali wa maneno. Maneno kama "kwenda uani" yakiwa na maana ya kwenda chooni yanaweza kutumika kwa lengo la kupunguza ukali wa maneno.

Hali kadhalika, uhakiki wa kazi ya ushairi huzingatia **wahusika** ambao hubeba sifa na tabia zilizomo katika jamii. Mara nyingi, wahusika huwa viumbe ambao hupewa matendo na lugha ili kuwasilisha ujumbe unaotolewa katika jamii hiyo. Kwa mfano, katika shairi la **Mama ni mama**, mhusika ni mama.

Vilevile, uhakiki wa ushairi huzingatia **mandhari** ambamo visa na matukio ya kifasihi hufanyika. Kipengele cha mandhari hakijitokezi kwa uwazi sana katika ushairi kama kinavyojitokeza katika tanzu zingine za fasihi andishi.

Mbali na fani, mhakiki anapaswa kuhakiki *maudhui*, yaani mambo yote ambayo mwandishi analenga kuyafikisha kwa hadhira. Anapohakiki maudhui, anazingatia kipengele cha *dhamira*, *ujumbe*, *migogoro*, *falsafa*, *mtazamo*, *msimamo*, na *itikadi*. Jambo kuu linalozungumziwa katika kazi ya fasihi huitwa **dhamira**. Pia, uhakiki wa kazi za fasihi huzingatia mafunzo yanayotokana na wazo kuu linalozungumziwa. Mafunzo hayo huitwa **ujumbe**. Mwandishi pia huzingatia **migogoro**, yaani tofauti za kimawazo au kimaisha zinazojitokeza baina ya wahusika. Hivyo, mhakiki huchambua sababu, mdhihiriko, na masuluhisho ya migogoro iliyojitokeza.

Hali kadhalika, mhakiki huchambua namna mwandishi anavyodhihirisha tafakuri yake kuhusu maisha. Tafakuri hiyo ya kina kuhusu vipengele vya maisha hujulikana kama **falsafa**. Pia, mhakiki huchambua **msimamo** wa mwandishi, yaani jinsi mwandishi anavyotetea na kusimamia bila kutetereka mambo anayowasilisha. Aidha, mhakiki huchambua **mtazamo** wa mwandishi, yaani jinsi anavyoyaona mambo na kuyawasilisha.

Pamoja na hayo, mwandishi huonesha mawazo na imani aliyonayo kuhusu uhusiano wa watu katika jamii. Mawazo na imani ya mwandishi kuhusu uhusiano wa watu katika jamii huitwa **itikadi**. Kipengele hiki pia huchambuliwa na mhakiki ili kuona namna imani hiyo inavyojitokeza katika kazi husika.

## Kazi ya 3.5

Kwa kuzingatia maelezo na mifano ya mashairi yaliyomo katika sura hii, kusanya mashairi yasiyopungua sita, kisha chambua maudhui na fani katika kila shairi.

**Zingatia**

Ushairi, kama utanzu mmojawapo wa fasihi andishi, una sifa bainifu zinazoutofautisha na tanzu zingine. Sifa mojawapo ya msingi ni matumizi ya lugha ambayo hujidhihirisha katika mambo mbalimbali. Kwanza, ushairi huwasilisha maudhui yake kwa maneno machache na kwa muhtasari, yaani kwa uwekevu. Mwandishi wa kazi ya ushairi huweza kutumia maneno machache kwa ustadi kuelezea dhana pana, tofauti na tanzu zingine za fasihi. Pili, ushairi huhusisha lugha ya mkato, mficho, picha, tamathali za semi, misemo, na mafumbo ili kuleta mvuto wa kazi ya ushairi pale inaposomwa.

Tatu, ushairi hutumia lugha iliyo tofauti na lugha ya kawaida, ikiwa ni pamoja na uwezo wa kufupisha au kurefusha maneno bila kukiuka misingi ya Kiswahili. Sifa nyingine ya ushairi ni uhuru wa kutumia mpangilio wa maneno ulio kinyume na utaratibu wa kisarufi uliozoeleka ili kuleta mtiririko mzuri wa mawazo kwa lengo la kueleza tukio au hisia fulani kuhusu maisha.

Aidha, kazi ya ushairi hujitosheleza kimaana kupitia mshororo na ubeti. Hivyo, ubeti wa shairi hubeba maana fulani iliyokusudiwa. Utoshelevu huweza kujitokeza hata katika mshororo.

## Kazi ya 3.6

**Soma beti zifuatazo, ambazo ni sehemu ya utenzi, kisha chambua vipengele vya fani na maudhui.**

**Mwanangu**

Ninalo jambo moyoni,
Takufaa maishani,
Njoo hapa barazani,
Nipate kukuusia.

Ufungue masikio,
Nikupatie funguo,
Kikuepuke kilio,
Nisemayo zingatia.

Dunia sasa yendavyo,
Mambo yake yawa hovyo,
Imekuwa ndivyo sivyo,
Kicheza taangamia.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 40 07/03/2022 16:50

Kwanza uache papara,
Tamaa ikakufura,
Sihadaike na sura,
Yakuti nazo rupia.

Mamia tumewazika,
Dunia ikiwacheka,
Kuwafika walotaka,
Mwishowe wakajifia.

Walikufa watu wale,
Wakatangulia mbele,
Waliona ni kelele,
Mema ukiwaambia.

Walipukutika hasa,
Kiendekeza anasa,
Kifo kiliwapangusa,
Dawamu wamepotea.

Basi tukaomboleza,
Mola pema kuwalaza,
Kaburini wakaoza,
Mwisho wa kusimulia.

Basi mwanangu elimu,
Ndicho kitu cha muhimu,
Uishike kwa nidhamu,
Mwanangu wanisikia?

Yataka uvumilivu,
Pia uwe msikivu,
Tena uache uvivu,
Elimu kuiendea.

Wengi walovumilia,
Sasa wanafurahia,
Matunda kujipatia,
Leo wanajichumia.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 41 07/03/2022 16:50

Wanajipiga fuadi,
Walokuwa wakaidi,
Kuiacha makusudi,
Shule wakaijutia.

Ina machungu dunia,
Usije ukajitia,
Kila kitu unajua,
Kumbe waungua jua.

Sasa kunena nakoma,
Kiwa me'sikiza vema,
Haikufiki zahama,
Ukaushike wosia.

## Zoezi la 3.1

1. Fafanua dhana zifuatazo:
   (a) Mshororo
   (b) Kituo bahari
   (c) Muwala
   (d) Kina
2. Kwa kutumia mashairi kutoka diwani teule, fafanua namna unavyoweza kutofautisha kazi ya mwandishi mmoja na mwingine.
3. Bainisha tofauti kati ya ngonjera na vipera vingine vya ushairi.
4. Eleza tofauti zisizopungua tano baina ya tenzi na mashairi.
5. Fafanua dhamira mbili zilizosawiriwa katika beti za sehemu ya utenzi uliousoma.

## Kuhakiki tamthiliya

### Kazi ya 3.7

**Soma kipande kifuatacho cha tamthiliya, kisha jibu maswali yanayofuata.**

*(Majira ya saa nane mchana, katika kijiji cha Ndatu, Mama Rumuli akiwa anafua sare za wanawe wa kiume huku akiimba.)*

**Mama Rumuli**: Tuwape elimu wanetu wa kiume, watusaidie maishani. (*Ghafla anasikika mtu akibisha hodi.*)



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 42 07/03/2022 16:50

**Mama Kazamwendo**: Hodi wenyewe!

**Mama Rumuli:** (*Anasimama huku akiitikia*.) Karibu Mama Kazamwendo! Habari za siku nyingi?

**Mama Kazamwendo:** (*Huku akitabasamu*) Salama rafiki yangu. Naona unafua nguo za shule za Yumbu na Kronto, za Rumuli ziko wapi?

**Mama Rumuli:** (*Anacheka kwa kejeli huku akishika kiuno*.) Ha ha haaaa! Weee! Mtoto wa kike shule ya nini bwana we!

**Mama Kazamwendo:** (*Huku akimshangaa rafiki yake*) Unazungumza nini Mama Rumuli? Unamaanisha hujampeleka shule binti yako Rumuli?

**Mama Rumuli:** (*Huku akibeza*) Weeee! Thubutu! Mimi na mume wangu hatuwezi kumpeleka mtoto wa kike shule hata siku moja. Atasaidia kazi za nyumbani na kuwapikia kaka zake wanaokwenda shuleni.

**Mama Kazamwendo:** (*Anaonekana akisikitika*.) Sikiliza nikwambie kitu Mama Rumuli. Watoto wote wana haki ya kusoma. Haijalishi ni wa kike au wa kiume kwani wote watatusaidia sisi wazazi na wao watanufaika hapo baadaye.

**Mama Rumuli:** Hapana! Hapana! Mama Kazamwendo, kumsomesha mtoto wa kike ni hasara kwani ataolewa na kwenda kufaidisha ukoo mwingine, au anaweza kubeba ujauzito masomoni. Sasa, yote hayo ya nini?

**Mama Kazamwendo:** (*Huku akimsisitiza rafiki yake*) Hakuna ukweli wowote katika hayo unayoyasema rafiki yangu. Watoto wa kike wakipewa elimu sawa na wa kiume, watatusaidia sote na jamii kwa ujumla na kuondoa kizazi tegemezi.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 43 07/03/2022 16:50

**Mama Rumuli:** Mimi sikubaliani na wewe hata kidogo.

**Mama Kazamwendo**: Mimi na mume wangu tunamsomesha binti yetu Kazamwendo, na sasa, yuko masomoni nje ya nchi. Rafiki yangu, achana na mawazo hayo potofu. Elimu ni muhimu kwa jinsi zote. (*Mama Kazamwendo anaonesha amemaliza maongezi. Anamuaga shoga yake na kuondoka*.)

**Mama Rumuli:** (*Ni siku ya Jumatatu saa 11:00 alfajiri. Mama Rumuli anamwamsha Rumuli ili awaandalie kaka zake chai wanywe kabla ya kwenda shuleni, huku akifoka.*) Wee Rumuli! Amka haraka uwaandalie kaka zako chai wasichelewe shule!

**Rumuli**: (*Anaitikia huku akinung'unika.*) Sawa mama!

**Yumbu**: (*Anaongea kwa kufoka.*) We Rumuli! Hayo maji ya kuoga bado tu? Fanya haraka tunataka kuwahi shule!

**Rumuli:** (*Anaacha kupika na kumpelekea kaka yake maji bafuni.*) Kaka maji tayari.

**Yumbu:** (*Kwa hasira*) Tuandalie na hiyo chai haraka! Tunachelewa shule!

**Rumuli:** (*Anaandaa chai mezani, kisha anawakaribisha*.) Chai iko tayari, karibuni!

**Kronto na Yumbu**: (*Wanakunywa chai wakiwa wamevalia sare zao za shule, kisha wanamuaga mama yao*.) Kwa heri mama! Tutaonana baadaye.

**Mama Rumuli**: Sawa! Mkasome kwa bidii. (*Baada ya kuagana na Kronto na Yumbu, anamgeukia Rumuli.*) Uoshe vyombo walivyotumia kaka zako. Pia, ufagie uwanja. Ukimaliza, uende shambani.

**Rumuli:** (*Majira ya saa 12:00 jioni, anarudi kutoka shambani huku akiwa amechoka. Anamkuta baba yake naye amerudi kutoka kazini.*) Shikamoo baba!

**Mzee Mbigi**: (*Anaitikia huku akimwangalia Rumuli.*) Marahaba! Rumuli nahitaji chakula. Njaa inaniuma sana.

**Rumuli:** (*Anaitika kwa unyonge.*) Sawa baba, ninakwenda kupika sasa hivi. Baada ya nusu saa, chakula kitakuwa tayari.

**Mama Rumuli:** (*Anaingia na kuuliza kwa sauti ya ukali.*) Wee Rumuli! Nina njaa sana! Chakula kiko tayari?

**Rumuli:** (*Anajibu kutoka jikoni.*) Ndiyo ninapika hivi sasa mama.

**Mama Rumuli:** Haya, fanya haraka!

(*Baada ya chakula kuiva, anawaandalia wazazi wake mezani, kisha anawakaribisha, na wote watatu wanajumuika mezani.*)

**Rumuli:** (*Wakiwa mezani*) Baba na mama, hivi mimi sina haki ya kwenda shuleni kama kaka zangu? Mimi ninafanya kazi zote hapa nyumbani, lakini kaka zangu wakirudi kutoka shuleni hula na kwenda kucheza …

**Mama Rumuli:** (*Anaingilia mazungumzo.*) Tena ishia hapo! Umekosa adabu! Nani amekuruhusu kuzungumza hivyo? Mwiko kumsomesha mtoto wa kike kwa kuwa hakuna faida yoyote tutakayoipata kutokana na kumsomesha.

**Mzee Mbigi:** Kweli mke wangu! Tena inabidi atafutiwe mchumba mapema asije kutuletea balaa huyu. (*Wote wanamaliza kula na kwenda kulala.*)



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 45 07/03/2022 16:50

(*Baada ya miaka mitano, Kazamwendo anarudi kutoka masomoni akiwa amehitimu shahada ya udaktari. Anawasili uwanja wa ndege na kupokelewa kwa furaha na wazazi wake*.)

**Mama Kazamwendo:** (*Akiwa na furaha*) Karibu sana binti yangu! Ni muda mrefu toka ulipoondoka kwenda nje ya nchi kimasomo. (*Mzee Chioko naye anadakia kwa kumkaribisha binti yao.*)

**Kazamwendo**: (*Akiwa anatabasamu*) Asanteni sana wazazi wangu! Nimefurahi sana kuwaona baada ya muda mrefu. Ninawashukuru sana kwa kunisomesha bila kujali jinsi yangu.

**Mzee Chioko:** (*Akimtazama bintiye*) Hongera sana binti yangu kwa kuwa umewawakilisha vyema watoto wa kike hapa kijijini kwetu.

**Kazamwendo:** Asante sana baba! Lakini unamaanisha nini kusema nimewawakilisha vyema?

**Mama Kazamwendo:** Umetuwakilisha vyema mwanetu. Wakazi wa kijiji chetu wanaamini kwamba kumsomesha mtoto wa kike ni hasara; hivyo, wanawabagua na kuwasomesha watoto wa kiume tu.

**Mzee Chioko:** (*Akimuunga mkono*) Kweli kabisa! Jirani yetu Mama Rumuli alikataa kabisa kumsomesha Rumuli. Hatimaye, walimwoza binti yao na kumsababishia maisha ya kunyanyasika kutokana na kukosa elimu.

**Mama Kazamwendo:** Si hivyo tu mume wangu, Yumbu na Kronto, kaka zake Rumuli, walipelekwa shule eti kwa sababu ni watoto wa kiume. Kilichotokea, wameshindwa mitihani kwa sababu hawakuzingatia masomo. Bora wangemsomesha Rumuli pengine angefanya vizuri na kuwasaidia.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 46 07/03/2022 16:50

(*Mama Rumuli na mume wake wanapata taarifa ya ujio wa Kazamwendo na kuwa amefanya vyema. Amehitimu shahada yake ya udaktari na amepangiwa kazi katika hospitali ya wilaya yao*.)

**Mama Rumuli:** (*Akiongea kwa masikitiko*) Mume wangu, bora tungempeleka mtoto wetu wa kike shuleni; ona tulimwoza na amenyanyasika huko. Sasa, amefukuzwa na mume wake. Ameshakuwa mzigo kwetu.

**Mzee Mbigi:** Ni kweli mke wangu. Kama nasi tungemsomesha mtoto wetu kama majirani zetu walivyofanya kwa binti yao, tungekuwa mbali. Tena, nimesikia Kazamwendo amewajengea wazazi wake jumba la kifahari na anawasaidia ndugu zake. (*Wote wanasikitika kwa kumnyima binti yao nafasi ya kusoma*.)

## Maswali

1. Pendekeza kichwa cha kipande cha tamthiliya ulichokisoma.
2. Fafanua sifa za tamthiliya.
3. Kwa kutumia sentensi tatu, eleza kama ungekuwa Mama Rumuli ungefanya nini baada ya kuona kilichompata Rumuli.
4. Bainisha wahusika waliojitokeza katika kipande hicho cha tamthiliya.
5. Eleza ujumbe ulioupata kutoka kipande cha tamthiliya ulichokisoma.
6. Fafanua mandhari ya utendaji katika kipande hicho cha tamthiliya.
7. Unajifunza nini kupitia mhusika Kazamwendo?

**Zingatia**

Tamthiliya ni njia mojawapo ya kuwasilisha maudhui. Mwandishi huteua wazo, kisha kuliwasilisha katika umbo la tukio litakaloweza kutendeka mbele ya hadhira. Hivyo, tamthiliya ni mchezo wa kuigiza ulioandikwa ili utendwe jukwaani au usomwe na hadhira kwa lengo la kufikisha ujumbe. Tamthiliya huigizwa na wahusika wa pande mbili au zaidi zinazokinzana. Ukinzani unaokuwapo husababishwa na wahusika ambao hujenga visa mbalimbali vinavyoleta au kukuza mgogoro ambao, ukitatuliwa, mchezo huwa umefika mwisho. Tamthiliya huweza kusomwa tu bila kuigizwa. Inapoigizwa, huitwa drama. Pia, tamthiliya hutegemea zaidi vitendo. Aidha, tamthiliya hutawaliwa na majibizano baina ya wahusika kutokana na dhana inayotendeka. Majibizano hayo baina ya wahusika hudokeza uhusiano wao, mitazamo yao, hisia zao, na kadhalika. Vilevile, huwa na muktadha maalumu wa kutendea jambo lililokusudiwa kutendwa. Pia, huwa na umithilishaji, yaani ubunifu kutegemeana na jambo linalotendwa. Tamthiliya hujumuisha wahusika, ambao ndio watendaji wa matendo mbalimbali kulingana na matakwa ya mwandishi na hadhira.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 47 07/03/2022 16:50

## Kazi ya 3.8

**Soma kipande kifuatacho cha tamthiliya, kisha jibu maswali yanayofuata.**

(*Katika kijiji cha Tupendane, Bwana Lutendege yupo nyumbani kwake anakagua banda la mifugo yake. Kisha, anaingia katika ghala alimohifadhi mazao waliyoyavuna. Anatazama rundo la magunia yaliyojaa nafaka na kupangwa vizuri, kisha anatikisa kichwa kwa masikitiko.*)

**Bwana Lutendege**: Mama Vuvuzela!

**Kazide:** Abee! Mume wangu.

**Bwana Lutendege:** Vuvuzela amekwenda wapi?

**Kazide:** Sina uhakika, lakini ninafikiri ameongozana na Galino ambaye nimemtuma akateke maji kisimani.

**Bwana Lutendege:** Haya mke wangu! Chukua mkeka ndani tukakae pale chini ya mti tuzungumze.

**Kazide:** Sawa mume wangu!

**Bwana Lutendege:** Usichelewe. Ni jambo muhimu.

**Kazide:** Ninakuja sasa hivi. (*Anafika na mazungumzo yao yanaanza.*)

**Bwana Lutendege:** Mke wangu, nimekuita hapa ninataka nikushirikishe jambo kuhusu mazao yetu.

**Kazide:** Ndiyo mume wangu!

**Bwana Lutendege:** Tumefanikiwa kupata mazao mengi msimu huu, lakini, kama unavyoona, bei ipo chini sana hapa kijijini. Hatuwezi kupata faida kubwa kama matarajio yetu.

**Kazide:** Kweli mume wangu, lakini … Sasa tutayauza wapi?

**Bwana Lutendege:** Usiwe na wasiwasi.

**Kazide:** Mmmh! Mimi ninakusikiliza wewe tu mume wangu.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 48 07/03/2022 16:50

**Bwana Lutendege:** Tutauza mazao yetu mjini.

**Kazide:** Mjini? Tunamjua nani huko mume wangu?

**Bwana Lutendege:** Unamkumbuka Sindile?

**Kazide:** Si yule mtoto wa Mzee Katundu wa pale bondeni?

**Bwana Lutendege:** Haswaaa! Huyohuyo ndiye atakayetusaidia.

**Kazinde:** Umewasiliana naye?

**Bwana Lutendege:** Hapana! Ila tukimaliza kuzungumza nitafanya hivyo.

**Kazinde:** Sawa mume wangu!

**Bwana Lutendege:** (*Baada ya mazungumzo yao, anawasiliana na Sindile ili kumweleza kuhusu kuuza mazao yao mjini.*) Habari za siku Sindile?

**Sindile**: Nzuri, shikamoo Bwana Lutendege!

**Bwana Lutendege:** Marahaba! Hujambo?

**Sindile:** Sijambo kabisa! Vipi huko kijijini mnaendeleaje?

**Bwana Lutendege:** Tunamshukuru Mungu, tunaendelea vizuri.

**Sindile:** Hongereni sana, maana ninasikia mwaka huu mmepata mavuno mengi.

**Bwana Lutendege:** Kweli kabisa, lakini huku bei ipo chini sana kutokana na watu kupata mavuno mengi.

**Sindile:** Huku mjini mahitaji ni makubwa sana kwa sababu watu wengi wanashindwa kusafirisha mazao yao kuleta huku.

**Bwana Lutendege:** Basi ninaomba unifanyie mpango ili niweze kuleta mazao yangu huko kwa ajili ya kuuza.

**Sindile:** Hakuna neno mzee. Wewe jiandae kuja. Suala la soko lisikupe shida maana wanaohitaji mazao ni wengi.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 49 07/03/2022 16:50

**Bwana Lutendege:** Nitashukuru sana nikifanikiwa kuuza.

**Sindile:** Hakuna neno mzee. We njoo tu.

(*Sindile na Bwana Lutendege wapo nje ya soko kuu la mazao la wilaya. Bwana Lutendege anaonekana akiwa na furaha baada ya kufanikiwa kuyasafirisha na kuyauza mazao yake hapo mjini.*)

**Sindile:** (*Anampa mkono wa pongezi Bwana Lutendege kwa kufanikiwa kuuza mazao yake yote.*) Hongera sana Mzee Lutendege!

**Bwana Lutendege:** Mwanangu Sindile, ninakushukuru sana kwa kunisaidia. Nimeuza mazao yangu kwa bei nzuri.

**Sindile:** Usijali Bwana Lutendege. Undugu ni kufaana; si kufanana.

**Bwana Lutendege:** Pokea pesa hizi kama shukurani yangu kwako.

**Sindile:** Asante sana! (*Anapokea pesa na kumwambia Mzee Lutendege waende wakajipongeze kwa kunywa pombe.*)

**Bwana Lutendege:** (*Wakiwa baa*) Ha! ha! ha! ha! Pombe? Safi sana.

**Sindile:** (*Huku wakiendelea kunywa pombe*) Haya ndiyo maisha ya mjini Bwana Lutendege!

**Bwana Lutendege:** Ha! ha! haaaa! Sawa, hakuna shida. Naomba kesho tubadilishe, twende tukanywe na kuonja nyama mahali pengine. (*Anavutiwa na maisha ya mjini ya starehe na kuisahau kabisa familia yake.*)

**Sindile:** Hakuna shida. Nitakupeleka. Sehemu ziko nyingi sana. Utachoka mwenyewe. Tumia pesa Bwana Lutendege. Kumbuka, tunaishi mara moja tu.

(*Miezi saba imepita Lutendege bado hajarudi. Vuvuzela na Galino pamoja na mama yao, Kazide, wapo nyumbani kwao, kijijini Tupendane, wamepumzika, huku wakiendelea na maongezi.*)

**Vuvuzela:** Mama, mbona baba harudi?

**Kazide:** Atarudi mwanangu. Yuko mjini anatafuta pesa.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 50 07/03/2022 16:50

**Galino**: Siku zote hizo! Pesa gani hizo?

**Kazide:** Ndiyo, pesa zinatafutwa kila siku mwanangu.

**Vuvuzela:** Sawa mama, usiku mwema!

**Kazide:** Haya wanangu! Kalaleni msisahau kuzima kibatari.

**Galino**: Sawa mama! (*Vuvuzela na Galino wanamuaga mama yao na kwenda kulala*.)

**Kazide:** (*Asubuhi sana, Kazide amefika nyumbani kwa Mzee Katundu.*) Habari za asubuhi Mzee Katundu!

**Mzee Katundu**: Nzuri Mama Vuvuzela, kwema?

**Kazide:** Kwema kidogo Mzee Katundu. Ninaomba unipatie namba za Sindile, ninamtafuta mume wangu. Toka amekwenda mjini kutafuta soko hajarudi.

**Mzee Katundu:** Pole Kazide, Sindile hapatikani kwenye simu.

**Kazide:** Mmmh! Ina maana huna mawasiliano na mwanao kabisa?

**Mzee Katundu:** Ndiyo! Sina mawasiliano naye kwa takribani mwezi mmoja sasa.

**Kazide:** Hakuna hata namba ya simu ya jirani yake au rafiki yake?

**Mzee Katundu:** Hajawahi kunipigia kwa namba nyingine yoyote.

**Kazide:** Mmmh! Haya, basi ninaomba akipatikana umwambie amwambie Bwana Lutendege kwamba ninamtafuta.

**Mzee Katundu:** Sawa!

**Kazide:** Haya, siku njema! Msalimie Mama Sindile.

**Mzee Katundu:** Sawa! Nitamsalimia.

(*Bwana Lutendege na Sindile wamekaa nyumbani kwa Sindile wakiendelea na maongezi. Bwana Lutendege anaonekana mnyonge.*)

**Bwana Lutendege:** Mwanangu Sindile, ninataka nirudi nyumbani. Ninaona afya yangu si nzuri.

**Sindile:** Kweli! Hata mimi ninaona afya yako haiko sawa. Aidha, ni muda mrefu umepita. Nenda ukaione familia yako pia. Hata hivyo, ninakushauri uende hospitalini ukapate vipimo kwanza.

**Bwana Lutendege:** Sawa, basi ngoja nikapime afya kwanza!

**Sindile:** Sawa!

**Bwana Lutendege:** Haya baadaye!

**Sindile:** Sawa!

**Bwana Lutendege:** (*Akiwa hospitalini, katika chumba cha daktari. Amejiinamia baada ya kupokea majibu ya vipimo vyake.*) Mungu wangu! Daktari unasema kweli?

**Daktari**: Ni kweli Mzee. Majibu ya vipimo yanaonesha una maambukizi ya virusi vya UKIMWI. Hata hivyo, utapewa maelekezo ya jinsi ya kuishi katika hali hiyo.

(*Kijijini Tupendane, Lutendege anaingia nyumbani kwake akiwa amesawijika. Anapokelewa na mkewe, na kukalishwa chini.*)

**Kazide:** Mume wangu! (*Mke wake anamtazama na kumshangaa baada ya kuona afya yake ilivyodhoofika.*)

**Bwana Lutendege:** Mke wangu! (*Anadondosha machozi.*)

**Kazide:** Kuna shida gani mume wangu? Mbona unalia?

**Bwana Lutendege:** Nisamehe sana mke wangu. (*Anazidi kutokwa na machozi.*)

**Kazide:** Niambie kuna nini? Wewe ni mume wangu. Nimekusamehe hata kabla ya kujua shida ni nini.

**Bwana Lutendege:** Siku zangu za kuishi ni chache sana hapa duniani.

**Kazide:** (*Anapigwa na butwaa.*) Una maana gani mume wangu?

**Bwana Lutendege:** Mmh! Nisamehe sana. (*Anamsimulia mkewe jinsi alivyochezea pesa zote za mavuno yao kwa kuendekeza starehe za mjini hadi kupata UKIMWI.*)

**Kazide:** (*Anauliza kwa uchungu huku akitokwa na machozi.*) Umefanya nini mume wangu? Mbona umekwenda kinyume na makubaliano yetu?

**Bwana Lutendege:** Ninakiri nimekosa. Ninaomba unisamehe mke wangu.

## Maswali

1. Eleza ujumbe ulioupata kutoka katika kipande cha tamthiliya ulichokisoma.
2. Eleza wasifu wa wahusika watatu katika kipande hiki cha tamthiliya.
3. Fafanua ni kwa namna gani pombe na starehe ni adui wa maendeleo.
4. Umepata funzo gani kutokana na kipande cha tamthiliya ulichokisoma?

**Zingatia**

Tamthiliya huweza kuonekana katika sura za aina mbili: ya kuhuzunisha na kufurahisha. Tamthiliya inayohuzunisha huitwa *tanzia*. Katika aina hii ya tamthiliya, mhusika mkuu hupewa umaarufu na sifa nyingi zinazovutia. Pia, mhusika mkuu huweza kukabiliwa na shida au changamoto ambazo hujitahidi kuzitatua bila mafanikio. Hivyo, tamthiliya ya aina hii huishia kwenye masikitiko na anguko la mhusika mkuu. Tamthiliya inayofurahisha au kuchekesha huitwa *ramsa*. Katika aina hii ya tamthiliya, utani, kejeli, na mizaha hutumika zaidi katika kuchekesha. Mwisho wa tamthiliya ya aina hii huwa furaha. Mhusika mkuu wa ramsa anaweza kuwa mtu yeyote isipokuwa ni lazima abebe matendo ya ucheshi. Wakati mwingine, ramsa hujulikana kama *komedia* au *futuhi* kutokana na matendo ya ucheshi na vichekesho anavyovibeba mhusika mkuu.

## Kazi ya 3.9

**Soma tamthiliya teule mojawapo, kisha:**

(a) Eleza taarifa muhimu za maisha ya mwandishi wa tamthiliya uliyoichagua.

(b) Chambua vipengele vya fani na maudhui katika tamthiliya hiyo.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 53 07/03/2022 16:50

## Zoezi la 3.2

1. Bainisha vipengele vya fani katika tamthiliya.
2. Eleza tofauti kati ya tamthiliya za tanzia na ramsa.
3. Fafanua mambo yanayotofautisha tamthiliya na tanzu zingine za fasihi andishi.
4. Eleza sifa za tamthiliya.

## Kuhakiki riwaya

### Kazi ya 3.10

**Soma kipande kifuatacho cha riwaya ya *Hatima ya Maisha Yangu*, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Mzee Haruni na mkewe Lwiza wanaishi katika Kijiji cha Isoka. Haruni na mkewe wamejaliwa kupata watoto wanne. Watatu wa mwanzo ni wa kiume ambao ni: Kija, Mkwaju, na Panta, na wa mwisho wa kike anaitwa Maisara. Maisara ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Maputo. Mzee Haruni ana dada yake, ambaye ni shangazi wa watoto wake, anayeitwa Yembe. Shangazi Yembe amejaliwa mtoto mmoja tu, anayeitwa Tensa. Familia ya Mzee Haruni iliishi pamoja kwa upendo na furaha.

Shangazi Yembe hakuwa mtu mzuri. Aliionea wivu familia ya Mzee Haruni kutokana na mashamba na mali walizokuwa nazo. Yeye alitaka amiliki mashamba na mali zote za kaka yake. Aliona njia pekee ya kumiliki mali za nduguye ni kumuua Mzee Haruni na mkewe. Kutokana na wivu na uchu wa mali aliokuwa nao Yembe, hakufikiria kabisa hatima ya Maisara na kaka zake ambao maisha yao yote yalitegemea wazazi wao.

Siku moja, Mzee Haruni na mkewe walikwenda kumtembelea Yembe nyumbani kwake. Hawakujua hila aliyokuwa nayo. Shangazi Yembe aliwaandalia Haruni na mkewe chakula kizuri. Alichanganya na sumu ndani yake, akawakaribisha, wakala, kisha wakaaga na kuondoka. Walipofika nyumbani kwao jioni, wakalala kwa uchovu wa shibe waliyokuwa nayo. Hawakuamka tena. Walilala usingizi wa milele. Azma ya shangazi ikatimia.

Habari za msiba wa Haruni na mkewe zilisambaa kijijini kwa haraka kama moto nyikani. Maisara na nduguze waliomboleza vifo vya wazazi wao kwa masikitiko makubwa. “Janga hili halikupaswa kutupata kwa sasa kwani bado tulikuwa tunawahitaji sana wazazi wetu. Tutakuwa wageni wa nani sisi?” Walisikika wakiomboleza. Siku zikapita, kisha majuma na hatimaye miezi, maisha yakaendelea.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 54 07/03/2022 16:50

Kweli, *duniani kuna watu na viatu*. Mara baada ya maombolezo ya msiba wa Mzee Haruni na mkewe Lwiza kuisha, Shangazi Yembe akaibuka na kudai apewe hati za viwanja na mashamba yote. Alidai kuwa Maisara na kaka zake walikuwa bado wadogo. Hivyo, wasingeweza kuzitunza mali za wazazi wao. Jitihada za Kija, Mkwaju, na Panta kuzuia mali za wazazi wao zisichukuliwe ziligonga mwamba kwa kuwa Shangazi Yembe aliambatana na mtoto wake, Tensa, pamoja na mwanasheria. "Shangazi, hiki unachotufanyia si sahihi hata kidogo. Baada ya pigo kubwa la kuondokewa na wazazi wetu, unatunyang'anya mali?" Kiza, ambaye ni kaka mkubwa wa Maisara, aliuliza kwa huzuni. "Nawaachia nyumba ya kuishi. Kwa nini hamna shukurani?" Aliuliza Shangazi Yembe kwa sauti ya ukali. "Kabidhi hati hizo haraka! Msinicheleweshe," aliamuru mwanasheria.

Bila aibu wala huruma, Shangazi Yembe akamiliki mali za kaka yake. Alijenga nyumba ya kifahari mjini ambako aliishi yeye na mwanawe, Tensa. Wakafanya starehe za kila aina, wakizifuja mali bila kuwakumbuka hata watoto wa mwenye mali.

Baada ya miezi kadhaa kupita, Maisara alihitimu kidato cha nne. Kwa bahati nzuri, pamoja na changamoto ya kupoteza wazazi wake wote wawili kwa mpigo, alifaulu vizuri katika mitihani yake. Alichaguliwa kuendelea na masomo ya kidato cha tano. Taarifa za matokeo mazuri ya mitihani ya Maisara zilipokelewa na Maisara mwenyewe na kaka zake kwa shangwe. Hata hivyo, punde, furaha yao iliyeyuka baada ya kukumbuka kuwa hawakuwa na fedha kwa ajili ya kununua mahitaji mbalimbali ya shule ili kumwezesha Maisara kuendelea na masomo ya kidato cha tano.

Kija alimsihi Shangazi Yembe awasaidie kulipa ada ya Maisara ili aendelee na masomo yake. Shangazi aliwapa kisogo, wala hakuwatazama mara mbili. Hatimaye, licha ya mali zote walizokuwa nazo wazazi wao, Maisara alishindwa kuendelea na shule kwa sababu ya kukosa ada.

Maisha ya Kija na wenzake yaliendelea kuwa magumu kwani hawakukosa tu pesa kwa ajili ya ada ya dada yao, bali pia chakula. Jioni moja, Mkwaju na Panta walikuwa wamekaa nje ya nyumba yao wakiwaza na kuwazua. "Haya maisha yataendelea hivi mpaka lini? Mateso haya jamani yataisha lini?" Alilalama Panta. "Ningekuwa na uwezo ningewafufua baba na mama," aliongeza Mkwaju. "Acha kuwaza yasiyowezekana kaka. Uwafufue wazazi kwani wewe umekuwa Mungu?" Alihoji Panta, kisha akasema kama mtu azindukaye kutoka ndotoni:

"Nimepata wazo Mkwaju."
"Unaota mchana Panta! Wazo gani?"
"Utalipenda hili wazo Mkwaju nakwambia."
"Usinitie kiwewe. Nimekuuliza wazo gani?"



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 55 07/03/2022 16:50

"Ngoja kwanza nikuulize, unamfahamu yule jamaa yetu?"

"Badala ya kujibu swali unaongeza swali! Jamaa wapo wengi. Unamaanisha yupi?"

"Dumi, unampata?"

"Acha kuuliza majibu. Dumi anahusikaje sasa na majanga yetu?"

"Anaweza kutusaidia."

"Kwa vipi? Usikute unataka kusema …"

"Ndiyo, hujakosea. Nataka kusema tumwoze dada yetu Maisara kwa rafiki yetu Dumi."

Mkwaju na Panta walibishanabishana hapo wee, baadaye wakakubaliana wamshirikishe kaka yao Kija ili wapate mawazo yake. Ingawa Kija hakulipenda kabisa wazo la Maisara kuolewa badala ya kuendelea na shule, aliunga mkono kwa sababu hakuwa na jinsi. "Dumi ana uwezo wa kifedha. Labda dada yetu atakuwa na furaha kuolewa na bwana mwenye pesa hata kama hampendi. Huenda Dumi atatusaidia na sisi mashemeji zake kujikwamua kimaisha maana taabu hizi zimezidi jamani. Ngoja nitaongea na Dumi kuhusu mpango huu kabla sijaongea na Maisara." Kija aliwaza kimyakimya.

Dumi alilipokea kwa mikono miwili wazo la kumwoa Maisara baada tu ya kupewa wazo hilo. Maisara alikuwa mzuri wa sura na tabia. Alilelewa kwa kufuata maadili ya Kiafrika. Alikuwa mwenye adabu, mpenda watu, mcheshi, na mchapa kazi. Dumi asingeweza kukataa fursa iliyojileta yenyewe hadi miguuni kwake. "Ukisikia mtu ana bahati ya mtende, basi ndiyo mimi sasa," Dumi aliwaza kimyakimya. Alitoa mahari kwa kaka mkubwa wa Maisara. Kwa shingo upande, Maisara akakubali kuolewa na bwana asiyempenda. Dumi na Maisara wakawa mume na mke.

Dumi alimchukua mkewe wakaenda kuishi mjini. Maisha ya mjini yalikuwa mazuri ndani ya jumba zuri la kifahari lenye kila aina ya vyakula na mahitaji mbalimbali. Kidogokidogo, Maisara akaanza kuzoea maisha ya kitajiri, ijapokuwa wazo la kuendelea na shule halikumtoka akilini.

Baada ya miezi kadhaa, Maisara akaanza kuona tabia ya Dumi ikibadilika. Alianza kurudi nyumbani usiku wa manane tena akiwa amelewa. Dumi akaanza kumshawishi mkewe kwenda kwenye kumbi za starehe kunywa pombe. Maisha ya aina hii yalikuwa mageni kwa Maisara; hivyo, alikataa kuambatana na mumewe kama alivyotaka. Yakaibuka mabishano ndani ya nyumba yao. Walivurugana kiasi cha kutoweza kuendelea kukaa pamoja. Dumi akaamua kumfukuza Maisara, "Toka mshamba mkubwa wewe! Rudi kijijini ndiko kunakokufaa! Hufai kuwa mke wangu. Toka lini *jogoo la shamba likawika mjini*?" Dumi alifoka huku akitupa nguo za mkewe nje. "Mama nipe radhi, kuishi na watu kazi," alisema Maisara akiinama na kuokota nguo zake huku akilia kwa kwikwi.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 56 07/03/2022 16:50

Maisara alikaa nje ya nyumba yao akiwa amechanganyikiwa. Hakujua pa kwenda. Hakutaka kabisa kurudi kijijini kwa kuwa alihofia kaka zake wangemwoza kwa mtu mwingine. Ulikuwa wakati mgumu sana kwa Maisara. "Nimekukosea nini Mungu? Majanga baada ya majanga kana kwamba nilizaliwa kwa ajili ya majanga. Sina hata mwelekeo. Huyu aliyedhaniwa na kaka zangu kuwa suluhisho la matatizo ndiyo kwanza ametatiza maisha yangu zaidi. Yaani nimetoka kama nilivyoingia. Kweli *dunia tambara bovu*, halifai hata kudekia." Maisara alikuwa amezama kwenye dimbwi la mawazo.

"Habari yako dada? Uko sawa?" Aliibuliwa kutoka kwenye dimbwi la mawazo na sauti ya mpita njia aliyejulikana kwa jina la Zaki. "Kuna tatizo lolote? Naweza kukusaidia?" Zaki aliendelea kuhoji kwa upole ingawa maswali yake hayakujibiwa.

Maisara hakuwa na namna, isipokuwa kumweleza Zaki kila kitu kilichomtokea. Alimweleza jinsi wazazi wao walivyowaacha peke yao duniani. Akamweleza kuhusu shangazi yao aliyegeuka kuwa adui yao mkubwa. Alimweleza kuhusu kaka zake waliomtoa mhanga kwa sababu ya hali ngumu ya maisha waliyokuwa nayo. Zaki alisikiliza simulizi ya Maisara kwa makini na kwa masikitiko. Alimwonea huruma, akaahidi kumsaidia. Akamchukua kwenda naye nyumbani kwake akawa sehemu ya familia yake. Zaki alikuwa mtu anayependa kusaidia watu katika jamii ingawa hakuwa tajiri wa kupindukia. Alipenda kuona kila mtu akiwa na furaha, anafikia malengo yake na kutimiza ndoto yake. Kwa hiyo, alidhamiria kumsadia Maisara. Hakika wahenga walisema *kila ubaya una pacha ya uzuri*.

Baada ya Maisara kuishi katika familia ya Zaki kwa miezi kadhaa, alifunga safari kwenda kijijini kwao. Aliwakuta kaka zake wakiwa wanaendelea kupambana na hali zao. Maisara aliwaeleza kila kitu kilichotokea. Kaka zake walisikitika sana. Walijutia uamuzi wao wa kumwoza dada yao kwa Dumi. Wakamwomba msamaha, akawasamehe. Maisara akarudi mjini kuendelea na maisha katika familia ya Zaki.

Wahenga walisema *ukimficha jogoo pakachani, kuna wakati atawika*. Hatimaye, siri ya shangazi Yembe ikafichuka. Yembe alipatwa na matatizo ya akili, akaropoka na kusema kila kitu alichokifanya huko nyuma. Maisara na kaka zake wakabaini kuwa shangazi yao ndiye aliyewaua wazazi wao kwa kuwawekea sumu kwenye chakula ....

## Maswali

1. Bainisha mambo ya msingi anayozungumzia mwandishi katika kipande cha riwaya ulichokisoma.
2. Mambo anayoyajadili mwandishi katika kipande hiki cha riwaya yana umuhimu gani kwa jamii?



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 57 07/03/2022 16:50

3. Fafanua matukio matatu yaliyojitokeza katika kipande cha riwaya ulichokisoma.
4. Chagua tukio moja lililokugusa kati ya matukio uliyoyabainisha katika swali la 3. Kama ungekuwa mhusika wa tukio hilo ungefanya nini?

**Zingatia**

Masimulizi marefu ya kubuni yenye muundo, mtindo maalumu, uchangamani wa matukio, pamoja na ujenzi wa wahusika wenye kusawiri ukweli kuhusu maisha huitwa riwaya. Riwaya ina sifa ya kuwa ndefu kwani huchanganya visa vingi vidogovidogo ambavyo, kwa ujumla wake, hukamilisha kisa kikuu kimoja. Urefu wa riwaya pamoja na uchangamani wake ndiyo sababu ya kutumia nyenzo ya uandishi kwani si rahisi kukumbukika na kusimulika kwa mdomo kama zilivyo tanzu zingine. Pia, huhusisha wahusika wengi, huwa na mandhari mahususi, na visa vyake huwa vinatendeka katika wakati fulani.

## Kazi ya 3.11

Chambua vipengele vya fani na maudhui katika kipande cha riwaya ulichokisoma katika kazi ya 3.10.

**Zingatia**

Katika uhakiki wa riwaya, mhakiki huchambua vipengele vya fani na maudhui kwa kuangalia mambo mbalimbali yaliyojitokeza katika kujenga visa vya riwaya hiyo. Kwa upande wa fani, riwaya hujengwa na muundo, mtindo, wahusika, mandhari, pamoja na matumizi ya lugha. Muundo, katika riwaya, hujumuisha mpangilio wa visa na matukio. Muundo huweza kuwa wa moja kwa moja, yaani kuanza na kisa cha kwanza hadi cha mwisho. Aidha, mwandishi anaweza kutumia muundo rejeshi, yaani kusimulia kwa kuanza na visa na matukio ya mbele, kisha kurejea kusimulia visa na matukio ya mwanzo. Pia, mwandishi anaweza kutumia muundo changamani, yaani kuchanganya visa na matukio katika kueleza kazi ya fasihi. Vilevile, mhakiki wa riwaya huchunguza namna ambavyo mwandishi ameipa kazi yake upekee unaoitofautisha na kazi za watunzi wengine. Upekee huo hujulikana kama mtindo. Mwandishi wa riwaya huweza kutumia mtindo wa masimulizi, majibizano, barua, shairi, na nyimbo. Hivyo, mhakiki anapaswa kuchunguza mtindo uliotumika katika kazi husika. Aidha, mhakiki huchambua wahusika waliotumika katika kazi ya fasihi. Wahusika ni viumbe wanaotumiwa na mwandishi kwa kuwapa sifa na tabia za watu waliopo katika jamii husika ili kufikisha ujumbe. Hivyo, wahusika wanaweza kuwa watu, wanyama, miti, mazimwi, majoka, au mawe. Kadhalika, mhakiki huchunguza mandhari, yaani mahali ambapo visa na matukio ya kifasihi hufanyika. Katika riwaya, mandhari huweza kuwa ya kijijini, mjini, mtoni, porini, shambani, baharini,



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 58 07/03/2022 16:50

au ya mahali pengine popote. Pia, mhakiki huchunguza lugha iliyotumika katika kazi ya fasihi. Mwandishi wa riwaya huweza kutumia tamathali mbalimbali za semi kama tashibiha, tashihisi, tashtiti, na kejeli kwa lengo la kuweka vionjo na mvuto katika kazi yake.

Kwa upande wa maudhui, mhakiki huchunguza na kuchambua dhamira, ujumbe, migogoro, mtazamo, falsafa, msimamo, pamoja na itikadi. Katika dhamira, mhakiki huchunguza mawazo ya mwandishi wa kazi ya fasihi. Kupitia mawazo hayo, mhakiki hubaini dhamira kuu na dhamira ndogondogo. Vilevile, mhakiki huchunguza kipengele cha ujumbe, yaani mafunzo yanayotokana na dhamira zilizopo katika kazi husika. Kipengele kingine cha maudhui ni mtazamo. Mhakiki hutakiwa kuchunguza namna ambavyo mwandishi huyachukulia mambo au matukio katika jamii anayoiandikia. Vilevile, kuna kipengele cha msimamo wa mwandishi. Katika kipengele hiki, mhakiki huchunguza namna mwandishi anavyoyatetea mambo anayoyaandikia. Kipengele kingine ni falsafa. Mhakiki huchambua imani ya mwandishi kuhusu vipengele mbalimbali vya maisha. Aidha, kuna kipengele cha migogoro. Katika kipengele hiki, kinachohakikiwa ni ukinzani unaojitokeza baina ya wahusika na namna unavyotatuliwa ili kupata suluhu. Mwisho ni kipengele cha itikadi, ambapo mhakiki huchunguza mawazo na imani aliyonayo mwandishi kuhusu mfumo wa uhusiano wa watu katika jamii.

## Kazi ya 3.12

Chagua riwaya mbili miongoni mwa riwaya teule, kisha linganisha na kulinganua dhamira zilizosawiriwa katika riwaya hizo.

**Zingatia**

Kuna aina kuu mbili za riwaya, ambazo ni riwaya pendwa na riwaya dhati. Riwaya dhati huchimbua na kuchambua matatizo au changamoto zilizopo katika jamii na kutafuta sababu, athari na namna ya kutatua matatizo au changamoto hizo. Changamoto hizo zinaweza kuwa za kifamilia, kisiasa, kitabaka au kiutamaduni. Riwaya dhati hulenga kumfikirisha msomaji na si kumburudisha tu.

Riwaya pendwa ni riwaya ambazo huandikwa kwa lengo la kumburudisha msomaji. Riwaya hizi husuka visa na matukio yake kwa namna ya kumsisimua msomaji. Mambo maarufu ambayo hutumiwa na waandishi wa riwaya pendwa katika kujenga visa na matukio ni kama vile upelelezi, mapigano, mapenzi, na ujasusi. Mara nyingi, hutumia wahusika walewale, hususani wahusika wakuu, katika masimulizi tofauti. Pia, hutumia zaidi mandhari ya mjini kuliko ya vijijini.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 59 07/03/2022 16:50

## Zoezi la 3.3

1. Bainisha sifa nne za riwaya pendwa.
2. Eleza mambo manne maarufu ambayo waandishi huyatumia katika kuandika riwaya pendwa ili kumburudisha msomaji.
3. Eleza tofauti kati ya riwaya dhati na riwaya pendwa.

**Zingatia**

Baada ya kuhakiki vipengele vyote vya fani na maudhui, mhakiki anapaswa kuchunguza kufanikiwa na kutofanikiwa kwa mwandishi katika kazi yake. Kufanikiwa na kutofanikiwa kwa mwandishi katika kuonesha ukweli hufafanuliwa kwa kuangalia ubora na udhaifu wa kazi ya fasihi. Kazi yoyote ya fasihi inaweza kuandikwa ikawa na ubora na/au udhaifu. Ubora na udhaifu wa kazi ya fasihi andishi hupimwa kwa kuzingatia vipengele vya fani na maudhui. Kwa upande wa maudhui, mhakiki hupima mambo yaliyosemwa ambayo tunayapata kwa kuchunguza vipengele vya maudhui. Tunaangalia kama dhamira zilizoibuliwa zina uhalisia kwa jamii iliyokusudiwa na zinaielimisha jamii hiyo. Pia, mhakiki hutakiwa kujiuliza kama kazi hiyo ina ujumbe unaofaa kwa jamii inayohusika. Vilevile, mhakiki huchunguza migogoro iliyoibuliwa kama inapewa masuluhisho sahihi na yanayoendana na maadili ya jamii husika. Ikiwa ndivyo, basi, mhakiki anaweza kusema kwamba mwandishi amefanikiwa, na, kinyume chake, mwandishi atakuwa hajafanikiwa.

Kwa upande mwingine, katika fani, tunapima jinsi mambo yalivyowasilishwa. Mhakiki anapaswa kuangalia kama mwandishi ameiumba kazi yake vizuri na ametumia mtindo sahihi. Mhakiki hujiuliza kama mwandishi ametumia lugha inayofaa, amewaumba wahusika wake vizuri na amechagua mandhari sahihi na ya kuvutia au la. Mhakiki akijiridhisha kuwa vipengele vyote vipo sawa, hufikia uamuzi kwamba mwandishi amefanikiwa, na, kinyume chake, mwandishi atakuwa hajafanikiwa katika kazi yake.

## Kazi ya 3.13

(a) Orodhesha riwaya pendwa nne na riwaya dhati nne unazozijua, kisha andika majina ya waandishi wa riwaya hizo.

(b) Soma riwaya teule mojawapo, kisha:

  (i) Andika taarifa muhimu za maisha ya mwandishi wa riwaya hiyo.

  (ii) Chambua vipengele vya fani na maudhui vilivyojitokeza katika riwaya hiyo.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 60 07/03/2022 16:50

## Zoezi la marudio

1. Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi:.
   (i) Tofauti ya kifani baina ya shairi la **Mama ni mama** na la **Kiswahili** ni ...............
      (a) urari wa vina na mizani
      (b) matumizi ya tamathali za semi
      (c) utoshelevu
      (d) matumizi ya lugha
      (e) matumizi ya picha

   (ii) Kipengele gani cha fani kati ya hivi vifuatavyo kinahusu silabi zenye sauti zinazofanana?
      (a) Mshorororo
      (b) Ubeti
      (c) Vina
      (d) Mizani
      (e) Utoshelevu

   (iii) Hadithi ndefu ya kubuni yenye uchangamani wa visa, wahusika, na mandhari huitwa ...............
      (a) tenzi
      (b) tanzia
      (c) tamthiliya
      (d) ramsa
      (e) riwaya

   (iv) Tamthiliya na tanzu zingine za fasihi andishi hutofautishwa na nini?
      (a) Ufasaha wa maneno machache
      (b) Utumizi wa lugha ya mkato na picha
      (c) Uwezo wa kubeba tanzu zingine
      (d) Urari wa vina na mizani
      (e) Matumizi ya vitendo na mazungumzo

   (v) Kipi kati ya hivi vifuatavyo si kipera cha fasihi andishi?
      (a) Ngonjera
      (b) Riwaya pendwa
      (c) Tanzia
      (d) Nyimbo
      (e) Mashairi

2. Oanisha maelezo yaliyopo katika Orodha **A** na dhana zilizopo katika Orodha **B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Imani na mawazo ya mwandishi kuhusu uhusiano wa watu katika jamii | A. muwala |
| (ii) Hali ya mwandishi kutetea mawazo yake bila kutetereka | B. itikadi |
| (iii) Uwiano wa mambo katika kazi ya fasihi | C. msimamo |
| (iv) Namna mwandishi anavyoyaona mambo kwa upana na kusimamia imani yake katika maisha | D. mtindo |
| (v) Humtofautisha mwandishi mmoja na wengine | E. falsafa |
| | F. mtazamo |
| | G. muundo |

3. Tofautisha dhana zifuatazo:
   (a) fani na maudhui
   (b) utenzi na shairi
   (c) tamthiliya na riwaya
   (d) muundo na mtindo
   (e) msimamo na mtazamo
   (f) ramsa na tanzia
4. Tumia shairi lolote kutoka diwani teule kufafanua namna shairi linavyojipambanua na tanzu za riwaya na tamthiliya.
5. Teua tamthiliya mbili kutoka katika tamthiliya teule, kisha hakiki muundo wa tamthiliya hizo.
6. Kwa kutumia mifano ya mashairi, riwaya, na tamthiliya iliyopo katika sura hii, linganisha na kulinganua matumizi ya wahusika.
7. Eleza vipengele vinavyohusiana na mwandishi ambavyo mhakiki anapaswa kuvichunguza kabla ya kuhakiki kazi yoyote ya fasihi.
8. Soma kwa makini sehemu ya riwaya ya *Hatima ya Maisha Yangu*, kisha hakiki muundo wake.
9. Kutokana na kipande cha tamthiliya ulichokisoma katika kazi ya 3.6, mwandishi ana maana gani anaposema *Undugu ni kufaana na si kufanana*?



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 62 07/03/2022 16:50

# Sura ya Nne

## Utungaji wa kazi za fasihi

**Utangulizi**

*Watu huweza kutumia fasihi kutoa maelekezo, mawazo, maoni au hisia zao kwa njia ya maandishi au mazungumzo. Utungaji wa kazi za fasihi huhusisha uibuaji wa mawazo na kuyawasilisha kisanaa. Katika sura hii, utajifunza mbinu na taratibu za kutunga mashairi ya kimapokeo. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kutunga mashairi, kukuza kipaji, kuelimisha, na kuburudisha jamii.*

### Dhana ya utungaji

**Kazi ya 4.1**

**Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Hodi nataka kujuza, nina mengi mzomzo,
Nataka kuyaeleza, yasokuwa na mzozo,
Sitaweza kunyamaza, taendekeza uozo,
Ninataka nena mema, yawafae maishani.

Ninaona wasumbuka, muda mwingi kupoteza,
Kalamu bora kushika, vizazi vingi kujuza,
Unda kwa kutiririka, uyapange kwa kuwaza,
Ninataka nena mema, yawafae maishani.

Mada nzuri angalia, epuka zenye makeke,
Hoja zako pangilia, yalo ndani yasomeke,
Ukiweza simulia, ukitaka yaandike,
Ninataka nena mema, yawafae maishani.

Alama za uandishi, muhimu kuzingatia,
Uyaweke maandishi, kwa lugha ya kuvutia,
Usiharibu mapishi, chumvi kuizidishia,
Ninataka nena mema, yawafae maishani.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 63 07/03/2022 16:50

Uzoefu zingatia, hadhira vema kujua,
Usije pata hatia, sheria kuzipindua,
Misemo kuitumia, lugha izidi kukua,
Ninataka nena mema, yawafae maishani.

Kiendeleze kipaji, kikufae maishani,
Kikupatie ulaji, kipato kikusheheni,
Zingatia upangaji, matukio andikoni,
Ninataka nena mema, yawafae maishani.

## Maswali

1. Andika kichwa cha shairi ulilolisoma.
2. Kutokana na shairi ulilolisoma, eleza maana ya utungaji.
3. Bainisha mambo manne ya kuzingatia katika utungaji.
4. Fafanua umuhimu wa utungaji kwa kuzingatia shairi ulilolisoma.
5. Eleza mambo ya msingi yanayoelezwa katika ubeti wa mwisho wa shairi.
6. Kwa nini ni muhimu kwa mtunzi kuijua vema hadhira anayoitungia?

**Zingatia**

Mtunzi huweza kuibua mawazo na kuyapanga katika mtiririko wenye mantiki. Kitendo hicho hujulikana kama utungaji. Utungaji unaweza kufanyika kwa kuandika au kwa kuzungumza. Utungaji wa kazi za fasihi huzingatia vipengele vya fani na maudhui. Fani ni ufundi anaoutumia mtunzi kuwasilisha maudhui kwa hadhira. Maudhui ni mambo yanayoelezwa katika kazi ya fasihi. Utungaji una taratibu muhimu ambazo mtunzi anapaswa kuzizingatia. Kwanza, mtunzi anapaswa kulielewa vizuri jambo analolitungia ili aweze kuiumba kazi yake kwa ustadi. Pili, anapaswa kuwa mbunifu katika kusawiri maudhui ili yaweze kuakisi jamii anayoiandikia. Tatu, mtunzi hana budi kuwasilisha mawazo kwa ufundi utakaoleta mvuto kwa hadhira. Nne, azingatie mpangilio mzuri wa mawazo kutoka mwanzo hadi mwisho wa utungo. Tano, awe na msamiati wa kutosha ili kuweza kufikisha ujumbe uliokusudiwa kwa jamii. Sita, azingatie matumizi mazuri ya alama za uakifishaji ili maana anayoilenga katika kazi yake ieleweke vizuri. Saba, anapaswa kutumia lugha kulingana na aina ya utungo.

Utungaji wa kila kipera unapaswa kuzingatia taratibu za kipera husika. Kwa mfano, utungaji wa tamthiliya huzingatia utaratibu tofauti na ule wa utungaji wa mashairi. Utungaji wa kazi mbalimbali za fasihi humwezesha mtunzi kuwa mbunifu, na kujenga uwezo wa kufikiri kitunduizi. Aidha, humwezesha kupanga mawazo kwa mtiririko wenye mantiki. Vilevile, kutokana na mambo anayoyatunga, mtunzi ataweza kuelimisha, kuburudisha, kukosoa, na kuikomboa jamii.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 64 07/03/2022 16:50

## Kutunga mashairi ya kimapokeo

### Kazi ya 4.2

**Soma shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata**.

Daima mtasimama, watetezi wenye nia,
Kamwe msije kukwama, bidhaa kutuzalia,
Kuona zenu neema, fursa kujipatia,
Mwafaa kuitwa mama, walezi wa Tanzania.

Mnazo nyingi tuhuma, walaji huwalilia,
Wanawanyima adhama, kasoro kuwatupia,
Ila nyinyi ndo alama, kadhia mwavumilia,
Mwafaa kuitwa mama, walezi wa Tanzania.

Msichukie lawama, hata wakiwafungia,
Wala msishike tama, ukiwa kujisikia,
Udhaifu kutazama, pale mloangukia,
Mwafaa kuitwa mama, walezi wa Tanzania.

Tambarare na milima, mabonde kujivukia,
Msikubali kuzama, uchumi utaumia,
Mzidi ishi daima, jamii kuhudumia,
Mwafaa kuitwa mama, walezi wa Tanzania.

Dhahabu moto kuchoma, ndo kwake kujing'aria,
Yavutia kutazama, kito wakigombania,
Ubora si lelemama, juhudi kushadidia,
Mwafaa kuitwa mama, walezi wa Tanzania.

Acheni ndoto kuzima, makusudi kusudia,
Nyinyi tumaini jema, makumi hadi mamia,
Kamwe msije tuzima, kaya zetu kutitia,
Mwafaa kuitwa mama, walezi wa Tanzania.

Kweli msije kukoma, kusudi kusimamia,
Ajira kwetu rehema, lengo letu kufikia,
Sisi na wenye kusoma, ulaji mwatupatia,
Mwafaa kuitwa mama, walezi wa Tanzania.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 65 07/03/2022 16:50

Mtatetewa daima, kamwe kutodidimia,
Zitakemewa dhuluma, ubora kupigania,
Ili msije kuhama, kwingine mkahamia,
Mwafaa kuitwa mama, walezi wa Tanzania.

Nyanja zingine zavuma, migongo yenu ni njia,
Mwatatua ulitima, wa taifa na raia,
Uchumi mnaufuma, tena pasipodhania,
Mwafaa kuitwa mama, walezi wa Tanzania.

Daraja duni kuhama, la juu tunahamia,
Mapinduzi ndo kiama, dhati hii ng'ang'ania,
Shime yetu taadhima, wajibu kutimizia,
Mwafaa kuitwa mama, walezi wa Tanzania.

Kileleni nasimama, mengi nimewaambia,
Nawaomba himahima, makini kuyawekea,
Mzuie na hujuma, nchi isije kuvia,
Mwafaa kuitwa mama, walezi wa Tanzania.

## Maswali

1. Pendekeza kichwa cha shairi ulilolisoma.
2. Bainisha lengo la mtunzi wa shairi hilo.
3. Fafanua sifa bainifu nne za shairi ukirejelea shairi ulilolisoma.
4. Eleza lugha iliyotumika katika shairi ulilolisoma.
5. Mtunzi ana maana gani anaposema "Mzuie na hujuma, nchi isije kuvia."
6. Eleza maana za maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika shairi ulilolisoma:
   (a) tuhuma
   (b) adhama
   (c) kito
   (d) nyanja
   (e) utilima
   (f) kiama
   (g) taadhima
   (h) kadhia
7. Bainisha kituo cha shairi ulilolisoma.
8. Onesha kina cha kati na cha mwisho katika ubeti wa kwanza.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 66 07/03/2022 16:50

**Zingatia**

Utungaji wa mashairi hutumia mpangilio maalumu wa maneno. Mpangilio huo huwa na ruwaza mahususi ya silabi, lugha ya mkato, picha, na tamathali za semi. Kuna aina mbili za mashairi, ambazo ni mashairi ya kimapokeo na mashairi ya kisasa. Mashairi ya kimapokeo hufuata kanuni za urari wa vina na mizani ilhali mashairi ya kisasa hayazingatii urari wa vina na mizani.

## Kazi ya 4.3

(a) Kusanya mashairi matano ya kimapokeo kutoka katika vitabu na magazeti.
(b) Chunguza mashairi hayo, kisha bainisha kanuni zilizotumika katika kuyatunga.
(c) Je, beti za kila shairi ulilolisoma zina mishororo mingapi?

**Zingatia**

Mtunzi wa shairi hawezi kuanza kutunga kabla ya kupata wazo la kutungia. Vilevile, anapaswa kuwa na msamiati wa kutosha. Aidha, anapaswa kuteua mbinu za kisanaa atakazozitumia katika shairi lake ili liwe na mvuto. Mtunzi wa mashairi ya kimapokeo anapaswa kuzingatia mpangilio maalumu wa maneno, urari wa vina na mizani, mishororo, pamoja na kituo. Pia, anapaswa kuzingatia muwala, utoshelevu, beti, matumizi ya lugha ya picha, pamoja na tamathali za semi. Shairi halipaswi kuwa na maneno mengi ya kurudiarudia ili kuepuka kupoteza mvuto wake. Kadhalika, mtunzi anapaswa kuijua hadhira anayoitungia pamoja na muktadha unaohusika.

## Kazi ya 4.4

(a) Kwa kuzingatia vipengele mahususi vya shairi la kimapokeo, tunga shairi lenye beti tano kuhusu utunzaji wa mazingira.
(b) Badilishana na mwanafunzi mwenzako shairi ulilolitunga, kisha chunguza na ubainishe vipengele vya mashairi ya kimapokeo vilivyozingatiwa.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 67 07/03/2022 16:50

**Zingatia**

Kuna taratibu maalumu zinazotakiwa kuzingatiwa katika kutunga mashairi ya kimapokeo. Miongoni mwa taratibu hizo ni mpangilio wa beti. Beti za shairi la kimapokeo hutakiwa kupangwa vizuri kwa namna ambayo vipande vyake vyote vinadhihirika bayana. Aidha, kila ubeti hutakiwa kujitosheleza kimaana. Vilevile, mtunzi hutakiwa kuzingatia matumizi sahihi ya herufi kubwa na ndogo pamoja na alama za uakifishaji. Alama za uakifishaji husaidia kuwasilisha maana iliyokusudiwa. Alama hizo ni kama vile mkato, kiulizo, mshangao, na nukta. Mbali na kufanya kazi ya kujenga maana, alama hizi pia hufanya kazi ya kujenga muundo wa kazi husika ya ushairi. Kwa mfano, alama ya mkato hutumika kutenganisha vipande vya mishororo ya mashairi. Nukta hutumika kuhitimisha ubeti.

## Kazi ya 4.5

**Chunguza shairi lifuatalo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Mwongo mie simtaki simtaki nakataa
Mwongo si wangu rafiki milele nitamwambia
Mwongo anitia chuki ananipa na kichaa
Mwongo ni mtu mbaya ni nani anamtaka
Mwongo katu hasifiki aibu anajitia
Mwongo na hakubaliki kwetu na kwa Mungu pia
Mwongo amwudhi Maliki yaso kweli kuongea
Mwongo ni mtu mbaya ni nani anamtaka

**Chanzo:** Komba, S.M (1976:40) na kuboreshwa na TET (2022)

## Maswali

1. Kwa kuzingatia taratibu za utunzi wa mashairi ya kimapokeo, onesha ukwapi na utao katika mshororo wa kwanza wa kazi ya 4.5.
2. Bainisha makosa matatu yanayojidhihirisha katika shairi ulilolisoma.
3. Andika upya shairi ulilolisoma kwa kuzingatia kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo.
4. Matumizi ya takriri katika shairi ulilolisoma yana umuhimu gani?
5. Eleza sifa mbili zinazotofautisha shairi la kimapokeo na la kisasa.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 68 07/03/2022 16:50

## Zoezi la marudio

1. Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi:
   (i) Ipi si sifa ya utungaji bora wa kazi za fasihi kati ya hizi zifuatazo?
      (a) Kuielewa jamii unayoiandikia
      (b) Kuzingatia vipengele vya fani na maudhui
      (c) Kuzingatia mambo yaliyo nje ya jamii
      (d) Kuelewa vizuri mada unayoiandikia
      (e) Kuzingatia matumizi mazuri ya alama za uakifishaji

   (ii) Kipi kati ya vipengele vifuatavyo hakihusiani na kanuni za utunzi wa mashairi?
      (a) Uakifishaji
      (b) Mpangilio wa mawazo katika beti
      (c) Mpangilio wa aya
      (d) Mpangilio wa vipande
      (e) Matumizi sahihi ya herufi kubwa

   (iii) Jumla ya silabi zinazounda mshororo huitwaje?
      (a) Vina
      (b) Bahari
      (c) Mizani
      (d) Kituo
      (e) Muwala

   (iv) Mstari unaorudiwarudiwa katika kila ubeti wa shairi kwa lengo la kusisitiza jambo huitwaje?
      (a) Kituo kimalizio
      (b) Utoshelevu
      (c) Muwala
      (d) Kituo bahari
      (e) Mshororo

   (v) Mashairi ya Kiswahili yamegawanyika katika makundi makuu mawili ambayo ni ...............
      (a) mashairi ya kimapokeo na masivina
      (b) mashairi ya kisasa na ngonjera
      (c) mashairi ya kimapokeo na ya kizamani
      (d) mashairi ya kimapokeo na ngonjera
      (e) mashairi ya masivina na mashairi ya kisasa

2. Oanisha maelezo yaliyopo katika Orodha **A** na dhana zilizopo katika Orodha **B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Mtiririko mzuri wa mawazo kutoka ubeti mmoja hadi mwingine ambao hukamilisha maana ya shairi zima | A. mizani |
| | B. ubeti |
| | C. vina |
| (ii) Hali ya ubeti kujikamilisha kimaana pasipo kutegemea kukamilishwa na ubeti mwingine | D. kipande |
| | E. muwala |
| (iii) Mstari wa mwisho wa ubeti katika shairi | F. kituo |
| (iv) Sehemu ya mshororo katika ubeti wa shairi ambayo hutenganishwa kwa alama ya mkato | G. utoshelevu |
| (v) Huundwa na mshororo mmoja au zaidi | |

3. Fafanua umuhimu wa kuzingatia alama za uakifishaji katika utungaji wa shairi la kimapokeo.
4. Kwa nini ni muhimu kuchagua mada mahususi wakati wa kutunga shairi la kimapokeo?
5. Bainisha kanuni za utungaji wa mashairi ya kimapokeo ambazo mwandishi anapaswa kuzizingatia.
6. Kuna umuhimu gani kuzingatia kanuni za utunzi wa mashairi ya kimapokeo?
7. Nini tofauti baina ya kituo na kituo bahari.
8. Eleza tofauti iliyopo kati ya vina na mizani kwenye shairi.
9. Tunga shairi la kimapokeo lenye beti tano kuhusu Mlima Kilimanjaro.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 70 07/03/2022 16:50

# Sura ya Tano


## Uandishi

**Utangulizi**

*Watu huweza kupata taarifa, maarifa na stadi katika maisha ya kila siku kwa njia mbalimbali. Miongoni mwa njia hizo ni uandishi. Katika sura hii, utajifunza uandishi wa insha, hotuba, risala, na kumbukumbu za mikutano. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuandika insha, hotuba, risala, na kumbukumbu za mikutano kwa kuzingatia taratibu za uandishi. Vilevile, umahiri huo utakuwezesha kukuza stadi za kusoma na kuandika.*

### Dhana ya uandishi

#### Kazi ya 5.1



**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata**.

Ilikuwa siku ya Jumanne. Niliamka mapema ili niwahi shuleni kwa ajili ya kwenda kwenye ziara ya kimasomo. Mwalimu wetu wa somo la Kiswahili anayeitwa Makupa alikuwa kiongozi wa ziara hiyo. Tulikuwa tunakwenda kutembelea maktaba ya mkoa iliyokuwa karibu na shule yetu ili kusoma vitabu, magazeti, na maandiko mengine. Lengo la ziara hiyo lilikuwa kupata maarifa kuhusu uandishi wa insha, hotuba, risala, na kumbukumbu za mikutano. Hivyo, kabla ya kuanza ziara, mwalimu alitueleza mambo muhimu ya kuzingatia wakati wa kusoma maandiko hayo. Mwalimu Makupa alituhimiza kuwa, tutakapokwenda huko, tusome zaidi maandiko ya insha, hotuba, risala, na kumbukumbu za mikutano. Kila mwanafunzi alitakiwa kuandika tini za mambo muhimu atakayoyasoma katika maandiko hayo. Hivyo, kwenye ziara, kila mwanafunzi alizingatia maelekezo ya mwalimu.

Siku iliyofuata, tulikuwa na kipindi cha somo la Kiswahili. Mwalimu Makupa aliingia darasani na kuanza kufundisha mada ya uandishi. Alianza kwa kuuliza, "Nini maana ya uandishi?" Kwa kuwa tulisoma maandiko mbalimbali tulipokwenda maktabani, kila mtu darasani alinyoosha mkono. Mwalimu alichagua baadhi ya wanafunzi wa kike na wa kiume kujibu swali hilo. Mmoja alielezea kiasi, na mwingine alifafanua zaidi, kisha mwalimu aliwapongeza kwa kujibu vyema. Baada ya maelezo hayo, Mwalimu Makupa alijumuisha mawazo hayo na kufafanua kuwa uandishi ni njia ya mawasiliano inayohusisha kuibua mawazo na kuyawasilisha kwa maandishi.

Mwalimu alitugawa katika vikundi vinane vyenye wanafunzi watanowatano na kutugawia kazi za vikundi. Kikundi cha kwanza kilipewa kazi ya kubainisha mambo ya kuzingatia katika uandishi kwa ujumla. Kikundi cha pili kilipewa kazi ya kubainisha mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha. Kikundi cha tatu na cha nne vilipewa kazi ya kubainisha muundo wa hotuba na mambo ya kuzingatia katika uandishi wa hotuba. Kikundi cha tano na cha sita vilipewa kazi ya kutofautisha hotuba na risala. Kikundi cha saba na cha nane vilipewa kazi ya kujadili mambo ya kuzingatia katika kuandika kumbukumbu za mikutano. Baada ya majadiliano, kila kikundi kiliwasilisha kazi yake. Uwasilishaji huo uliambatana na maswali na majibu, ambapo sote tulishiriki kikamilifu. Mwalimu Makupa alituambia kuwa, katika vipindi vinavyofuata, tutaandika insha, hotuba, risala, na kumbukumbu za mikutano.

## Maswali

1. Kama wewe ungekuwa miongoni mwa wanafunzi wa Mwalimu Makupa, ungeelezaje maana ya uandishi?
2. Kujifunza mada ya uandishi kuna umuhimu gani?
3. Kwa nini Mwalimu Makupa aliwahimiza wanafunzi wasome maandiko kama insha, hotuba, na kumbukumbu za mikutano?
4. Unadhani ni kwanini Mwalimu Makupa aliwahimiza wanafunzi kuandika tini?
5. Umejifunza nini kutokana na habari uliyoisoma?

**Zingatia**

Mawazo mbalimbali huweza kuwasilishwa kwa njia ya maandishi. Mchakato wa uwasilishaji wa mawazo kwa njia ya maandishi hujulikana kama uandishi. Uandishi ni stadi muhimu katika maisha yetu ya kila siku kwani huchochea stadi za kufikiri na kupanga mawazo kimantiki. Pia, husaidia kukuza uwezo wa kujieleza na hufanikisha mawasiliano. Mtu akiwa mahiri katika uandishi, anaweza kupata mafanikio mbalimbali katika maisha yake na kuinufaisha jamii kwa ujumla. Kwa mfano, Shaaban Robert na Mathias Mnyampala wamekuwa maarufu kwa sababu ya uandishi wao wa vitabu vya fasihi.

Kuna mambo ya msingi ya kuzingatia katika uandishi. Kwanza, mwandishi anatakiwa kujua jambo analotaka kuliandikia; endapo halifahamu vyema, anapaswa kulifanyia utafiti. Pili, mwandishi anapaswa kuifahamu hadhira anayoiandikia ili aweze kuchagua maudhui na lugha anayopaswa kutumia kulingana na kiwango cha uelewa wao. Tatu, mwandishi anapaswa kuzingatia taratibu za uandishi, ambazo zinajumuisha kufuata muundo wa aina ya andiko linalolengwa, pamoja na kutumia kwa usahihi alama za uakifishaji na kuzingatia sarufi ya lugha inayohusika. Aidha, taratibu hizo zinahusisha kuweka kila wazo katika aya moja na kulikuza kwa utoshelevu hadi linapokamilika.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 72 07/03/2022 16:50

## Kuandika insha

### Kazi ya 5.2

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Hapo zamani, katika Kijiji cha Manajuka, alikuwapo mzee mmoja aliyeitwa Kanju. Mzee Kanju alikuwa maarufu sana kutokana na ucheshi na uhodari wake wa kufanya kazi. Katika himaya yake, alifuga mbuzi, kondoo, ng'ombe, na kuku. Mzee Kanju alikuwa na watoto wawili, Merija na Sirimo. Aliwapenda sana watoto wake kutokana na juhudi walizozionesha katika masomo. Aliwasihi wazingatie elimu kwani aliamini kuwa elimu ni ufunguo wa maisha.

Siku moja, Mzee Kanju alimshtukiza Merija na kumuuliza alichojifunza shuleni. Merija alimwambia kuwa alijifunza maana ya insha, aina zake, umuhimu na mambo ya kuzingatia katika uandishi wa insha. Mzee Kanju alimtaka binti yake ampe maelezo zaidi kuhusu aina za insha walizojifunza. Merija alimjibu kuwa walijifunza insha za maelezo, insha za usimulizi, na za ufafanuzi. Mzee Kanju akamuuliza tena, "Mbona ninasikia kuna insha za hoja na insha za wasifu?" Merija akamjibu, "Tulijifunza insha za hoja tulipokuwa kidato cha pili, na insha za wasifu tulijifunza tulipokuwa kidato cha kwanza." Mzee Kanju akauliza, "Unaweza kunielezea kidogo kuhusu insha hizo za hoja mlizojifunza?" Merija akamwelezea kuwa insha za hoja huandikwa ili kutoa mawazo, maoni au hoja kuhusu jambo fulani. Maelezo ya Merija yalisababisha Mzee Kanju aamini kuwa watoto wake wako makini kufuatilia wanayofundishwa na walimu, hata kama ni ya miaka iliyopita. Hivyo, aliwaahidi kuendelea kuwanunulia vitabu vya masomo mbalimbali wanayosoma shuleni. Kwa kuwa hakuwa na fedha za kutosha, aliuza ng'ombe mmoja na kuwanunulia mahitaji yote ya shule. Merija na Sirimo walifurahi sana na kumwahidi baba yao kuwa watasoma kwa bidii hadi wafike chuo kikuu.

### Maswali

1. Kwa nini Mzee Kanju alisema kuwa elimu ni ufunguo wa maisha?
2. Eleza wasifu wa Mzee Kanju.
3. Kutokana na habari uliyosoma, mwandishi amebainisha aina gani za insha?
4. Bainisha mambo ya kuzingatia wakati wa uandishi wa insha.
5. Eleza umuhimu wa kuandika insha.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 73 07/03/2022 16:50

**Zingatia**

Insha ni utungo wa maneno yenye mtiririko wa mawazo kuhusu jambo fulani. Jambo linaloelezwa au kusimuliwa katika insha huitwa mada ya insha. Utungo huu una muundo maalumu ambao hujumuisha *kichwa*, *utangulizi*, *kiini*, na *hitimisho*. Kuna aina mbalimbali za insha kutegemeana na lengo la mwandishi. Miongoni mwa aina hizo ni insha za maelezo, usimulizi, ufafanuzi, na hoja.

Unapotaka kuandika insha, unatakiwa kuzingatia mambo makuu mawili. Kwanza, ni kuchagua mada ya kuandikia. Unapaswa kuelewa mada utakayoichagua ili uweze kuielezea vizuri. Pia, mada inapaswa kuzingatia upeo na kiwango cha kueleweka kwa walengwa uliowakusudia. Pili, unatakiwa kujua maudhui unayotaka kuyafikisha kwa hadhira yako.

Utaratibu utakaokuongoza katika kuandika insha yako vizuri ni kufuata mchakato wa uandishi hatua kwa hatua. Kwanza, kusanya mawazo kuhusiana na mada uliyoichagua ili kupata hoja za msingi. Pili, chambua mawazo hayo ili kujua mawanda na mtitiriko wa insha yako. Kwa kawaida, mawazo yanayokusanywa ni mengi. Hivyo, unatakiwa kuyachuja na kuteua mawazo yanayoendana na lengo lako. Tatu, panga mawazo yako katika aya kwa mtiririko wenye mantiki, kisha anza kuandika insha yako hadi ikamilike.

Insha itasomeka na kueleweka vizuri ikiwa itazingatia ufasaha na usanifu wa lugha. Hivyo, unapaswa kuzingatia ufasaha na usanifu wa lugha. Kadhalika, unatakiwa kuzingatia matumizi sahihi ya alama za uakifishaji kama vile nukta, mkato, alama ya kuuliza, na alama za kufunga na kufungua usemi, pamoja na herufi kubwa na ndogo.

Vilevile, unapaswa kuandika insha kwa mpangilio mzuri wa aya. Kila wazo liwe na aya inayojitegemea. Usichanganye mawazo zaidi ya moja katika aya moja. Pia, zingatia urefu wa sentensi. Sentensi zako zisiwe ndefu sana; ziwe fupifupi na zenye kueleweka. Aidha, unapaswa kuandika hitimisho la insha kwa kuzingatia wazo kuu.

Uandishi wa insha humwezesha mwandishi kukuza uwezo wa kujieleza, kubuni, na kutafiti masuala mbalimbali. Uandishi pia ni njia ya mawasiliano ambayo humwezesha mtu kuwasilisha mawazo yake kwa malengo ya kuelimisha, kutaarifu, kuhoji, kushawishi, na kuunga mkono jambo fulani.

## Zoezi la 5.1

1. Fafanua muundo wa insha.
2. Taja aina za insha unazozifahamu na ueleze kila moja imo katika kundi gani kati ya makundi unayoyafahamu.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 74 07/03/2022 16:50

## Insha za maelezo

### Kazi ya 5.3

**Soma insha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Shule yetu inaitwa Ngoru. Shule hii imezungukwa na miti ya mijohoro na bustani za maua. Upande wa mbele wa shule una bustani za maua ya rangi mbalimbali yanayovutia. Maua hayo yana rangi ya kijani, nyekundu, njano, na nyeupe. Upande wa nyuma wa shule yetu una vyoo vya wasichana na vya wavulana. Pia, una vyoo vya walimu ambavyo vimejengwa mbali kidogo na vyoo vya wanafunzi.

Shule ya Ngoru ina vyumba kumi na vinne vya madarasa na chumba kimoja cha maktaba. Kadhalika, kuna jengo la ofisi za walimu. Majengo haya yamezungukwa na bustani za maua. Chumba cha maktaba kina mlango wa grili na kwa ndani kuna mlango wa mbao. Vilevile, chumba hicho kina madirisha makubwa yenye kuingiza hewa ya kutosha. Ukiingia maktabani, kuna rafu zilizojaa vitabu vya aina mbalimbali. Kuna vitabu vya kiada, ziada, rejea, na vya hadithi. Vyumba vya madarasa vina milango ya mbao inayofunguka kwa nje na madirisha makubwa yanayopitisha hewa ya kutosha.

Kwenye jengo la walimu, kuna mlango wa mbao na madirisha makubwa. Ukiingia ndani, mna meza na viti vya walimu. Meza zimetandikwa vitambaa vya rangi ya hudhurungi vinavyopendezesha ofisi hiyo. Aidha, kuna ofisi ya mkuu wa shule ambayo ina mlango wa grili na wa mbao. Ndani ya ofisi hiyo, mna meza moja iliyotandikwa vitambaa vyeupe vinavyofanya ofisi hiyo ionekane nadhifu. Pia, mna viti vitatu: viti viwili ni kwa ajili ya wageni, na kimoja ni cha mkuu wa shule. Aidha, pembeni ya viti vya wageni kuna makochi. Ukutani zimebandikwa chati zenye taarifa mbalimbali. Taarifa hizo ni pamoja na ratiba ya masomo, mchanganuo wa nyadhifa za walimu, mgawanyo wa masomo kwa walimu pamoja na idadi ya vipindi kwa kila darasa.

Katika vyoo vya shule yetu, kuna matundu ya kutosha kukidhi mahitaji ya wanafunzi. Ndani ya vyoo, kuna sakafu na kuta zenye marumaru na mabomba ya maji ya kunawia mikono.

Wageni wanaokuja kuitembelea shule yetu huisifu kwa namna ilivyojengwa na kupambwa kwa miti na bustani za maua.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 75 07/03/2022 16:50

## Maswali

1. Pendekeza kichwa cha insha uliyoisoma.
2. Insha uliyoisoma ni ya aina gani kati ya aina za insha ulizojifunza? Tetea jibu lako.
3. Fafanua muundo wa insha uliyoisoma.
4. Eleza wazo kuu lililomo katika kila aya ya insha uliyoisoma.
5. Bainisha sifa za insha uliyoisoma.

**Zingatia**

Insha za maelezo hutoa maelezo kuhusu mtu, vitu, au mahali. Moja ya sifa za insha hizi ni kumjengea msomaji taswira au picha kutokana na uelezaji anaoutumia mwandishi. Taswira hizo huhusisha milango yote ya fahamu. Kadhalika, insha za maelezo hutumia lugha ya kawaida inayoeleweka kirahisi. Insha za maelezo pia huwa wazi kwa sababu lengo lake ni kuelezea jambo fulani kwa uwazi.

Uandishi wa insha hizo humtaka mwandishi awe na jambo la kuelezea na ajue jinsi ya kulielezea na kulisisitiza katika insha yake. Namna mojawapo nzuri ya kulielezea jambo ni kufanya uteuzi mzuri wa maneno ili kuifanya insha iwe na mvuto. Kadhalika, mpangilio na mtiririko wa insha za maelezo unapaswa kuwa na mantiki.

## Zoezi la 5.2

1. "Insha za maelezo zinaweza kuwa za aina mbalimbali, ilimradi zizingatie taratibu za uandishi wa insha na sifa zinazohusika na insha hizo." Fafanua usemi huu.
2. Eleza faida za kuandika insha za maelezo.

## Kazi ya 5.4

(a) Chagua mada uipendayo, kisha andika insha ya maelezo isiyopungua maneno 250.

(b) Badilishaneni insha zenu, kila mmoja asome insha ya mwenzake, na aitathmini kama imezingatia utaratibu wa uandishi wa insha za maelezo. Kila mmoja awasilishe tathmini yake kwa ajili ya majadiliano.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 76 07/03/2022 16:50

## Insha za usimulizi

### Kazi ya 5.5

**Soma insha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Dengu, Bwaki, Naki, na Zufa walikuwa wanafunzi wa Shule ya Sekondari Msicheze. Dengu na Zaki walikuwa wanasoma kidato cha kwanza, na Bwaki na Zufa kidato cha pili. Wanafunzi hawa walioishi kijiji kimoja walikuwa marafiki. Walipoanza shule, walikuwa na maendeleo mazuri, na walikuwa wanafanya vizuri katika masomo yao.

Urafiki wao uliimarika zaidi kutokana na kushiriki kwao katika michezo. Marafiki hawa wote walipenda sana kucheza mpira wa miguu. Kila siku jioni, baada ya muda wa masomo, wanafunzi waliporuhusiwa kwenda nyumbani, wao walibaki kufanya mazoezi ya mpira wa miguu pamoja na wanafunzi wengine.

Mambo yalianza kuwaharibikia marafiki hao pale Dengu na Zaki walipoingia kidato cha pili, na Bwaki na Zufa kidato cha tatu. Walianza tabia ya utoro ambayo iliwasababishia kutofanya vizuri katika masomo. Mwalimu wa nidhamu aliwaita na kuwaonya kuhusu tabia hiyo. Aliwaeleza madhara ya utoro na waliahidi kujirekebisha. Waliamua kubadilika kwani waliona kuwa, wakiendelea na utoro, watashindwa kufaulu mitihani ya kidato cha pili.

Bwaki na Zufa waliona wana muda wa kutosha kwani kulikuwa na mwaka mmoja zaidi kabla ya kuingia darasa la mitihani. Hivyo, waliendelea na tabia ya kutoroka na kwenda kuungana na vikundi vya vijana wa mtaani kwao waliokuwa wanacheza kamari. Punde si punde, mwaka wa tatu ulikwisha na wakaingia kidato cha nne. Tabia ya utoro iliendelea na walishindwa kuwa makini katika masomo kwani *mshika mawili moja humponyoka*. Waliona masomo ni magumu. Wakaanza kukata tamaa na masomo yakawashinda.

Wakati wa kuanza mitihani ya kidato cha nne ulipowadia, walifanya mitihani hiyo bila kuwa na stadi na maarifa ya kutosha. Hivyo, walishindwa kujibu vizuri maswali. Matokeo yalipotoka, walipata daraja la mwisho. Wenzao wote walifaulu mitihani vizuri. Matokeo hayo yaliwafanya wajutie tabia zao. Waliona aibu walipokutana na wanafunzi wenzao pamoja na marafiki zao, Dengu na Zaki. Hilo lilikuwa fundisho kwa wanafunzi wote waliokuwa watoro shuleni hapo.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 77 07/03/2022 16:50

## Maswali

1. Pendekeza kichwa cha insha uliyoisoma.
2. Insha hiyo ni ya aina gani? Eleza sababu za jibu lako.
3. Kwa kutoa mifano, fafanua muundo wa insha uliyoisoma.
4. Bainisha mawazo makuu ya kila aya katika insha uliyoisoma.
5. Eleza maudhui yaliyomo katika insha uliyoisoma ukiyahusisha na hali halisi katika maisha.

**Zingatia**

Insha za usimulizi zinazingatia mfuatano wa matukio kulingana na utokeaji wake kiwakati. Zinaweza kuhusu historia ya maisha ya mtu mmoja, kundi la watu, au mahali. Insha za aina hii hubainisha mandhari, mtiririko wa matukio, na wahusika. Mwandishi wa insha ya usimulizi anapaswa kuipanga vizuri insha yake akizingatia kisa anachotaka kukisimulia, mtiririko wa matukio, mandhari, wahusika, na matumizi sahihi ya lugha.

## Kazi ya 5.6

Soma insha mbalimbali za usimulizi na ufafanuzi, kisha chunguza miundo yake. Linganisha na linganua insha hizo.

## Zoezi la 5.3

1. "Insha za usimulizi zinaweza kuwa za aina mbalimbali, ilimradi zizingatie mambo muhimu ya uandishi wa insha na sifa zinazohusika." Fafanua usemi huu.
2. Eleza faida za kuandika insha za usimulizi.

## Kazi ya 5.7

(a) Andika insha ya usimulizi yenye maneno yasiyopungua 250 kuhusu mada uipendayo. Iwasilishe darasani kwa ajili ya majadiliano.

(b) Badilishana na mwenzako. Kila mmoja asome na atathmini insha ya mwenzake kama imeandikwa kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa insha za usimulizi. Kila mmoja awasilishe tathmini yake kwa ajili ya majadiliano.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 78 07/03/2022 16:50

## Insha za ufafanuzi

### Kazi ya 5.8

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Donga ni mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Kisanji. Shule hiyo iko katika Kijiji cha Kunke. Donga ni mwanafunzi mwenye bidii katika masomo yake. Siku zote, Donga hupenda kufanya vitu ambavyo anaona vinafaa katika jamii yake. Licha ya maarifa na juhudi alizonazo katika masomo, Donga pia ni mtunzaji mzuri wa mazingira katika kijiji chake. Siku moja alipokuwa akitoka shuleni, aliona moto mkubwa ukiteketeza hifadhi ya msitu.



Jambo hilo halikumpendeza Donga. Aliamua kuandika insha inayohusu uharibifu wa mazingira ambayo atawasomea wanakijiji siku ya mkutano. Alipomweleza mwenyekiti wa kijiji, wazo lake lilikubaliwa. Insha hiyo ilikuwa kama ifuatavyo:

*Mazingira ni jumla ya vitu vyote vinavyomzunguka mwanadamu. Vitu hivyo ni kama mimea, milima, na mabonde. Mazingira yana umuhimu mkubwa sana katika jamii. Mathalani, mimea hutupatia hewa safi, na huwezesha mvua kunyesha.*

*Kuna mambo mengi ya kufanya ili kuhakikisha mazingira yanakuwa safi na bora katika jamii. Kwa mfano, tunaweza kuotesha miti katika maeneo ambayo hayana miti, kuotesha nyasi, na kuepuka uharibifu wa vyanzo vya maji. Kufanya hivyo kutasaidia kuhifadhi unyevunyevu unaowezesha mimea kuota na kustawi kwenye ardhi. Hayo ni baadhi ya mambo ambayo kila mtu akiyafanya mazingira yatakuwa salama na tutapunguza changamoto za kimazingira kwa kiasi kikubwa.*

*Mambo yanayoweza kusababisha uharibifu wa mazingira ni uchomaji na ukataji ovyo wa misitu, uharibifu wa vyanzo vya maji, na kutupa taka ovyo. Kwa kufanya hivyo, jamii, pamoja na viumbe wengine kama wanyama, wadudu, na mimea hupata madhara. Mifano ya madhara hayo ni ukame, njaa, mafuriko, magonjwa, na upotevu wa viumbe hai. Kutokana na madhara hayo, jamii haina budi kupiga vita uharibifu wa mazingira. Watu watakaoharibu mazingira wachukuliwe hatua kali na wapewe adhabu stahiki ili iwe fundisho kwa wengine. Hivyo, ni jukumu la kila mwanadamu kuyatunza mazingira ili kuepusha madhara yatokanayo na uharibifu wa mazingira.*

Ilipofika siku ya mkutano, mwenyekiti aliwaeleza wanakijiji kuwa kuna kijana anataka kuwaambia jambo la msingi. Hivyo, aliomba wamruhusu ili wasikilize alichowaandalia. Wananchi waliridhia, Donga akapewa nafasi ya kusoma insha yake kuhusu athari za uharibifu wa mazingira. Donga aliisoma insha yake kwa ufasaha, na, baada ya kumaliza, wanakijiji walimpigia makofi na kumpongeza kwa elimu nzuri aliyoitoa. Mwenyekiti alimshukuru Donga kwa insha yake nzuri yenye kuelimisha jamii. Vilevile, alimpongeza kwa kujiamini na kuweza kuandika mambo halisi yaliyopo katika kijiji chao. Baada ya hapo, mwenyekiti aliwahimiza wanakijiji kuzingatia elimu waliyopewa na kuwatangazia kuwa watakaoharibu mazingira, watachukuliwa hatua kali. Mwenyekiti alimalizia kwa kusema, "Tukiyatunza mazingira, nayo yatatutunza."

## Maswali

1. Insha aliyoiandika Donga ni ya aina gani?
2. Kwa kuzingatia muundo wa insha, bainisha kipengele kinachokosekana katika insha ya Donga. Eleza athari za kukosekana kwa kipengele hicho.
3. Fafanua mawazo makuu aliyoyazingatia Donga katika insha yake.
4. Donga alizingatiaje kiwango cha uelewa wa hadhira yake?
5. Mwenyekiti alikuwa na maana gani aliposema, "Mazingira tukiyatunza, nayo yatatutunza?"



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 80 07/03/2022 16:50

**Zingatia**

Insha za ufafanuzi huelezea jambo kwa kina ili liweze kueleweka kwa wasomaji au hadhira. Mwandishi anaweza kulinganisha na kulinganua mambo anayoyaeleza. Kwa mfano, katika insha yake, Donga amelinganisha mazingira yanayotunzwa na yasiyotunzwa kwa kueleza athari za uharibifu wa mazingira. Insha za ufafanuzi hujikita katika kufafanua ukweli wa jambo. Kwa mfano, unaweza kuandika insha ya kufafanua mfumo wa mmeng'enyo wa chakula au mambo mengine ya kisayansi.

Muundo wa insha ya ufafanuzi ni sawa na muundo wa insha zingine, yaani unajumuisha *kichwa*, *utangulizi*, *kiini*, na *hitimisho*. Ukiandika insha hizi mara kwa mara, utajenga uwezo wa kufafanua mambo kwa kina. Vilevile, utakuza uwezo wako wa kusoma maandiko mbalimbali na kuyatumia maarifa unayoyapata kufafanua mambo kwa kueleza ukweli wake.

## Zoezi la 5.4

1. Fafanua muundo wa insha ya ufafanuzi.
2. Eleza tofauti kati ya insha za usimulizi na insha za ufafanuzi.

## Kazi ya 5.9

(a) Andika insha ya ufafanuzi isiyopungua maneno 250 kwa kutumia moja kati ya mada zifuatazo:
   (i) Ugonjwa wa UKIMWI
   (ii) Uzalendo
   (iii) Umuhimu wa kilimo
(b) Bainisha mambo uliyoyazingatia wakati wa kuandika insha yako.

# Kuandika hotuba

## Kazi ya 5.10

**Soma hotuba ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**HOTUBA YA MKUU WA MKOA WA ZAMOYONI KWA WANANCHI WA KIJIJI CHA KUMEKUCHA ILIYOTOLEWA TAREHE 10/10/2021**

Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya,

Mheshimiwa Mkurugenzi,

Mheshimiwa Diwani,

Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kijiji,

Ndugu waandishi wa habari,

Ndugu wananchi wa Kumekucha,

Mabibi na mabwana,

Itifaki imezingatiwa.

Habarini za leo?

Ndugu wananchi,

Ninatumia fursa hii kuwashukuru kwa kujitokeza kwa wingi kuhudhuria mkutano huu muhimu. Ninatambua kuwa mna majukumu mengi ya kufanya, lakini mmeyasitisha na kuja kunisikiliza. Asanteni sana!

Ndugu wananchi,

Ninatambua kuwa asilimia kubwa ya wananchi wa Kijiji cha Kumekucha ni wakulima na wachache ni wafugaji. Pia, ninatambua kuwa nyinyi ni ndugu kwani mnashirikiana katika shughuli mbalimbali za kijamii. Aidha, ninatambua kwamba mnashiriki katika shughuli za maendeleo bila kujali itikadi zenu. Hongereni sana!

Ndugu wananchi,


Pamoja na umoja wenu, ninasikitika kusema kwamba kuna wachache wanaoharibu taswira ya kijiji chetu. Watu hawa hawatutakii mema. Wanataka kuvuruga amani ya kijiji chetu. Wana dhamira ya kurudisha nyuma maendeleo yetu. Kamwe, tusikubali!

Ndugu wananchi,

Nimepata taarifa kuwa kuna baadhi ya wafugaji wanavamia mashamba ya wakulima na kuingiza mifugo yao. Jambo la kusikitisha zaidi, wanawapiga wakulima hao na kuwajeruhi. Jambo hili halikubaliki hata kidogo! Vilevile, kuna baadhi ya wakulima wanaovamia maeneo ya wafugaji. Huo ni uchokozi unaosababisha uvunjifu wa amani. Suala hilo nalo halikubaliki.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 82 07/03/2022 16:50



Ndugu wananchi,

Sote tunatambua kuwa maendeleo ya taifa letu yanategemea shughuli mbalimbali za kiuchumi, zikiwamo za kilimo na ufugaji. Hivyo, wakulima na wafugaji ni watu muhimu, na kila mtu ana haki ya kuthaminiwa. Kwa hiyo, tuishi kwa amani na kwa kufuata sheria za nchi. Kuvamia eneo la mwenzako na kumjeruhi ni kosa la jinai.

Ndugu wananchi,

Ninapenda kuwajulisha kwamba serikali yetu iko makini. Tutawashughulikia wale wote wanaovuruga amani ya nchi yetu. Bahati nzuri, wale wote wanaojihusisha na vitendo vya kihalifu wanajulikana. Kwa hiyo, nimekuja hapa ili nitoe rai kwa wale wenye tabia hizo waache mara moja. Tumieni viongozi wa kijiji kutatua changamoto zenu. Tatizo lisiposhughulikiwa, lifikisheni ngazi za juu.

Ndugu wananchi,

Baada ya kuzungumza hayo, ninaomba nitumie fursa hii kuwashukuru tena kwa kunisikiliza. Ni matumaini yangu kuwa mtayazingatia maelekezo yote niliyoyatoa na mtakayopewa na viongozi wengine. Kwa kufanya hivyo, sote tutaishi kwa amani na upendo, na, hatimaye, tutapata maendeleo zaidi. Asanteni sana kwa kunisikiliza!



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 83 07/03/2022 16:50

## Maswali

1. Eleza muundo wa hotuba uliyoisoma.
2. Mwandishi ametumia njeo gani?
3. Kwa kutumia mifano, fafanua nafsi aliyoitumia mwandishi wa hotuba.
4. Mwandishi ametumia maneno gani kubainisha hoja zake katika hotuba uliyoisoma.
5. Fafanua lugha aliyoitumia mwandishi katika hotuba.
6. Eleza umuhimu wa kuandika hotuba.

**Zingatia**

Hotuba ni maelezo ambayo hutolewa na mtu mmoja kwa hadhira kwa lengo maalumu. Kwa mfano, hotuba inaweza kutolewa ili kuwashawishi na kuwahimiza watu kufanya kazi kwa bidii, kutoa taarifa fulani kwa watu kuhusiana na jambo fulani, kutoa pole, kufanya kampeni, na kuelimisha kuhusu suala fulani. Kwa kawaida, hotuba huandikwa kwa ajili ya kusomwa mbele ya hadhira.

Aina za hotuba huweza kutofautishwa kwa kuzingatia lengo la hotuba na muktadha zinamowasilishwa. Hivyo, tunaweza kupata aina mbalimbali za hotuba. Kwa mfano, kuna hotuba za mahubiri au mawaidha, za nasaha, na za mihadhara. Pia, kuna hotuba zinazohusu masuala ya kisiasa ambazo hutolewa na wanasiasa kama vile viongozi wa serikali. Vilevile, kuna hotuba za taarifa kama vile za utafiti na ripoti mbalimbali za wataalamu.

Uandishi wa hotuba huzingatia vipengele vifuatavyo: *kichwa*, *mwanzo*, *utangulizi*, *kiini,* na *hitimisho*. *Kichwa* cha hotuba huandikwa kwa ufupi kwa lengo la kuonesha aliyeiandika hotuba hiyo, walengwa wa hotuba hiyo, pamoja na tarehe ambayo hotuba hiyo itasomwa. *Mwanzo* wa hotuba hujumuisha salamu ya jumla ambayo huwa na lengo la kuchangamsha na kuamsha ari ya wasikilizaji kusikiliza kitakachozungumzwa. Kwa mfano, kama ni hotuba ya kisiasa, huanza na *Wananchi oyee*! *Vijana safiii*! *Wanawake hai hoi*! Salamu hizi huwa kichombezo na hutofautiana kutegemeana na hadhira iliyohudhuria kwenye tukio husika. Katika *utangulizi*, watu mbalimbali hutajwa. Watu hao huweza kuwa waheshimiwa na watu muhimu kulingana na vyeo na nyadhifa zao. Watu hao hutajwa kuanzia wale wa nyadhifa za juu na kumalizia na watu wasiokuwa na nyadhifa. Vilevile, shukurani hutolewa kwa hadhira, na, wakati mwingine, hudokeza kiini cha hotuba hiyo. *Kiini* hubeba lengo kuu la hotuba, ambapo mawazo hupangwa katika utaratibu maalumu ili kuwa na mtiririko wenye kuleta maana. Katika sehemu hii, mtoa hotuba hueleza ujumbe au dhamira ya hotuba yake. Baada ya kiini, hufuata *hitimisho*, ambapo mtoa hotuba hutoa shukurani kwa wasikilizaji. Pia, mtoa hotuba anaweza kuwatakia baraka wasikilizaji wake baada ya kuwashukuru.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 84 07/03/2022 16:50

## Kazi ya 5.11

Kusanya kazi mbalimbali zenye hotuba zilizorekodiwa au zilizoandikwa, kisha sikiliza au soma hotuba hizo na kuchunguza muundo wake.

(a) Andika hotuba kuhusu mada yoyote unayoipenda kwa kuzingatia taratibu za uandishi wa insha.

(b) Wasilisha hotuba uliyoiandika katika kipengele (a) mbele ya wanafunzi wenzako darasani.

**Zingatia**

Mambo kadhaa ya msingi hupaswa kuzingatiwa katika uandishi wa hotuba. Kwanza, lugha inayotumika ni lazima iwe fasaha na inayoeleweka. Pili, hotuba inapaswa kuwa katika kauli halisi, na njeo yake iwe ya wakati uliopo. Tatu, hotuba lazima iakisi hali, mawazo, na fikira zilizotulia na kupangiliwa kimantiki ili kujenga maana iliyokusudiwa. Nne, hotuba lazima ieleze ukweli wa jambo linalowasilishwa. Tano, suala la muundo wa hotuba linapaswa kuzingatiwa. Kipengele chochote kati ya hivi kikikosekana katika hotuba, kinaweza kuharibu hotuba nzima.

Wakati wa kuwasilisha hotuba, mtoa hotuba anapaswa awe na sauti inayosikika vizuri.

## Kazi ya 5.12

Ukiwa kama kiongozi wa wilaya, andaa hotuba utakayoiwasilisha kwa wananchi wa wilaya yako. Hotuba hiyo ihusu mada mojawapo kati ya hizi zifuatazo:

(a) Athari za ajira kwa watoto

(b) Sensa ya watu na makazi

(c) Madhara ya rushwa katika jamii

# Kuandika risala

## Kazi ya 5.13

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata**.

Shule ya Sekondari Kwedihoma iliyopo katika Kijiji cha Kitalu ina miaka minne tangu ilipoanzishwa. Shule hii ilianzishwa kwa nguvu za wananchi. Shule hiyo imekuwa ikikabiliwa na uhaba wa vyumba vya madarasa, madawati, chumba cha maabara, na maktaba.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 85 07/03/2022 16:50

Siku moja, katika kikao cha Bodi ya Shule, uongozi ulijadili namna ya kutatua changamoto hizo. Mwenyekiti wa Bodi alitoa wazo kuwa waitishe harambee ili wananchi wachangie mawazo kuhusu maendeleo ya shule yao. Wajumbe wote waliafiki wazo lake na kupendekeza siku ya mkutano wa wananchi wote. Pia, walikubaliana kuwaalika mheshimiwa mbunge na mheshimiwa diwani, ambapo mheshimiwa mbunge alipendekezwa kuwa mgeni rasmi. Vilevile, walikubaliana kuandaa risala itakayosomwa mbele ya mgeni rasmi. Wajumbe wawili waliteuliwa kuandaa risala na barua za mialiko kwa mgeni rasmi na wageni waalikwa. Aidha, walimchagua kijana hodari wa kupiga mbiu kuzunguka kijiji kizima ili kutangaza tarehe ya mkutano, muda na mahali mkutano utakapofanyikia.

Siku ya mkutano ilipowadia, wanakijiji wengi walihudhuria kutokana na hamasa na maneno ya bashasha waliyoyapata kutoka kwa mpigambiu. Mgeni rasmi alipowasili, Mwenyekiti wa Bodi alimkaribisha pamoja na wageni waalikwa, na wananchi waliohudhuria. Muda wa kusoma risala ulipowadia, Mwenyekiti wa Bodi alisoma risala hiyo ambayo iliandikwa hivi:

***RISALA YA WANANCHI WA KIJIJI CHA KITALU KWA MGENI RASMI, MHESHIMIWA MHAPA LUKO (MBUNGE)***

*Ndugu Mgeni Rasmi,*

*Mheshimiwa Diwani,*

*Ndugu Wajumbe wa Bodi ya Shule ya Sekondari Kwedihoma,*

*Ndugu wafanyabiashara waalikwa,*

*Ndugu wazazi, waandishi wa habari, na wananchi wote mliohudhuria katika mkutano huu,*

*Itifaki imezingatiwa.*

*Ndugu mgeni rasmi, kwa niaba ya wananchi wa Kijiji cha Kitalu, tunayo furaha kujumuika nawe katika mkutano huu unaotarajiwa kuleta tija kwa jamii ya Kitalu na taifa kwa ujumla. Tuna imani kwamba unaelewa fika jitihada zinazofanywa na wananchi wa Kitalu, hususani katika ujenzi wa Shule ya Sekodari Kwedihoma.*

*Ndugu mgeni rasmi, Shule ya Sekondari Kwedihoma ina jumla ya wanafunzi mia sita na arobaini, walimu kumi na sita, na walinzi wawili. Shule yetu ni ya kutwa na ina wanafunzi wa kidato cha kwanza hadi cha nne. Shule ina vyumba vinane vya madarasa vyenye mikondo miwili kwa kila darasa. Pia, ina chumba kimoja cha walimu na ofisi ya mkuu wa shule.*



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 86 07/03/2022 16:50

*Ndugu mgeni rasmi, miongoni mwa mafanikio tuliyonayo hapa shuleni ni ongezeko la wanafunzi kutokana na shule yetu kufanya vizuri kitaaluma. Pia, tumefanikiwa kupata ufaulu wa wastani katika masomo yote kwa ngazi ya wilaya, mkoa, na taifa kwa takribani miaka mitatu mfululizo.*

*Ndugu mgeni rasmi, licha ya mafanikio hayo, kuna changamoto kadhaa ambazo zimekuwa zikiikabili shule yetu. Miongoni mwa changamoto hizo ni upungufu wa vyumba vya madarasa na madawati, hali inayosababisha wanafunzi kusoma kwa kurundikana.*

*Ndugu mgeni rasmi, changamoto nyingine ni ukosefu wa maktaba unaosababisha wanafunzi kushindwa kujifunza kupitia vitabu mbalimbali na kupata maarifa zaidi kuhusu wanachojifunza. Vilevile, shule yetu haina chumba cha maabara. Hivyo, wanafunzi wa mchepuo wa sayansi wanapata tabu kwenda kufanya majaribio ya kisayansi katika shule ya jirani.*

*Ndugu mgeni rasmi, kutokana na changamoto hizo, tumeamua tuitane hapa ili tufanye harambee ya kuchangia ujenzi wa vyumba vya madarasa na chumba cha maabara. Tutaanza kutatua changamoto hizo kwanza kwani si rahisi kuzitatua zote kwa pamoja.*

*Ndugu mgeni rasmi, kutokana na uzoefu wetu wa kushiriki katika shughuli za maendeleo, kuna watu wanaoweza kuchangia kwa kushiriki moja kwa moja katika ujenzi, na wengine kwa kutoa fedha au vifaa vya ujenzi. Tunaheshimu na kuthamini mchango wa kila mmoja. Hivyo, tunakuomba uendeshe zoezi la harambee ili kuisaidia shule yetu kupunguza changamoto hizi.*

*Ndugu mgeni rasmi, bila kupoteza muda, tunakuomba ufungue rasmi zoezi letu la harambee kwa ajili ya ujenzi wa shule ya watoto wetu. Asanteni sana kwa kunisikiliza!*

Mwenyekiti wa Bodi alipomaliza kusoma risala, alimkaribisha mgeni rasmi kuanza zoezi la harambee. Mheshimiwa Mbunge alifungua zoezi hilo kwa kuanza na ahadi. Aliahidi kutoa mifuko 100 ya saruji na mabati 100. Alifuatiwa na Mheshimiwa Diwani ambaye aliahidi kutoa shilingi milioni moja. Baada ya viongozi hao kutoa ahadi zao, walifuatiwa na wafanyabiashara ambao waliahidi kutoa vifaa mbalimbali vya ujenzi. Wanakijiji waliahidi kutoa fedha na nguvu zao katika ujenzi. Baada ya zoezi la harambee kuisha, Katibu wa Bodi alitoa taarifa ya fedha taslimu na ahadi zilizotolewa. Kwa kuwa wanakijiji tayari walishatoa michango ya fedha taslimu na ahadi ya nguvukazi, ilikubaliwa kwamba ujenzi huo uanze mara moja. Mwenyekiti wa Bodi alimshukuru mgeni rasmi na wananchi wote kwa moyo wa kujitolea na ushirikiano waliouonesha, kisha aliahirisha mkutano.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 87 07/03/2022 16:50

## Maswali

1. Kwa nini wajumbe wa Bodi ya Shule waliamua kumwalika mgeni rasmi na wageni wengine?
2. Eleza muundo wa risala.
3. Kwa nini risala haikusomwa na mgeni rasmi?
4. Umejifunza nini kutokana na risala uliyoisoma?
5. Kwa nini Bodi ya Shule iliamua kuandika risala na si hotuba?

**Zingatia**

Risala ni taarifa ambayo, aghalabu, huandaliwa na kusomwa na mtu mmoja mbele ya mgeni rasmi kwa niaba ya kundi fulani la watu kwa lengo la kueleza mahitaji yao mbalimbali. Risala huwasilishwa kwa kusomwa. Pamoja na kuwa risala humlenga mgeni rasmi, huilenga pia hadhira inayohusika ili kupata ujumbe huo. Mara nyingi, risala husomwa katika shughuli mbalimbali za kijamii.

## Kazi ya 5.14



(a) Katika vikundi vya wanafunzi watatu, someni maandiko mbalimbali yanayohusu risala.

(b) Kila mmoja aeleze muundo wa risala alizozisoma katika kipengele (a).

**Zingatia**

Risala hujengwa na vipengele kadhaa, ikiwa ni pamoja na *kichwa* ambacho hutaja kwa ufupi lengo au kusudi la risala hiyo. Pia, hujengwa na *utangulizi* ambao ni sehemu ya utambulisho. Sehemu hii humtaja mgeni rasmi, viongozi, na watu wengine waliohudhuria. Vilevile, risala hujengwa na kipengele cha *kiini* ambacho hueleza maudhui ya risala hiyo. Katika kiini, maudhui yote ambayo aghalabu huwa mafanikio na changamoto, huelezwa. Aidha, risala huwa na *hitimisho* ambalo hueleza rai, maoni, na mapendekezo mbalimbali ya waandaji kwa ufupi. Pia, katika kipengele hiki, shukurani kwa waalikwa hutolewa.

Unapoandika risala, ni muhimu kuzingatia matumizi ya lugha fasaha na lengo la risala hiyo. Hali kadhalika, unapaswa kupangilia hoja katika mtiririko unaofaa na wenye mantiki. Risala ni njia mojawapo ya mawasiliano inayotumiwa na wanajamii katika matukio maalumu.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 88 07/03/2022 16:50

## Zoezi la 5.6

1. Fafanua maana ya risala.
2. Eleza mambo ya kuzingatia katika uandishi wa risala.
3. Risala huwa na muundo gani?
4. Kwa nini ni muhimu kuandika risala?
5. Fafanua vipengele vinne ambavyo huweza kuelezwa katika hitimisho la risala.

## Kazi ya 5.15

(a) Andika risala kwa kuzingatia utaratibu wa uandishi wa risala, kisha mpatie mwenzako aisome.

(b) Jadiliana na wenzako kuhusu vipengele vilivyozingatiwa katika risala hiyo.

## Kuandika kumbukumbu za mikutano

## Kazi ya 5.16

**Soma habari ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata**.

Katika Kijiji cha Mbalule, palikuwa na mzee mmoja aliyejulikana kwa jina la Nyasuma. Mzee huyu alikuwa na busara na hekima kijijini hapo. Wanakijiji wa Mbalule walimpenda sana kwa sababu ya uhenga wake. Mzee Nyasuma alikuwa na mke na mtoto mmoja wa kike aliyejulikana kwa jina la Zuneka.

Zuneka alikuwa mtoto wa pekee katika familia yao. Hivyo, alipendwa sana na wazazi wake. Licha ya kuwa mtoto wa pekee kwao, Zuneka alikuwa mtiifu na mwenye adabu sana kwa watu wa marika yote. Hali hiyo ilimfanya apendwe sana na watu wote katika kijiji chao. Zuneka alikuwa mwanafunzi wa kidato cha nne katika Shule ya Sekondari Kipupwe. Katika shule hiyo, walimu wengi walimpenda sana kutokana na nidhamu yake. Jitihada zake katika masomo zilimpa sifa nzuri shuleni hapo na katika shule za jirani.

Zuneka alikuwa na desturi ya kusimamia usafi wa mazingira kila alipofika shuleni. Alihakikisha kuwa mazingira yote ya shule ni safi kabla ya kuingia darasani kwa sababu yeye ndiye alikuwa kiranja mkuu wa shule yao. Siku moja, baada ya shule kufunguliwa, Zuneka na viongozi wengine wa serikali ya wanafunzi walifanya mkutano. Katika mkutano huo, alikuwapo mwalimu Loungo ambaye alikuwa zamu wiki hiyo. Pia, alikuwapo mwalimu Gakitindi ambaye alikuwa mwalimu wa unasihi. Mkutano uliongozwa na Zuneka ambaye alikuwa mwenyekiti.

Mwenyekiti **alifungua mkutano** kwa kuwakaribisha wajumbe. Katika salamu za ufunguzi, alianza kwa kuwapongeza wajumbe kwa likizo ndefu waliyokuwa nayo na kwa majukumu ambayo wamekuwa wakiendelea nayo. Alisema, "Hongereni sana kwa likizo! Ninaamini kila mmoja amefurahia na amejifunza mambo mengi huko nyumbani, na kwamba tumewasaidia vyema wazazi wetu majukumu mbalimbali." Aliendelea kusema, "Kama tujuavyo, ni utaratibu wetu, sisi viongozi, kufanya mikutano pale tunapokaribia kufunga shule na tunapofungua. Tunafanya hivyo ili kutathmini na kujadiliana kuhusu mambo mbalimbali yanayotuhusu sisi viongozi na kujiwekea mikakati mbalimbali katika muhula mpya. Tumekuwa tukifanya hivyo ili kuhakikisha kunakuwa na mgawanyo mzuri wa majukumu kwa viongozi wote."



Baada ya maelezo hayo, alimkaribisha mwanafunzi aliyeitwa Mbolela ambaye ni katibu ili asome ajenda ya mkutano. Katibu alisoma ajenda. Baada ya kumaliza kusoma, mwenyekiti alimpa nafasi ya kusoma **muhtasari wa kumbukumbu za mkutano uliopita** kwa ajili ya kuthibitisha taarifa hizo kabla ya kuendelea na dondoo jingine la ajenda. Wajumbe walisikiliza na kusahihisha sehemu zilizokuwa na dosari. Kisha, walithibitisha kuwa hizo zilikuwa kumbukumbu sahihi za mkutano uliopita. Baada ya zoezi hilo, katibu aliruhusiwa kusoma dondoo lililofuata katika ajenda, ambapo mwenyekiti alianza kulifafanua kabla ya kuwapa wajumbe nafasi



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 90 07/03/2022 16:50

ya kujadili na kutoa maoni yao. Walipomaliza kujadili madondoo yote ya msingi, waliingia katika dondoo la **mengineyo**. Wajumbe walitaja na kuelezea mambo mengine ambayo hayakujadiliwa katika madondoo msingi ya ajenda ya mkutano huo. Mwishoni, mwenyekiti alisimama kwa ajili ya dondoo la mwisho ambalo lilikuwa **kufunga mkutano**. Mwenyekiti aliwashukuru wajumbe kwa kushiriki vyema katika mkutano, kisha alifunga mkutano.

Baada ya mkutano kufungwa, walimu walimpongeza Zuneka na viongozi wengine kwa kuwa waadilifu katika majukumu ya uongozi wa shule waliyopewa. Mwalimu Gakitindi aliwasisitiza viongozi hao kusoma kwa bidii kwani elimu ndiyo kila kitu katika maisha. Mwalimu Loungo naye aliongeza kwa kusema, "Mtakapopata changamoto yoyote, msisite kutuona ili tusaidiane kuzitatua."

Walimu walipomaliza kuzungumza, waliwaruhusu viongozi hao kwenda kuendelea kusimamia shughuli za usafi. Wanafunzi wengi walifurahi kumwona Zuneka kwani walimpenda sana kwa sababu ya jitihada, upendo, na uchangamfu wake. Pia, Zuneka alifurahi kuwaona wanafunzi wenzake. Aliungana nao katika kazi ya kufyeka nyasi.

## Maswali

1. Kutokana na habari uliyoisoma, eleza maana ya kumbukumbu za mikutano.
2. Bainisha mambo ya kuzingatia katika uandishi wa kumbukumbu za mikutano.
3. Kwa kutumia mifano, fafanua vipengele vya kumbukumbu za mikutano.
4. Eleza kwa ufupi maana ya neno ajenda.

**Zingatia**


Kumbukumbu za mkutano huandikwa ili kusaidia katika utekelezaji na ufuatiliaji wa mambo yaliyojadiliwa, kuridhiwa, kuamuliwa na kuazimiwa katika mkutano. Pia, huwa kama marejeleo ya waliohudhuria, maadhura, pamoja na mambo mengine yaliyofanyika. Hivyo, kumbukumbu za mkutano ni muhtasari unaoandikwa kwenye mkutano kueleza mambo yaliyojadiliwa na uamuzi uliofikiwa katika mkutano. Kumbukumbu huandikwa kwa ufupi kwa kudondoa mambo muhimu ili kutoa picha ya jumla ya yaliyojiri mkutanoni. Katika uandishi wa kumbukumbu za mkutano, mwandishi anapaswa awe na stadi za kusikiliza na kuandika ili aweze kufupisha mambo yanayojadiliwa na kukubaliwa wakati wa mkutano.

Kumbukumbu za mkutano zina mpangilio maalumu ambao huhusisha kichwa cha kumbukumbu, orodha ya waliohudhuria na ambao hawakuhudhuria pamoja na ajenda ya mkutano. Vilevile, huzingatia hoja muhimu tu kwa sababu mambo mengi hujadiliwa mkutanoni; hivyo, yale muhimu tu ndiyo huandikwa. Kadhalika, uwasilishwaji wake hutumia mtindo mwepesi na sentensi zake huwa kamilifu ili kuziwezesha kueleweka kirahisi kwa atakayezisoma.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 91 07/03/2022 16:50

## Kazi ya 5.17



(a) Kusanya kumbukumbu mbalimbali za mikutano.

(b) Chunguza na ubainishe muundo na lugha iliyotumika katika kuandika kumbukumbu hizo.

**Zingatia**

Mkutano wowote ule unatakiwa uwe na ajenda. Ajenda hubeba madondoo yanayopaswa kujadiliwa kwa siku hiyo. Madondoo hayo hujumuisha utangulizi unaobeba vipengele vya ufunguzi wa mkutano, matangazo na uthibitisho wa kutimia kwa akidi. Aidha, kama mkutano utajadili kumbukumbu za mkutano uliotangulia, basi kutakuwa pia na dondoo la kupitia kumbukumbu za mkutano uliopita, kisha lifuate dondoo la yatokanayo na kumbukumbu na masuala mengine yatakayozungumziwa. Kadhalika, ajenda hujumuisha dondoo la mengineyo, ambapo mambo ambayo hayakujadiliwa katika madondoo ya msingi hujadiliwa. Aidha, kipengele cha kufunga mkutano hujumuishwa katika ajenda, ambapo katika kipengele hiki, mkutano huahirishwa. Wakati wa mkutano, katibu huandika tini za kumbukumbu na, baada ya mkutano, huandaa kumbukumbu za mkutano kwa kuziandika kikamilifu.

Muundo wa kumbukumbu za mkutano huwa na mambo kadha wa kadha. Kwanza, huwa na *kichwa cha kumbukumbu* ambacho huandikwa kwa herufi kubwa, wino uliokoza, na kwa ufupi kikijumuisha walengwa wa mkutano, lengo, mahali mkutano ulipofanyika, tarehe ambayo mkutano ulifanyika na muda ambapo ulianza.

Pili, kumbukumbu huwa na *mahudhurio* ambayo hubainisha orodha ya watu waliohudhuria na wasiohudhuria mkutano. Orodha ya wasiohudhuria mkutano huweza kuonesha waliotoa taarifa na ambao hawakutoa taarifa. Vilevile, huweza kuonesha waliohudhuria kwa kualikwa. Wasiohudhuria wanaweza kubainishwa endapo mkutano unahusisha watu wachache. Kwa mkutano unaohusisha watu wengi, ni vigumu kuorodhesha wale ambao hawakuhudhuria mkutano; hivyo, idadi ya waliohudhuria tu ndiyo huorodheshwa.

Tatu, kumbukumbu za mkutano huwa na *ajenda* ambayo hujumuisha madondoo yaliyojadiliwa katika mkutano. Madondoo ya ajenda huandikwa kwa ufupi na huorodheshwa kwa kufuatana na kwa namba. Uwekaji wa namba hurahisisha urejeleaji wa kumbukumbu. Dondoo la kufungua mkutano hueleza muda ambao mkutano ulifunguliwa na aliyefungua mkutano huo. Pia, dondoo la kupitia kumbukumbu za mkutano uliopita hujumuishwa kama lipo. Kwa kawaida, upitiaji hufanyika kama mkutano huo ni mwendelezo wa mkutano uliopita. Wajumbe wa mkutano hupaswa kuyapitia yaliyojadiliwa katika mkutano uliopita ili kuyathibitisha kuwa ni kumbukumbu sahihi. Dondoo la kupitia kumbukumbu za mkutano uliopita



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 92 07/03/2022 16:50

halitakuwapo endapo mkutano huo unafanyika kwa mara ya kwanza. Mapitio ya kumbukumbu za mkutano uliopita hufuatiwa na dondoo la yatokanayo na kumbukumbu za mkutano uliopita kwa lengo la kujua utekelezaji wa maamuzi na maazimio ya mkutano. Baada ya dondoo la yatokanayo na kumbukumbu za mkutano uliopita, hufuata madondoo yanayohusu mambo yaliyojadiliwa katika mkutano unaohusika. Uamuzi uliofikiwa kutokana na madondoo hayo hutambulishwa kwa maneno kama vile iliamuliwa, iliazimiwa, ilihojiwa, iliagizwa, ilielezwa na kadhalika. Maneno hayo huandikwa kwa herufi kubwa na wino uliokoza ili yaweze kuonekana kwa urahisi.

Dondoo la mwisho huhusu kufunga mkutano. Dondoo hili hueleza muda ambao mkutano ulifungwa na aliyefunga mkutano huo. Mwishoni mwa kumbukumbu za mkutano, huandikwa jina la katibu na mwenyekiti, saini zao pamoja na tarehe ili kuzipa kumbukumbu urasmi.

## Zoezi la 5.7

1. Eleza lengo la kuandika kumbukumbu za mikutano.
2. Bainisha tofauti zilizopo baina ya ajenda na madondoo.
3. Fafanua changamoto zinazoweza kujitokeza endapo kumbukumbu za mkutano hazitaandikwa vizuri.

## Kazi ya 5.18

**Soma mfano ufuatao wa kumbukumbu za mkutano, kisha jibu maswali yanayofuata.**

**KUMBUKUMBU ZA MKUTANO WA VIONGOZI WA SERIKALI YA WANAFUNZI WA SHULE YA SEKONDARI IGOMBA ULIOFANYIKA TAREHE 05 JUNI 2021 KATIKA UKUMBI WA SHULE YA SEKONDARI IGOMBA KUANZIA SAA 3:00 ASUBUHI**

**MAHUDHURIO**

**Waliohudhuria**

| | | |
|---|---|---|
| 1. | Zuneka Nyasuma | Mwenyekiti |
| 2. | Mbolela Walwa | Katibu |
| 3. | Kajuju Mwakatope | Mjumbe |

| | |
|---|---|
| 4. Kandida Sitembei | Mjumbe |
| 5. Nyabusu Kajige | Mjumbe |
| 6. Katembo Bulugu | Mjumbe |

**Waalikwa**

| | |
|---|---|
| 1. Kalika Loungo | Mwalimu wa zamu |
| 2. Itika Gakitindi | Mwalimu wa unasihi |

**Maadhura**

| | |
|---|---|
| 1. Mpita Peter | Mjumbe |
| 2. Bushagala Kapango | Mjumbe |

**Wasiohudhuria**

| | |
|---|---|
| 1. Nazurula Sichoki | Mjumbe |
| 2. Mwaifanga Mkuniza | Mjumbe |

**AJENDA**

1. Kufungua mkutano
2. Kupitia kumbukumbu za mkutano wa tarehe 06 Oktoba 2020
3. Yatokanayo na kumbukumbu za mkutano uliopita
4. Tathmini ya utendajikazi wa viongozi kwa muhula wa kwanza (Januari - Juni 2021)
5. Mgawanyo wa majukumu kwa muhula wa pili (Julai - Disemba 2021)
6. Mengineyo
7. Kufunga mkutano

**Dondoo Na. 1 katika Ajenda: Kufungua Mkutano**

1.1 Mkutano ulifunguliwa saa 3:00 asubuhi kwa salamu na taarifa fupi ya makaribisho kutoka kwa mwenyekiti.

**Dondoo Na. 2 katika Ajenda: Kupitia Kumbukumbu za Mkutano wa Tarehe 06 Oktoba 2020**

2.1 Kumbukumbu zilizosomwa na katibu na **ILIKUBALIWA** kuwa yaliyoandikwa ndiyo yaliyojadiliwa.

**Dondoo Na. 3 katika Ajenda: Yatokanayo na Kumbukumbu za Mkutano Uliopita**

3.1 **ILIARIFIWA** kuwa ufadhili wa wanafunzi wenye ulemavu umeshapatikana na kwamba utaanza kutolewa ndani ya miezi mitatu ijayo.

3.2 **ILIFAFANULIWA** kuwa wanafunzi wote waliokuwa wamesimamishwa masomo wamerejeshwa kwa sharti la kujirekebisha.

**Dondoo Na. 4 katika Ajenda: Tathmini ya Utendajikazi wa Viongozi kwa Muhula wa Kwanza (Januari - Juni 2021)**

4.1 **ILIARIFIWA** kwamba tathmini ya utendajikazi wa viongozi kwa muhula wa kwanza wa masomo ilifanyika. Tathmini hiyo ilifanyika kwa kuangalia bidii ya viongozi katika kutekeleza majukumu waliyopangiwa, weledi, ufanisi, na ushirikiano baina ya viongozi wenyewe pamoja na ushirikiano walioupata kutoka kwa walimu na wanafunzi wote.

4.2 **ILIARIFIWA** kuwa baadhi ya viongozi walitekeleza majukumu yao vizuri. Hawa walipongezwa.

4.3 **ILIARIFIWA** zaidi kuwa kuna viongozi waliolegalega. Hawa walihimizwa kufanya vizuri.

4.4 **ILIELEZWA** kuwa kulikuwa na changamoto mbalimbali za utendajikazi wao katika muhula wa kwanza kama vile uzembe na utoro.

**Dondoo Na. 5 katika Ajenda: Mgawanyo wa Majukumu kwa Muhula wa Pili (Julai - Desemba 2021)**

5.1 **ILIJADILIWA** na **KUKUBALIWA** kuwe na mgawanyo mpya wa majukumu ili kila kiongozi apate uzoefu wa kusimamia majukumu mbalimbali.

5.2 **ILIHIMIZWA** kuwe na ushirikiano na bidii katika kazi baina ya viongozi ili kuleta maendeleo katika shule yao.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 95 07/03/2022 16:50

**Dondoo Na. 6 katika Ajenda: Mengineyo**

6.1 **YALIPENDEKEZWA** mambo mbalimbali kwa ajili ya kuboresha mazingira ya shule. Mambo hayo ni kuongezwa kwa vifaa vya kufanyia usafi, ukarabati wa viwanja vya michezo, na kuongezwa kwa vitabu ili kila mwanafunzi apate fursa ya kujisomea bila kusumbuliwa.

6.2 **ILISHAURIWA** kuanzishwe mradi wa ugawaji wa taulo za kike shuleni ili kuwasaidia wasichana ambao hulazimika kutohudhuria masomo wakiwa katika hedhi.

**Dondoo Na. 7 katika Ajenda: Kufunga Mkutano**

7.1 Mkutano ulifungwa na mwenyekiti mnamo saa 6:30 mchana kwa kuwashukuru wajumbe kwa ushirikiano na michango yao ya mawazo.

Zimeandaliwa na: Mbolela Walwa (Katibu)

Saini: …………………. Tarehe: ………………………

Zimeidhinishwa na: Zuneka Nyasuma (Mwenyekiti)

Saini: …………………. Tarehe: ………………………

## Maswali

1. Kumbukumbu za mkutano ulizozisoma zilikuwa na lengo gani?
2. Eleza hatua utakazozifuata wakati wa kuandika kumbukumbu za mikutano.
3. Kuna umuhimu gani wa kuandika kumbukumbu za mikutano?

**Zingatia**

Kumbukumbu za mikutano huandikwa kwa kufupisha mambo muhimu tu yanayojadiliwa. Pia, uandishi wa kumbukumbu lazima ufuate mpangilio na mfuatano wa madondoo ya ajenda ya mkutano ili mambo yaliyojadiliwa yabainike katika uandishi. Vilevile, kumbukumbu za mkutano huandikwa kwa maneno na sentensi zenye maana kamili ili kuepusha utata. Kadhalika, hutumia njeo ya wakati uliopita na kauli ya utendwa ili kuonesha kwamba yaliyoandikwa ni makubaliano ya mkutano na si maamuzi ya mtu mmoja.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 96 07/03/2022 16:50

## Kazi ya 5.19



(a) Katika vikundi andaeni ajenda, kisha fanyeni mkutano wa mfano. Kila kikundi kichague katibu aandike kumbukumbu za mkutano huo na kuwasilisha darasani.

(b) Eleza ubora na upungufu wa kumbukumbu zilizowasilishwa darasani.

## Zoezi la marudio

1. Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi:

(i) Kazi zifuatazo huwa na mada mahususi na hueleza ukweli wa jambo <u>isipokuwa</u> ...............
  (a) hotuba
  (b) kumbukumbu za mikutano
  (c) risala
  (d) insha
  (e) ajenda

(ii) Andiko ambalo huandikwa kwa lengo la kueleza mahitaji mbalimbali kwa mtu anayehusika linafahamika kwa jina gani?
  (a) Kumbukumbu za mkutano
  (b) Risala
  (c) Kiini cha insha
  (d) Hotuba
  (e) Insha ya kiada

(iii) Andiko gani husaidia na hurahisisha utekelezaji wa mambo yaliyokubaliwa?
  (a) Risala
  (b) Kumbukumbu za mkutano
  (c) Insha ya kiada
  (d) Hotuba
  (e) Insha ya ufafanuzi

(iv) Kipengele gani huonesha idadi ya wajumbe waliofika na ambao hawakufika kwenye mkutano?
  (a) Kichwa cha kumbukumbu
  (b) Ajenda
  (c) Mengineyo
  (d) Mahudhurio
  (e) Hitimisho



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 97 07/03/2022 16:51

(v) Maelezo maalumu yanayotolewa kwenye hadhara huitwa …….. .
   (a) hotuba
   (b) risala za taarifa
   (c) kumbukumbu za mkutano
   (d) risala za mafundisho
   (e) insha za kiada

2. Oanisha maana zilizopo katika Orodha **A** na dhana zilizopo katika Orodha **B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi ili kuleta maana sahihi ya Kiswahili.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Hutumiwa kuonesha kuwa sentensi imekamilika | A. nuktapacha |
| | B. mkato |
| (ii) Hutumika kuonesha kuwa kuna orodha inafuata | C. ritifaa |
| | D. nuktamkato |
| (iii) Hutumiwa kwenye nukuu kuonesha kuwa kuna maneno ambayo yameachwa | E. nukta |
| | F. alama za mtajo |
| (iv) Hutumika kuweka pumziko fupi | G. nuktakatishi |
| (v) Hutumiwa kuonesha kuwa maneno yanayofuata au yanayotangulia yamesemwa au yametamkwa na msemaji mwingine | |

3. Chambua vipengele vya kuzingatia katika uandishi wa kumbukumbu za mkutano.
4. Eleza tofauti baina ya risala na hotuba.
5. Muundo wa hotuba unatofautiana vipi na muundo wa insha?
6. Fafanua tofauti zilizopo kati ya insha za maelezo na insha za usimulizi.
7. Insha hutofautianaje na risala?
8. Fafanua mazingira yanayochochea kuwapo kwa matumizi ya hotuba.
9. Kumbukumbu za mikutano huandikwa na nani?
10. Kuna tofauti gani kati ya kipengele cha *mwanzo* na *utangulizi* katika hotuba?



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 98 07/03/2022 16:51

# Sura ya Sita

## Ufahamu

**Utangulizi**

*Mtu anaweza kufahamu au kuelewa jambo kwa kusikiliza, kuona, au kusoma. Akishalielewa jambo hilo, anaweza kulielezea kwa maneno yake mwenyewe bila kupoteza maana yake ya msingi. Katika sura hii, utajifunza ufahamu wa kusikiliza, kuona, na kusoma. Umahiri utakaoujenga utakuwezesha kuelewa mambo mbalimbali kwa njia ya kusikiliza, kuona, na kusoma. Pia, utakuza stadi za kuzungumza, kusoma, kuandika, na kufupisha habari.*

### Dhana ya ufahamu

**Kazi ya 6.1**

**Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**



### Maswali

1. Je, unafikiri kijana anayeonekana kwenye picha anataka kufanya nini?
2. Pendekeza njia ambazo ungeweza kuzitumia ili kutatua changamoto aliyonayo kijana huyo.
3. Unajifunza nini kutokana na picha uliyoichunguza?

**Zingatia**

Ufahamu ni uelewa wa jambo au habari kutokana na kusikiliza, kuona, au kusoma. Uelewa huo humsaidia mtu kulielezea jambo hilo kwa maneno yake bila kupoteza maana yake. Uelezaji huo unaweza kufanywa kwa njia ya mazungumzo au maandishi. Ufahamu hukuza stadi za kuzungumza, kusikiliza, na kusoma. Vigezo vinavyotumiwa kutambua ikiwa mtu ameelewa alichokisikia, alichokiona, au alichokisoma ni uwezo wake wa kukielezea kwa maneno yake mwenyewe bila kupoteza maana, uwezo wa kujibu maswali, au wa kukifupisha.

Jambo ambalo mtu anapaswa kuzingatia katika ufahamu ni kumakinikia suala analolisikiliza, analoliona, au analolisoma. Wakati mwingine, anapaswa kuwa mdadisi ili kukuza uelewa wake. Hali hii itamwezesha kupata maarifa na ujuzi utakaomsaidia katika maisha yake. Vilevile, atajenga uwezo wa kufupisha habari yoyote.

## Ufahamu wa kusikiliza

### Kazi ya 6.2



**Msikilize mwenzako akikusomea wimbo ufuatao, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Tufani iso kifani, ni hatari nakwambia,
Jihadhari x 2 usije kuangamia.

Tufani ni hatarishi, katu huwezi ikinga,
Jihadhari x 2 usije kuangamia.

Tufani yaangamiza, wakubwa hata wadogo,
Jihadhari x 2 usije kuangamia.

Tufani yaleta homa, maafa yasababisha,
Jihadhari x 2 usije kuangamia.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 100 07/03/2022 16:51

Tufani ikikukumba, wapi utakimbilia,
Jihadhari x 2 usije kuangamia.

Tufani inamaliza, nguvukazi ya taifa,
Jihadhari x 2 usije kuangamia.

Wasikilize wakuu, usije vunjika guu,
Jihadhari x 2 usije kuangamia.

Ndugu zetu walokumbwa, na tufani tuwapende,
Tuwapende x 2 katu tusije watenga.

Tuwapende kwa upeo, kamwe tusiwabague,
Tuwapende x 2 katu tusije watenga.

## Maswali

1. Katika wimbo uliousikiliza, mtunzi anazungumzia nini?
2. Kwa nini mtunzi amerudiarudia kibwagizo katika wimbo wake?
3. Mtunzi ana maana gani anaposema, "Tufani inamaliza, nguvukazi ya taifa"?
4. Umejifunza nini kutokana na wimbo uliousikiliza?
5. Eleza kuhusu lugha ya picha iliyotumika katika wimbo uliousikiliza.

**Zingatia**

Ufahamu wa kusikiliza ni uwezo wa kulielewa na kulielezea kwa usahihi jambo unalolisikiliza. Unaweza kupata habari kwa kusimuliwa, na/au kusomewa. Msikilizaji anatakiwa kusikiliza kwa makini na kuelekeza mawazo yake katika jambo linalosomwa au kuzungumzwa ili kubaini mawazo makuu yanayozungumzwa au yanayosomwa. Kadhalika, ili kutokwamisha mawasiliano, msikilizaji anapaswa kufahamu utaratibu wa matamshi na kuelewa lafudhi ya lugha anayotumia mzungumzaji ili asishindwe kuelewa kile kinachosimuliwa au kinachosomwa. Aidha, msikilizaji anatakiwa kuwa makini kusikiliza kama kuna semi zilizotumika ili aweze kuzihusisha na matini husika. Hivyo, msikilizaji anapaswa kuwa makini katika kufasiri na kuchanganua mambo anayoyasikia. Ufahamu wa kusikiliza ni muhimu sana kwani unamwezesha msikilizaji kupata taarifa, maarifa, na ujuzi utakaomsaidia katika shughuli za kila siku.

## Kazi ya 6.3



Sikiliza taarifa ya habari kutoka kituo chochote cha redio au televisheni, kisha andika ufupisho wa taarifa hiyo.

**Zingatia**

Baada ya kusikiliza habari, unaweza kujipima kama umeielewa kwa kubaini mawazo makuu yaliyomo katika habari hiyo. Hivyo, unatakiwa kuisikiliza kwa makini ili uweze kuisema au kuieleza kwa ufupi na kwa lugha rahisi. Unapofupisha habari uliyoisikiliza, unatakiwa kuielezea kwa muhtasari na kwa maneno yako bila kupoteza maana ya msingi. Pia, unapaswa kuyapanga mawazo hayo katika mtiririko unaofaa na wenye mantiki. Ufupisho ni kipengele muhimu cha kupima usikivu na uelewa wako na, hivyo, kudhihirisha kuwa ulichokisikiliza umekielewa.

## Zoezi la 6.1

1. Fafanua mambo muhimu ya kuzingatia katika ufahamu wa kusikiliza.
2. Msikilize mwenzako akisoma habari ifuatayo, kisha bainisha mawazo makuu.

   Wananchi wa Kijiji cha Lunga walikuwa na maendeleo sana kutokana na mshikamano waliokuwa nao. Waliishi kwa upendo na kusaidiana kwa hali na mali. Walikuwa na miradi ya kuku na ng’ombe ambayo iliwawezesha kupata fedha kwa ajili ya maendeleo ya kijiji chao.

   Kwa bahati mbaya, maisha hayo mazuri yalibadilika ghafla. Baadhi ya wazee walijiingiza katika imani za kishirikina na kuharibu ustawi wa kijiji. Imani hizo ziliwafanya wachukiane. Maendeleo yaliyokuwa yameshamiri kijijini hapo yalitoweka mithili ya moshi utokomeavyo angani. Miradi yote ilikufa na upendo ulitoweka. Watu wengi hawakufurahishwa na imani hizo potofu. Walijitahidi kurudisha hali ya amani kwa kuwaunganisha vijana na kuwapa elimu. Vijana hao walielimika na kuanza kukemea imani potofu.

3. Fupisha kwa kuzungumza kwa maneno yasiyozidi 50 habari uliyoisikiliza.

## Ufahamu wa kusoma

### Kazi ya 6.4

**Soma kisamafunzo kifuatacho, kisha jibu maswali yanayofuata**.

Odafa ni msichana aliyezaliwa katika familia ya watoto watano wa Mzee Zumbe. Katika familia yao, kulikuwa na wasichana wawili na wavulana watatu. Odafa alikuwa mtoto wa pili kuzaliwa. Hali ya familia yao ilikuwa **duni**. Kwa sababu hiyo, baadhi ya watoto hawakuweza kuendelea na masomo ya sekondari. Mama yake Odafa, aliyeitwa Nachao, alikuwa mvumilivu, mchapakazi, na mwenye upendo.

Siku moja, Mzee Zumbe na familia yake walikwenda shambani kulima. Walipokuwa wanalima, Odafa alianzisha mazungumzo, akasema, "Nawaonea huruma wazazi wangu." Mzee Zumbe akadakia, "Umewaza nini mpaka kusema hayo mwanangu?" Odafa akaeleza, "Nimetafakari kuhusu maisha ya familia yetu yalivyo duni. Tunalima eneo dogo kwa sababu ya kutumia jembe la mkono, na tunapata mavuno kidogo. Ninajua kuwa *jembe halimtupi mkulima*, lakini lini tutakuwa na uwezo wa kulima kwa trekta? Lini tutaondokana na **ukata**?" Mama yake aliposikia maneno hayo, alihuzunika sana kwani naye alikuwa anaumia kutokana na maisha magumu waliyokuwa nayo. "*Mungu si Athumani* mwanangu, iko siku na sisi tutaupa kisogo ukata. Usikate tamaa, wewe una nafasi ya kubadili maisha yetu. Sisi tumeshazeeka, lakini maisha yenu ndiyo yanaanza," mama alisema kwa tabasamu.

Maneno ya mama *yaliuchoma moyo* wa Odafa. Wakati huo, Odafa alikuwa anasoma kidato cha nne. Aliamua kusoma kwa bidii kwani aliamini kuwa *elimu ni ukombozi wa maisha yao*. "Hata mkulima na mfugaji wanahitaji elimu ili waweze kufuga na kulima kwa **tija**," Odafa alisema kimoyomoyo.

Odafa alihitimu masomo yake ya kidato cha nne. Baada ya miezi kadhaa, matokeo yalitoka na alikuwa amefanya vizuri katika mitihani yake. Alichaguliwa kujiunga na kidato cha tano. Alipofika huko, aliendelea na jitihada zake katika masomo akafaulu na kwenda chuo kikuu. Alijiunga na Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine. Alipohitimu mafunzo yake ya chuo kikuu, hakutaka kusubiri kuajiriwa. Alitumia taaluma yake ya kilimo kwenye mashamba ya familia. Kwa kuwa hakuwa na mtaji, aliamua kuanzisha kilimo cha mbogamboga kwa kutumia nguvu zake mwenyewe. Aliwashauri ndugu zake waungane naye kwani *kidole kimoja hakivunji chawa*. Aliamini kuwa kilimo cha mbogamboga kitawawezesha kupata fedha za mtaji na za **kujikimu**. Ndugu zake walikubali mawazo ya Odafa kwa kuwa *umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu*. Waliungana na kufanya kazi kwa bidii. Jitihada zao zilizaa matunda mazuri. Msimu wa kwanza, walipata mazao mengi. Walipoyavuna



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 103 07/03/2022 16:51

na kuyauza, walipata fedha za kutosha na kuamua kuendeleza kilimo cha alizeti. Walianza na ekari tano. Alizeti hiyo ilipandwa na kutunzwa kitaalamu hadi ilipopevuka. Walipoiuza, walipata mtaji mkubwa zaidi uliowawezesha kulima mazao mengine ya biashara na chakula. Katika kilimo hicho, walitoa ajira kwa watu mbalimbali wa kijijini kwao. Maisha yao yalibadilika kutoka kuwa duni na kuwa bora.

Baada ya miaka mitano, kila mmoja alikuwa na uwezo wa kuendesha maisha yake. Walinunua maeneo kadhaa kwa ajili ya kuendeleza kilimo. Odafa alikuwa na moyo wa upendo kwa ndugu zake na jamii nzima inayowazunguka. Aliitisha mkutano wa vijana wote pale kijijini na kuwashauri waanzishe vikundi vidogovidogo vitakavyowasaidia kujikomboa kimaisha. Aliwaeleza kuwa, watakapojiunga katika vikundi na kubuni miradi, wataweza kupata mkopo kutoka katika taasisi za kifedha. Vijana wote walikubaliana na ushauri wa Odafa. Odafa aliwaambia kuwa, watakapojiunga katika vikundi, wasisahau kuandaa katiba za vikundi zitakazowaongoza. Aliwaahidi kumtafuta mtaalamu wa masuala ya uanzishaji wa vikundi ili aje kuwapa semina kuhusu utaratibu wa kuanzisha vikundi. Vijana walimshukuru Odafa kwa ushauri mzuri.

## Maswali

1. Pendekeza kichwa cha habari cha kisamafunzo ulichokisoma.
2. Kwa nini Odafa hakutaka kusubiri kuajiriwa baada ya kuhitimu mafunzo yake ya chuo kikuu?
3. Eleza wasifu wa Odafa kutokana na kisamafunzo ulichokisoma.
4. Kwa nini vijana walihitaji mtaalamu wa masuala ya uanzishaji wa vikundi?
5. Umejifunza nini kutokana na kisamafunzo ulichokisoma? Fafanua mafunzo yasiyopungua matatu uliyoyapata.
6. Eleza maana ya msamiati na semi zifuatazo:
   (a) duni
   (b) tija
   (c) ukata
   (d) kujikimu
   (e) elimu ni ukombozi wa maisha
   (f) choma moyo
   (g) kidole kimoja hakivunji chawa



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 104 07/03/2022 16:51

**Zingatia**

Ufahamu wa kusoma ni uelewa unaojengwa kwa kusoma matini mbalimbali. Unaposoma, unatakiwa kuzingatia maana za maneno, sentensi, na habari yote kwa ujumla. Pia, unapaswa kuelewa maana za msamiati na misemo kama ilivyotumika katika matini husika. Hii ni kwa sababu neno linaweza kuwa na maana zaidi ya moja. Unaweza kutumia kamusi kupata maana ya msingi, ingawa muktadha katika matini ndio wa kuzingatia zaidi. Pia, unatakiwa kubainisha mawazo makuu yaliyomo katika matini.

Kuna njia mbili za kusoma, yaani, kusoma kimya na kusoma kwa sauti. Kusoma kimya ni namna ya usomaji ambapo msomaji husoma andiko pasipo kutoa sauti. Katika kusoma kimya, unapaswa kuzingatia alama za uakifishaji. Vilevile, usomaji wa namna hii unakuhitaji uwe makini. Hupaswi kuhamisha mawazo kutoka kwenye habari unayoisoma.

Kusoma kwa sauti ni namna ya usomaji ambapo msomaji hutamka maneno yaliyomo katika matini anayoisoma kwa kutoa sauti. Unaposoma kwa sauti, unapaswa kuzingatia matamshi sahihi, na nguvu ya utamkaji katika silabi za maneno au sentensi zilizowekewa mkazo ili kupata maana sahihi za maneno. Aidha, unaposoma kwa sauti, unapaswa kutamka maneno kwa usahihi. Ili kufahamu vizuri jambo unalolisoma, huna budi kuzingatia kanuni za usomaji bora. Kanuni hizo ni kusoma kwa sauti inayosikika vizuri, kutamka maneno kwa usahihi na kwa kuzingatia lafudhi ya Kiswahili, kuzingatia alama za uakifishaji, pamoja na kusoma kwa kasi stahiki.

Usomaji mzuri utakusaidia kujenga mazoea mazuri ya kusoma na kutamka maneno kwa usahihi na kuwa na kasi stahiki ya usomaji wa matini mbalimbali. Pia, utamwezesha atakayekusikiliza kuzingatia na kuelewa kwa urahisi jambo unalolisoma.

## Kazi ya 6.5

**Soma hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

Hapo zamani za kale, kulikuwa na kijana mmoja aliyeitwa Kizi. Kijana huyo alikuwa na umri wa miaka ishirini na alikuwa akiishi na wazazi wake. Kizi alikuwa kifungua mimba na kitinda mimba kwa mama yake. Hivyo, alipendwa sana na wazazi wake. Wazazi wake walikuwa na uwezo kimaisha; hivyo, walimpatia mahitaji yake yote. Jambo hili lilimfanya Kizi abweteke na kujiona mtu wa matawi ya juu. Hakujishughulisha na kazi yoyote ya kumwingizia kipato. Alipenda kukaa kijiweni na kupiga domo na vijana wenzake waliokuwa wanafanya biashara ndogondogo.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 105 07/03/2022 16:51

Baada ya miezi kadhaa kupita, wazazi wa Kizi walifariki dunia kwa ajali ya gari. Kizi hakuamini masikio yake alipopata taarifa hizo. Alipata mshtuko na kuzirai. Majirani walimpeleka hospitalini ambako alipatiwa matibabu na kulazwa kwa muda wa siku tatu. Wakati akiwa hospitalini, ndugu waliamua kuzika miili ya wazazi wake kwani iliharibika sana. Ilikuwa huzuni isiyo na kifani.

Kizi alipozinduka, alijikuta yuko hospitalini akiwa ametundikiwa dripu. Aliangalia huku na kule akidhani angeona mtu wa kumtua mzigo wa majonzi alioubeba moyoni mwake. Mara, nesi aliingia na kuanza kuongea naye, "Kizi, unajisikiaje? Hii dripu imekwisha. Ngoja niitoe." Kizi aliitikia na kuuliza kwa upole, "Ninajisikia vizuri. Samahani nesi, leo ninaweza kuruhusiwa kurudi nyumbani?" Nesi alimjibu, "Kama unaendelea vizuri, daktari anaweza kukuruhusu. Usiwe na wasiwasi." Punde si punde, daktari wa zamu aliingia wodini. Baada ya kupata taarifa ya maendeleo ya Kizi, alimruhusu kurudi nyumbani. Ndugu yake, aitwaye Hato, aliyekuwa nje ya wodi, aliitwa kwenda kumchukua.

Kizi alijawa na huzuni nyingi. Alijiona kama hana thamani ya kuishi tena duniani. Ama kweli c*hozi ni kiwakilishi cha maneno ambayo moyo hauwezi kuongea*. Walirudi nyumbani kwa kutumia usafiri wa umma, jambo lililomfanya Kizi ajisemee kimoyomoyo, "Nimeanza maisha ambayo sikuyazoea. Nilikuwa situmii usafiri wa umma. Leo nimeupanda usafiri huu. Ama kweli *maisha ni mlima mrefu*."

Walipofika kituoni, walishuka kwenye basi na kuelekea nyumbani kwa baba yake mdogo. Kizi aliuliza, "Hato, kwa nini usinipeleke nyumbani kwetu unanipeleka kwenu?" Hato akamjibu, "Kwa sababu kule kwenu kuna wageni wengi waliokuja kwenye msiba, na wewe unahitaji kupumzika." Kizi alikubali kwa shingo upande kwenda kwa baba yake mdogo.

*Kila lenye mwanzo halikosi kuwa na mwisho*. Baada ya msiba, ndugu wote walirudi nyumbani kwao. Kizi alikabidhiwa kwa baba yake mdogo kama mlezi. Hata hivyo, aliomba kukaa kwenye nyumba yao kwani aliona maisha ya huko kwa baba yake mdogo ni duni. Baba yake mdogo alimsihi abaki kwa muda nyumbani kwake hadi kipindi cha maombolezo kitakapokwisha. Kizi alikataa na kwenda kuishi katika nyumba yao ingawa hakuwa na fedha za kutumia. Alipokuwa huko, alitumia vitu vilivyoachwa na wazazi wake mpaka fedha za mirathi zilipotoka. Hata hivyo, fedha hizo *hazikufua dafu* kwani hakuwa na elimu ya utunzaji fedha. Zilipukutika mithili ya majani yapukutikayo mtini wakati wa kiangazi. Fedha hizo zilipoisha, Kizi aliishi maisha magumu sana. Hali hiyo ilisababisha Kizi *akate tamaa* na kuamua kujiingiza katika utumiaji wa dawa za kulevya. Alidhani anapoteza mawazo kumbe anaangamia.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 106 07/03/2022 16:51

Saa, siku, na miezi ikapita, Kizi akawa mwathirika wa dawa za kulevya. Siku moja akiwa amejilaza chini ya mti karibu na nyumba yao, alisikia kishindo cha mtu; akakurupuka akidhani ni polisi wamekuja kumkamata. Kumbe alikuwa rafiki yake aliyeitwa Muba. Wakaanza mazungumzo.

**Muba**: Habari za siku nyingi rafiki yangu? Pole sana kwa msiba wa wazazi wako! Taarifa za msiba nilizipata nikiwa safarini.

**Kizi**: (*Huku akitoa machozi*) Asante rafiki yangu! Wazazi wangu wameniachia mtihani mkubwa sana. Nilizoea maisha ya raha. Sasa hayapo tena. Nilidharau watu kwa sababu tulikuwa tunaishi maisha ya kifahari. Nilisahau kuwa utajiri ni wa wazazi wangu; wakiondoka, wanaondoka nao. Nilitakiwa kusoma kwa bidii ili nipate elimu ya kunisaidia kuboresha maisha yangu. Jamani nimeumbuka mie eeeh! (*Aliangua kilio*.)

**Muba**: (*Anambembeleza kwa kumpigapiga mabegani.*) Usilie rafiki yangu. *Kazi ya Mungu haina makosa*. Kilichobaki ni kuwaombea, wapumzike mahali pema peponi. Pia, ninakuombea Mungu akutie nguvu, akubariki uweze kujikimu kimaisha. Hii itakusaidia kuachana na dawa za kulevya. Dawa za kulevya zina madhara mengi. Unaweza kufungwa jela na uwezo wa kufikiri unaweza kupungua kwa sababu akili inadumaa. Pia, unaweza kupata maambukizi ya magonjwa au hata kupoteza maisha. Wewe ni mtu muhimu sana katika taifa hili. Dawa za kulevya zinaathiri nguvukazi ya taifa; ndiyo maana serikali inazipiga vita.

**Kizi**: Muba, mimi sikupenda kutumia dawa za kulevya, ila toka wazazi wangu waondoke duniani, ninaona kama sina maana katika dunia hii. Hata hivyo, ninakubaliana na elimu uliyonipatia kuhusiana na madhara ya utumiaji wa dawa za kulevya. Sasa, nitafanyaje rafiki yangu ili nisiendelee kutumia dawa hizi?

**Muba**: Kama uko tayari, nikupeleke kwenye kituo cha ushauri na unasihi, kitengo kinachoshughulikia watu walioathirika kwa dawa za kulevya. Hao watakupa ushauri mzuri utakaokufaa. Baada ya kutoka huko, nitakupa mtaji wa kukuwezesha kuanzisha biashara. Nitakuongoza ili uwe mjasiriamali kama mimi, kwani *kuvunjika kwa koleo si mwisho wa uhunzi*.

Kizi alikubaliana na mawazo ya rafiki yake. Akapelekwa kupatiwa unasihi. Hatimaye, alibadilika na kuungana na rafiki yake, Muba, mpaka akawa mwalimu kwa wengine. Ama kwa hakika, *akufaaye kwa dhiki ndiye rafiki wa kweli*.

## Maswali

1. Mwandishi ana maana gani anaposema, "Kizi alikuwa kifungua mimba na kitinda mimba kwa mama yake?"
2. Kwa nini Kizi alijuta baada ya wazazi wake kufariki?
3. Kama ungekuwa mzazi wa Kizi, ungemlea kama alivyolelewa na wazazi wake? Eleza sababu za jibu lako.
4. Kwa nini Muba alimshauri Kizi aende kwenye kituo cha ushauri na unasihi kabla ya kuungana naye kwenye ujasiriamali?
5. Kama ungepewa nafasi ya kumshauri Kizi, ungemshauri nini?
6. Fafanua mafunzo uliyoyapata kutokana na hadithi uliyoisoma.
7. Eleza maana ya maneno na semi zifuatazo kama zilivyotumika katika hadithi uliyoisoma.
   (a) bweteka
   (b) zirai
   (c) kifani
   (d) uhunzi
   (e) kitengo
   (f) kupiga domo
   (g) kufua dafu
   (h) kwa shingo upande
   (i) kuvunjika kwa koleo, si mwisho wa uhunzi
   (j) akufaaye kwa dhiki, ndiye rafiki wa kweli
   (k) zilipukutika mithili ya majani yapukutikayo mtini wakati wa kiangazi

## Kazi ya 6.6

**Soma kimya hadithi ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**

"Ndugu wazazi, kumbe safari yenu inahusu harusi ya Lui?" Mwalimu mkuu aliwauliza wazazi. "Ndiyo!" Wazazi walijibu kwa pamoja bila aibu. "Inategemewa kufungwa lini?" Mkuu wa shule aliendelea kuhoji. "Harusi hii ilikuwa ifanyike wakati Lui atakapomaliza kidato cha nne, lakini ametufanyia uhuni na vituko visivyoelezeka. Nasi sasa tunachukiwa na kudharauliwa na kila mtu hapa kijijini. Hii imetuudhi sana. Tumetungiwa nyimbo na kufanyiwa kila shutuma. Hatuna raha; hivyo, tumeona bora tuje kukuomba umfukuze shule ili kiburi kimwishe. Nasi tupo tayari hata kukulipa kiasi chochote cha fedha ukitimiza haja yetu hii," Mzee Loko alieleza.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 108 07/03/2022 16:51

Muda wote mkuu wa shule alikuwa akimtazama Mzee Loko kwa chati sana. Kisha, akauliza swali la kuchochea mazungumzo zaidi, “Lui ana kiburi kumbe?” Mama Lui hakutaka hilo limpite; himahima akatoa maelezo yake, “Mama wee! Lui usimwone hivi. Mwanangu hataki kufuata utamaduni wetu wa kuolewa. Anataka eti achague mchumba mwenyewe. Haoni kama mahari ni kitu cha msingi. Kiburi hicho kinatokana na elimu mliyompa. Sasa ameharibika. Anafanya apendavyo. Hii elimu gani isiyojali adabu wala utii?” Mama Lui alimaliza kuongea huku jasho na machozi yakimtoka.

Baada ya kuwasikiliza, mwalimu aliona awaelimishe kwanza kabla hajawatolea kauli ya mwisho. Alikwishatambua kwamba wazazi wa Lui walikuwa wamepitwa na wakati. Kila upya wa mawazo waliuita kiburi.

(Imeboreshwa kutoka TET, 1996)

## Maswali

1. Bainisha mambo matatu ya kuzingatia wakati wa kufupisha habari.
2. Kwa maneno yasiyopungua 50 na yasiyozidi 60, fupisha habari uliyoisoma.
3. Eleza faida unazozipata kutokana na kufupisha habari.

**Zingatia**

Unapomaliza kusoma kifungu cha habari, unaweza kueleza jambo linalosemwa na mwandishi kwa kuandika kwa maneno yako ufupisho wa kile ulichokisoma na kukielewa. Kwa hiyo, unatakiwa kuisoma habari kwa makini na kubainisha mawazo makuu yaliyomo. Vilevile, unapaswa kuyapanga mawazo hayo kwa mtiririko wenye mantiki kwa kuyaunganisha na kuyaeleza kwa ufupi bila kupotosha maana ya msingi ya habari hiyo. Pia, wakati wa kufupisha habari, ni muhimu kuzingatia njeo, kauli, na nafsi kama zilivyotumiwa katika matini uliyoisoma au kuisikiliza. Aidha, unapaswa kuzingatia matumizi sahihi ya alama za uakifishaji. Baada ya kufupisha habari, kumbuka kusoma ufupisho wako ili kurekebisha makosa yanayoweza kujitokeza.

Ufupisho ni njia mojawapo ya kudhihirisha kuwa umekielewa ulichokisoma. Vilevile, ukifupisha habari au hadithi mbalimbali, utakuza uwezo wako wa kupanga mawazo kimantiki na kuyaeleza kwa ufupi.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 109 07/03/2022 16:51

## Zoezi la 6.2

1. Fafanua mambo ya kuzingatia katika ufahamu wa kusoma.
2. Eleza kanuni za usomaji bora.
3. Kwa nini ni muhimu kuzingatia matumizi sahihi ya alama za uakifishaji wakati wa kusoma habari?

## Ufahamu wa kuona

### Kazi ya 6.7

**Chunguza picha ifuatayo, kisha jibu maswali yanayofuata.**



### Maswali

1. Unaona nini katika picha hiyo? Fafanua.
2. Kwa nini mtu anayeonekana kwenye picha ameshikilia mguu wake?
3. Kama ungekuwa wewe, ungefanya nini katika mazingira hayo?
4. Watu wanaoonekana kwenye picha wanafanya nini?
5. Andika kifungu cha habari kisichozidi maneno 80 kutokana na picha uliyoichunguza.




KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 110 07/03/2022 16:51

**Zingatia**

Ufahamu wa kuona huweza kujengwa kwa kutazama vitu, kuvichunguza, au kushuhudia matukio, kisha kutafakari kwa lengo la kupata ujumbe. Katika maisha ya kila siku, tunapata uelewa kwa kuona vitu au mambo mbalimbali, kuyatafakari, na kuweza kuyatolea maelezo pale yanapohitajika. Matukio mengine huweza kuhifadhiwa kwa picha. Ukichunguza picha hizo, unaweza kupata ujumbe na kuusimulia kwa maandishi au mazungumzo kutokana na ulichokiona. Unapochunguza, unatakiwa kuwa makini kutafakari kwa kina kile unachokiona ili kuweza kukieleza kwa usahihi bila kupotosha maana. Wakati mwingine, ni vizuri kuuliza na kupata ufafanuzi ili uweze kutoa maelezo yaliyo sahihi. Hali kadhalika, katika matukio, unaweza kudadisi zaidi na kupata uelewa wa kina.

## Kazi ya 6.8



Tembelea mazingira ya soko au gulio yaliyopo katika eneo unaloishi. Chunguza namna usawa wa jinsia unavyozingatiwa au kutozingatiwa kutokana na shughuli zinazofanyika hapo. Andika habari yenye maneno yasiyopungua 250 kuhusu ulichokibaini katika uchunguzi wako.

## Zoezi la marudio

1. Jibu maswali yafuatayo kwa kuchagua herufi ya jibu sahihi:
   (i) Ufahamu unaweza kujengwa kupitia vitendo vya ...............
      (a) kusikia, kutenda, na kuona
      (b) kusoma, kusikia, na kutenda
      (c) kuona, kusikia, na kusoma
      (d) kuona, kutenda, na kusoma kwa makini
      (e) kuona, kusikia, na kutenda kwa makini

   (ii) Miongoni mwa mambo muhimu ya kuzingatia katika ufahamu ni ...............
      (a) kujibu maswali ya kuchagua
      (b) kuwa makini na jambo unalotaka kulifahamu
      (c) kutoa maelezo ya kina kuhusu wahusika
      (d) kuchambua kwa kina habari uliyopewa
      (e) kutoa mifano inayoeleweka



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 111 07/03/2022 16:51

(iii) Sentensi ipi kati ya hizi zifuatazo inaeleza ukweli kuhusu ufupisho wa kusoma?
  (a) Unapofupisha habari, unatakiwa kuzingatia alama za uakifishaji tu.
  (b) Unapofupisha habari, unatakiwa kuandika kwa muhtasari.
  (c) Unapofupisha habari, unatakiwa kuonesha wahusika wote.
  (d) Unapofupisha habari, hutakiwi kuandika neno lolote linalotokana na habari ya awali.
  (e) Unapofupisha habari, unatakiwa kuandika maneno yaleyale ili usipoteze maana iliyokusudiwa.

(iv) Alikwenda dukani kununua kalamu, madaftari, na rula. Andika ufupisho wa sentensi hii ...............
  (a) Alikwenda dukani kununua vifaa vya kuandikia.
  (b) Alikwenda dukani kununua samani za shule.
  (c) Alikwenda dukani kununua malighafi.
  (d) Alikwenda dukani kununua baadhi ya vifaa.
  (e) Alikwenda dukani kununua vifaa vya shule.

(v) Usomaji upi husaidia kupima uwezo wa kutamka maneno kwa ufasaha na kutumia lafudhi ya lugha husika?
  (a) Kusoma kwa burudani
  (b) Kusoma kwa sauti
  (c) Kusoma kimya
  (d) Kusoma kwa makini
  (e) Kusoma kwa ziada

2. Oanisha maelezo yaliyopo katika Orodha **A** na dhana zilizopo katika Orodha **B** kwa kuandika herufi ya jibu sahihi.

| **Orodha A** | **Orodha B** |
|---|---|
| (i) Huzingatia matamshi sahihi ya maneno na nguvu ya utamkaji wa silabi zenye mkazo | A. kusoma kwa burudani |
| (ii) Kusoma juujuu bila mazingatio | B. kusoma kwa ziada |
| (iii) Kusoma bila kutoa sauti kwa ajili ya kupata ufahamu | C. kusoma kwa sauti |
| (iv) Kusoma kwa ajili ya kujiburudisha na kupata maarifa yanayohusu jamii | D. kusoma kimya |
| (v) Kusoma kwa ajili ya kujipatia maarifa zaidi | E. kusoma kipurure |
| | F. kusoma kwa ajili ya ufupisho |
| | G. kusoma kwa harakaharaka |

3. Jadili kauli kwamba "Wanafunzi wanapaswa kujikita katika ufahamu wa kusoma kimya tu kwa kuwa unajitosheleza".
4. Kwa nini ni muhimu kujifunza kuandika ufupisho?
5. Andika habari yenye maneno yasiyopungua 250 kuhusu tukio lolote ulilowahi kulishuhudia.
6. Fafanua mambo ya kuzingatia katika ufahamu wa kusoma.
7. Kwa kutumia mifano halisi, tofautisha ufahamu wa kusikiliza na wa kusoma.
8. Ufahamu una umuhimu gani katika maisha yako ya kila siku?
9. Unafikiri ni changamoto gani unaweza kuzipata unapofupisha habari ya kusikiliza?



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 113 07/03/2022 16:51

## Faharasa

**Adhimu** enye thamani au enye ubora wa kipekee

**Ajenda** orodha ya mambo yatakayozungumzwa kwenye mkutano au kikao

**Akidi** idadi ya wajumbe wa mkutano inayotosha kuruhusu mkutano kufanyika na maamuzi kuwa halali

**Bashasha** furaha, uchangamfu au ucheshi

**Chakachua** fanya ujanja au hila ili kupata au kubadilisha kitu kwa lengo la kupata faida

**Data** taarifa zinazotumiwa kuelezea au kuthibitisha hoja

**Dijiti** mfumo unaotumia namba kufichua alama za kielektroni zilizofichwa ili ziweze kuonekana kwenye televisheni, kompyuta, simu, au intaneti

**Dondoo** kipengele cha ajenda ya mkutano

**Duni** enye thamani ndogo, hafifu

**Fariki** tokwa na uhai, kata roho, kufa

**Fuadi** moyo

**Hatamu** madaraka, uongozi au utawala

**Hisa** kiwango kinachotolewa kama sehemu ya mtaji katika biashara

**Jinai** kosa la uhalifu

| | |
|---|---|
| **Kinyonyi** | kifaa kidogo kinachotumika kuhifadhia au kuhamishia data kwenye kompyuta |
| **Kipimajoto** | kifaa kinachotumika kupima halijoto katika mwili |
| **Kipurure** | bila umakini |
| **Kisimbuzi** | kifaa kinachofichua alama za kielektroni zilizofichwa ili ziweze kusikika na kuonekana kwenye simu, televisheni, redio, faksi, na intaneti kwa kutumia mfumo wa kidijiti |
| **Kitunduizi** | kwa makini |
| **Kujikimu** | kufanya shughuli za kujipatia mahitaji yako ya maisha |
| **Lahaja** | tofauti katika matamshi, maumbo, na matumizi ya maneno baina ya jamii za wazungumzaji wa lugha yenye asili moja |
| **Liturujia** | utaratibu wa kuendesha ibada katika dini ya Kikristo |
| **Maadhura** | mtu au watu walioomba udhuru, aghalabu, katika kikao au mkutano |
| **Makala** | habari zilizoandikwa kuelezea jambo |
| **Manamba** | wafanyakazi wahamiaji katika mashamba makubwa |
| **Matini** | kifungu cha habari kilichoandikwa |
| **Mawanda** | upana au kikomo cha jambo fulani |
| **Mbiu** | wito |



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 115 07/03/2022 16:51

**Rafu** kabati lililo wazi la kuhifadhia vitu kama nguo na vitabu, pengine huitwa shubaka

**Rikwama** kifaa chenye gurudumu moja au zaidi kinachosukumwa au kukokotwa ambacho hutumika kubeba mizigo

**Ruksa** idhini inayotolewa na mtu au chombo chenye mamlaka kwa mtu, watu, au chombo ili kutekeleza jambo fulani, pengine huitwa ruhusa

**Rupia** sarafu ya asili ya Kihindi iliyokuwa ikitumika katika makoloni ya Mwingereza ya Afrika Mashariki

**Satelaiti** chombo kilichotengenezwa na kuwekwa angani kuzunguka dunia au sayari yoyote ili kukusanya taarifa kwa ajili ya mawasiliano

**Sawijika** onesha hali ya kukosa nuru au furaha kwa sababu ya njaa, maradhi au kwa kusongwa na masaibu mbalimbali katika maisha

**Silabi** sehemu ya neno ambayo huundwa na irabu peke yake au konsonanti na irabu ambayo hutamkwa mara moja kama fungu moja la sauti

**Tahajia** uwasilishaji wa sauti kwa herufi katika maandishi

**Tasfida** aina ya usemi ambayo hutumia lugha ya staha au ya kificho badala ya kutumia moja kwa moja lugha ya matusi au yenye kukera ikizungumzwa hadharani; pia tasifida

**Tini** kazi anazoandika mwanafunzi wakati wa masomo au kumbukumbu za somo anazotumia mwalimu kufundishia darasani

**Tovuti** mahali katika mtandao penye ukurasa mmoja au zaidi panapoweza kutolewa taarifa kuhusu jambo maalumu

**Uakifishaji** uwekaji wa alama za uandishi kama vile nukta, mkato, na alama ya kuuliza katika maandishi

**Ufisadi** ubadhirifu au wizi wa mali zilizopo katika dhamana yako kwa ajili ya kujinufaisha kibinafsi

**Ukata** hali ya kukosa fedha

**Walalahoi** watu wenye kipato cha chini

**Yakuti** kito chenye rangi ya zambarau iliyokaribia kuwa kama rangi ya waridi iliyofifia



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 117 07/03/2022 16:51

# Bibliografia

Baraza la Kiswahili la Taifa (2017). *Mwongozo kwa Waandishi wa Kiswahili Sanifu*. Dar es Salaam: TUKI na BAKITA.

Baraza la Kiswahili la Taifa (2017). *Kamusi Kuu ya Kiswahili*, *Toleo la 2*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Hamawand, Z. (2011). *Morphologhy in English, Word Formation in Cognitive Grammar*. New York: Continuum International Publishing Group.

Hassan, F.F. (2021). *Mofolojia ya Kiswahili*. Dar es Salaam: Maccony Printing Press.

Kane, T.S. (2000). *Oxford Essential Guide to Writing*. New York: Oxford University Press.

Kiango, J.G. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Utungaji II*. Dar es Salaam: TUKI.

Kihore, Y.M., Massamba, D.P.B. & Msanjila, Y.P. (2003). *Sarufi Maumbo ya Kiswahili Sanifu* (*SAMAKISA*): *Sekondari na Vyuo*. Dar es Salaam: TUKI.

King'ei, K. (2014). *Taaluma ya Uandishi.* Nairobi: The Jomo Kenyatta Foundation.

Komba, S.M. (1977). *Uwanja wa Mashairi*. Dar es Salaam: Ben and Company Ltd.

Massamba, D.P.B. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Ufahamu na Ufupisho I.* Dar es Salaam: TUKI.

Massamba, D.P.B. (2009). *Stadi za Lugha ya Kiswahili: Ufahamu na Ufupisho II*. Dar es Salaam: TUKI.

Matei, A.K. (2008). *Darubini ya Sarufi: Ufafanuzi Kamili wa Sarufi ya Kiswahili*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.

Mbaabu, I. (2007). *Historia ya Usanifishaji wa Kiswahili*. Dar es Salaam: TUKI.

Mgullu, R.S. (2001). *Mtalaa wa Isimu: Fonetiki, Fonolojia, na Mofolojia ya Kiswahili*. Nairobi: Longhorn Publishers Ltd.

Mohamed, M.A. & Mohamed, S.J. (2014). *Kamusi ya Visawe - Swahili Dictionary of Synonyms*. Nairobi: East African Publishers Ltd.

Mulokozi, M.M. (2017). *Utangulizi wa Fasihi ya Kiswahili*. Dar es Salaam: KAUTTU.

Plag, I. (2002). *Word Formation in English*. Cambridge: Cambridge University Press.

Shiach, D. (2009). *How to Write Essays*. United Kingdom: How to Content.

Taasisi ya Elimu Tazania (1996). *Kiswahili Kidato cha Nne.* Dar es Salaam: Oxford University Press.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Kiswahili kwa Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita: Fasihi*. Dar es Salaam: TET.

Taasisi ya Elimu Tanzania (2019). *Kiswahili kwa Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Tano na Sita: Lugha na Sarufi*. Dar es Salaam: TET.

Taasisi ya Taaluma za Kiswahili (2014). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu, Toleo la 3*. Nairobi: Oxford University Press.

Taasisi ya Uchunguzi wa Kiswahili (2003). *Makala za Semina ya Kimataifa ya Waandishi wa Kiswahili III: Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.

Wamitila, K.W. (2008). *Kanzi ya Fasihi: Misingi ya Uchanganuzi wa Fasihi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Ltd.

Wamitila, K.W. (2016). *Kichocheo cha Ushairi*. Nairobi: Vide~Muwa Publishers Ltd.

Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi (2005). *Muhtasari wa Kiswahili kwa Shule za Sekondari Kidato cha I-IV.* Dar es Salaam: Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi.



KISWAHILI KIDATO CHA 4_ LANGUAGE.indd 119 07/03/2022 16:51

Kiswahili Shule za Sekondari Kitabu cha Mwanafunzi Kidato cha Nne

ISBN 978-9987-09-396-0

*Mali ya Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Hakiuzwi*